SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

## OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

# RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2021

OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI
S.L.P 258, Maisara - Zanzibar, Simu: +255 24 2234009, Nukushi: +255 24 2234009
Baruapepe: info@ocagz.go.tz, Tovuti: www.ocagz.go.tz

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU**
**WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR**

# RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

# KUHUSU UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2021

Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Kifungu cha 112 pamoja na Sheria Nambari 12 ya mwaka 2016 ya Usimamizi wa Fedha za Umma kifungu namba 123 (4) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa za ukaguzi huo kila mwaka.

## DIRA

Kuwa na Taasisi ya ukaguzi iliyo huru na inayoongoza katika kusimamia uwajibikaji na uwazi

## DHAMIRA

Kusimamia uwajibikaji katika Taasisi za umma kwa kufanya ukaguzi wa hesabu wenye kuleta tija na kulihakikishia Taifa kwamba rasilimali za Umma zitatumika kama ilivyokusudiwa

**Katika kuhakikisha uwazi na uwajibikaji unapatikana katika matumizi mazuri ya rasilimali za umma Ofisi hii inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:-**

### Uaminifu

Kuhakikisha Ofisi ina kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala bora unaozingatia sheria.

### Uadilifu

Kuwa ni Ofisi inayozingatia misingi ya uadilifu kwa kutoa huduma bila ya upendeleo.

### Kuwa Huru

Kuwa ni Ofisi iliyo huru na inayotekeleza majukumu yake bila ya kuingiliwa kwa mujibu wa sheria

### Uwezo na Taaluma ya Ukaguzi

Kuwa ni Ofisi yenye kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora wa kiwango cha juu.

### Kutunza Siri

Kuwa ni Ofisi yenye kutunza siri katika utekelezaji wa kazi zake.

### Uwazi na Uwajibikaji

Kutoa taarifa sahihi na muhimu kwa wadau ili kuweza kupima uwajibikaji katika matumizi bora ya rasilimali za Umma.

## YALIYOMO

YALIYOMO....................................................................................V

ORODHA YA MAJADWELI.........................................................................VIII

VIFUPISHO....................................................................................VII

SHUKURANI....................................................................................X

DIBAJI.......................................................................................XIII

MUHTASARI....................................................................................XV

**SURA YA KWANZA**...........................................................................1

TAARIFA YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO.....................................1

1.0 UTANGULIZI...............................................................................1

1.1 UWANZISHWAJI WA OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU KISHERIA..........................................................................1

1.2 MAJUKUMU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI.....................................................................................2

1.3 UPEO NA MADHUMUNI YA UKAGUZI..................................................3

1.4 VIWANGO VYA UKAGUZI VILIVYOTUMIKA..........................................3

1.5 MBINU ZA UKAGUZI ZILIZOTUMIKA..................................................3

**SURA YA PILI**..............................................................................5

2.0 UWASILISHAJI WA HESABU ZA MIRADI YA MAENDELEO.......................5

2.1 TATHMINI YA UFANISI WA MIRADI YA MAENDELEO.........................6

2.2 DOSARI ZA UJUMLA ZILIZOBAINIKA KATIKA USIMAMIZI WA FEDHA.6

2.3 MAPENDEKEZO YA JUMLA.............................................................9

**SURA YA TATU**.............................................................................10

3.0 MIRADI ILIYOTEKELEZWA KATIKA SEKTA YA ELIMU...........................10

3.1 MRADI WA KUENDELEZA ELIMU MBADALA AWAMU YA II (ALSD II).10

3.2 MRADI WA UJENZI NA UNUNUZI WA VIFAA KWA AJILI YA SKULI ZA SEKONDARI ZANZIBAR....................................................................12

3.3 MRADI WA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA KWA ELIMU (GPE II).......14

3.4 MRADI WA UIMARISHAJI WA ELIMU YA SEKONDARI ZANZIBAR (ZISP)........................................................................................19

3.5 MPANGO WA LISHE MASHULENI (HGSFP)....................................24

3.6 MRADI WA UJENZI WA DAHALIA YA WANAUME KATIKA SKULI YA SEKONDARI YA MOH'D JUMA PINDUA - PEMBA.............................26

**SURA YA NNE**............................................................................30

4.0 MIRADI ILIYOTEKELEZWA KATIKA SEKTA ZA FEDHA NA MIPANGO MIJI..........................................................................................30

4.1 MRADI WA MABORESHO YA USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA (PFMRP)........................................................................................30

4.2 MRADI WA HUDUMA ZA JAMII MIJINI ZANZIBAR (ZUSP..................33

4.3 MRADI WA UJENZI WA UKUMBI WA MIKUTANO WA UMOJA NI NGUVU - PEMBA...............................................................................40

4.4 MIRADI YA UJENZI WA MAHANGA YA KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) - PEMBA........................................................49

**SURA YA TANO**..........................................................................58

5.0 MIRADI ILIYOTEKELEZWA KATIKA SEKTA YA UCHUMI WA BULUU, KILIMO NA MAMBO YA KALE..........................................................58

5.1 MRADI WA MAMLAKA YA UVUVI WA BAHARI KUU ZANZIBAR (SWIOFISH1 - GEF GRANT)..........................................................58

5.2 MRADI WA MAMLAKA YA UVUVI WA BAHARI KUU ZANZIBAR (SWIOFISH1 – IDA)..................................................................63

5.3 MRADI WA UZALISHAJI WA MPUNGA (ERPP)................................66

5.4 MRADI WA UHIFADHI WA ENEO LA KIHISTORIA LA MKAMANDUME PEMBA....69

5.5 MRADI WA MATUKIO KATIKA SEHEMU MBALIMBALI ZA UTALII ZANZIBAR....81

**SURA YA SITA**....98

6.0 MIRADI ILIYOTEKELEZWA KATIKA SEKTA ZA AFYA....98

6.1 MRADI WA KUDHIBITI VVU, KIFUA KIKUU NA UKOMA ZANZIBAR (ZIHTLP)....98

6.2 MRADI WA KUTOKOMEZA MALARIA ZANZIBAR (ZAMEP)....101

6.3 MRADI WA UJENZI WA JENGO LA MAMA NA MTOTO - HOSPITALI YA CHAKE CHAKE PEMBA....106

**SURA YA SABA**....112

7.0 MIRADI ILIYOTEKELEZWA KATIKA SEKTA ZA MIUNDOMBINU NA NISHATI....112

7.1 MRADI WA UIMARISHAJI WA SEKTA YA UMEME ZANZIBAR....112

7.2 MRADI WA KUSAIDIA SEKTA YA UCHUKUZI (TSSP)....114

## ORODHA YA MAJADWELI

**Jadweli Nambari 1 :** Uwasilishaji wa hesabu za Miradi ya Maendeleo.......5

**Jadweli Nambari 2 :** Kuwepo kwa ongezeko la fedha za mradi...............12

**Jadweli Nambari 3 :** Utekelezaji wa Mradi kinyume na bajeti iliyopangwa....17

**Jadweli Nambari 4 :** Kutotekelezwa kwa Shughuli za Mradi zilizopangwa.....18

**Jadweli Nambari 5 :** Taarifa ya fedha za mradi....................................21

**Jadweli Nambari 6 :** Kutokuwasilishwa kwa makato ya kodi ya zuio.........27

**Jadweli Nambari 7 :** Ujenzi wa Dahalia kinyume na makubaliano ya mkataba........................................................28

**Jadweli Nambari 8 :** Makadirio ya mapato na matumzi ya Mradi wa PFMRP...........................................................32

**Jadweli Nambari 9 :** Malipo yasiyokuwa na vielelezo.............................32

**Jadweli Nambari 10 :** Taarifa za fedha za mradi..................................36

**Jadweli Nambari 11:** Ujenzi wa Ukumbi kinyume na makubaliano ya mkataba........................................................43

**Jadweli Nambari 12:** Kodi iliyostahiki kulipwa Serikalini kwa mujibu wa mkataba........................................................44

**Jadweli Nambari 13:**Kodi iliokatwa kwa mujibu wa hati za malipo..........45

**Jadweli Nambari 14:** Kodi halisi iliyowasilishwa..................................45

**Jadweli Nambari 15:**Kodi iliokatwa kwa mujibu wa hati za malipo...........46

**Jadweli Nambari 16:** Kodi halisi iliyowasilishwa..................................46

**Jadweli Nambari 17 :** Malipo ya fedha yaliokosekana kwa ukaguzi...........49

**Jadweli Nambari 18 :** Ununuzi wa vifaa vya Ujenzi...............................55

**Jadweli Nambari 19 :**Fedha zilizoombwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi.............................................................60

**Jadweli Nambari 20 :** Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa.....61

**Jadweli Nambari 21 :** Mafanikio mabaya ya matokeo ya haraka ya mradi....62

**Jadweli Nambari 22 :** Fedha zilizoombwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi..64

**Jadweli Nambari 23 :** Malipo kwa Wafanya watoa huduma ambao hawakusajiliwa..................................................65

**Jadweli Nambari 24 :** Kutokutekelezwa kwa baadhi ya shughuli za mradi....66

**Jadweli Nambari 25 :** Taarifa ya fedha za mradi...................................68

**Jadweli Nambari 26 :** Utekelezaji wa Mradi kinyume na Bajeti................69

**Jadweli Nambari 27 :** Malipo ya kodi ya VAT yasiokuwa na vielelezo.........71

**Jadweli Nambari 28 :** Kutokulingana kwa bei ya ununuzi wa vifaa ukilinganisha na bei halisi ya sokoni........................................74

**Jadweli Nambari 29 :** Vifaa vilivyonunuliwa ambavyo havikuonekana.......75

**Jadweli Nambari 30 :** Malipo ya kodi ya VAT yasiokuwa na vielelezo.........78

**Jadweli Nambari 31:**Malipo ya kodi ya VAT yasiokuwa na vielelezo..........80

**Jadweli Nambari 32 :** Mapato na Matumizi..........................................82

**Jadweli Nambari 33 :** Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa...92

**Jadweli Nambari 34 :** Taarifa ya fedha za mradi...................................92

**Jadweli Nambari 35 :** Vifaa ambavyo havikurikodiwa katika daftari la ghalani..........................................................99

**Jadweli Nambari 36 :** Matumizi yaliyofanyika nje ya bajeti...................101

**Jadweli Nambari 37 :** Kutokutekelezwa kwa baadhi ya shughuli za Mradi..........................................................102

**Jadweli Nambari 38 :** Uingiaji wa fedha za mradi................................104

**Jadweli Nambari 39 :** Orodha ya fidia za waliothirika na mradi (PAA).......105

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **ADB** | Benki za Maendeleo ya Afrika |
| **ADF** | Mfuko wa Maendeleo Afrika |
| **AFD** | Shirika la Maendeleo la Ufaransa |
| **BADEA** | Shirika la Maendeleo ya Uchumi Barani Afrika |
| **CAG** | Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali |
| **DOEM** | Idara ya Nishati na Madini |
| **DSFA** | Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu |
| **ERPP** | Mradi wa Kuendeleza Uzalishaji wa Mpunga |
| **GAFSP** | Mpango wa Kilimo na Usalama wa Chakula Duniani |
| **GPE** | Ushirikiano wa Kimataifa wa Elimu |
| **IDA** | Shirika la Kimataifa la Maendeleo |
| **IPSAS** | Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi katika Sekta ya Umma |
| **MFDB** | Benki ya Maendeleo ya Afrika |
| **MOIC** | Wizara ya Miondo Mbinu Na Mawasiliano |
| **PFMRP** | Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma |
| **SIDA** | Shirika la Maendeleo la Kimataifa |
| **TANROADS** | Wakala wa Barabara Tanzania |
| **TSSP** | Mradi wa Kusaidia Sekta ya Usafirishaji |
| **USD** | Dola ya Kimarekani |
| **WB** | Benk ya Dunia |
| **WEMA** | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali |
| **ZECO** | Shirika la Umeme Zanzibar |
| **ZMC** | Baraza la Manispaa |

## SHUKURANI

Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zake za mara kwa mara anazoendelea kuzichukuwa ikiwa ni pamoja na kuweka msisitizo na kutoa maelekezo katika kufanya marekebisho juu ya dosari mbali mbali zinazobainishwa katika Ripoti za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali pamoja na hatua anazoendelea kuzichukua kutokana na hoja za ukaguzi zinazoibuliwa kuhusu matumizi ya fedha pamoja na usimamizi wa rasilimali za Umma.

Shukurani zangu za dhati ziende kwa Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa kujitolea kwa dhati kujadili na kutoa maelekezo pamoja na kufuatilia hatua zinazochukuliwa na Serikali kutokana na dosari zilizojitokeza na kuibuliwa katika Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kusimamia uwajibikaji na utekelezaji wa majukumu ya watendaji katika sekta mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada mbali mbali zinazochukuliwa katika kuimarisha na kuijengea uwezo Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kutekeleza majukumu yake ya kikatiba.

Vile vile napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora pamoja na Bodi ya Utumishi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kusimamia maadili na nidhamu ya wafanyakazi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kupelekea kuimarika kwa nidhamu na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu ya kazi za ukaguzi.

Kwa namna ya kipekee niwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT), Tanzania Audit Corporation (TAC Associates), Claritas International pamoja na Ernst & Young (EY) kwa kufanya kazi za ukaguzi kwa mashirikiano na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na juhudi zao mbali mbali walizozichukuwa hadi kukamilika kwa ripoti hii.

Mwisho, niwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyengine kuanzia kazi za ukaguzi, ufuatiliaji wa maeneo mbali mbali yaliyokaguliwa hadi kukamilika kwa ripoti hii ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Aidha, nitakuwa mchache wa shukurani kama sitatambua jukumu la vyombo mbali mbali vya habari kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuutambulisha Umma juu ya kazi zinazofanywa na Ofisi ya Mdhibiti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambapo matokeo na mapendekezo ya kazi hizo huwasilishwa kwa jamii kupitia kazi za ukaguzi zilizofanywa na Ofisi hii.

Natumia fursa hii, kuwasihi wafanyakazi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuendelea kuwa na moyo wa dhati katika kufanya kazi kwa bidii na kuongeza mashirikiano kwa ajili ya siku zijazo ili kuendelea kudumisha nidhamu ya Ofisi ya Mdhibiti katika kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora, kuhimiza uwajibikaji na kuzingatia thamani ya fedha katika makusanyo ya fedha na matumizi ya rasilimali za Umma.

## DIBAJI



Ninafuraha kubwa ya kuwasilisha Ripoti ya Ukaguzi inayohusu Ukaguzi wa Taarifa za Miradi ya Maendeleo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2021. Wasilisho hilo ni kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Kifungu cha 112 pamoja na kifungu namba 123(4) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 ambapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa zake za ukaguzi huo kila mwaka. Taarifa hizo zitaelezea hali halisi ya mapato na matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Washirika wa Maendeleo kwa kuzingatia utekelezaji wa sheria mbali mbali zikiwemo Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016, Sheria Nambari 11ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 pamoja na sheria nyenginezo.

Kwa Mujibu wa Mamlaka niliyonayo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ni jukumu langu la kutoa taarifa huru, zilizosahihi na zilizojitosheleza kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusiana na usimamizi wa fedha pamoja na matumizi sahihi ya rasilimali za Umma na hatimae taarifa hizo kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi kwa hatua za utekelezaji. Nilifanya ukaguzi huu kwa kuzingatia Viwango kubalifu vya kitaifa na kimataifa vya Taasisi za Juu za Hesabu za Serikali (ISSAIs) vinavyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi (INTOSAI) ambazo zinahusu ukaguzi wa Sekta za Umma.

Ripoti hii imejumuisha mambo mbali mbali yaliyobainika katika ukaguzi nilioufanya wa Miradi ya Maendeleo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo katika ukaguzi huo jumla ya Miradi Ishirini (20) nimeikagua kwa Unguja na Pemba kwa lengo la kutoa tathmini halisi ya namna ya miradi mbali mbali ya Maendeleo inavyotekelezwa ili kuhakikisha kwamba taratibu,

kanuni na sheria zinazotumika katika usimamizi wa fedha na utekelezaji wa miradi hiyo zinafuatwa ipasavyo na kwamba fedha za miradi zinatumika kama ilivyokusudiwa ili kuwanufaisha wananchi wa Zanzibar kwa kupata maendeleo kutokana na utekelezaji wa miradi hiyo iliyofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Wahisani wa Maendeleo.

Kwa ujumla, ripoti hii inajumuisha miradi inayofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Wahisani wa maendeleo ambapo baadhi ya Wahisani hao ni pamoja na Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden (SIDA), Shirika la Kimataifa la Maendeleo (IDA), Mfuko wa Maendeleo Afrika (ADF), Shirika la Maendeleo ya Uchumi Barani Afrika (BADEA) n.k.

Ni matarajio yangu kuwa ripoti hii itasaidia Serikali na wadau mbali mbali wa miradi ya maendeleo kuweza kufanya tathmini iwapo fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo zimetumika kwa usahihi na kwa malengo yaliyokusudiwa. Vile vile kupitia ripoti hii Serikali itaweza kubaini kwa kiasi gani Maafisa Masuuli wanavyowajibika katika kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hatua wanazozichukua katika usimamizi wa miradi hiyo ili kuweza kupatikana tija na ufanisi kwa Wananchi wa Zanzibar.

Nichukue fursa hii kwa dhati kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein A. Mwinyi kwa jitihada zake anazoendelea kuzichukuwa katika kufuatilia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa lengo la kusimamia na kuimarisha uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za Umma hali inayopelekea kuimarika kwa Utawala Bora.

..........................................

**DKT. OTHMAN ABBAS ALI**

**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

**ZANZIBAR**

# MUHTASARI

Muhtasari wa matokeo ya ukaguzi wa Taarifa za Hesabu za Miradi ya Maendeleo yanayopaswa kuzingatiwa kwa umakini na Serikali, Baraza la Waakilishi, Maafisa Masuuli na Wadau wengine wa miradi ya maendeleo na kufuatiwa na mambo muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa miradi hiyo pamoja na muhtasari wa mapendekezo ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

Katika ukaguzi wa taarifa za fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021, jumla ya Wizara saba (7) ziliwasilisha taarifa za Hesabu za miradi ya maendeleo katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ambapo jumla ya Miradi Ishirini (20) ilikaguliwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, miradi hiyo imefadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Washirika wa maendeleo. Miradi hiyo ni kama ifuatayo;

(i) Mradi wa Kuendeleza Elimu Mbadala Awamu ya II (ALSD II),

(ii) Mradi wa Ujenzi na Ununuaji wa Vifaa kwa ajili ya Skuli za Sekondari Zanzibar (BADEA II), Mradi wa Ushirikiano wa Kimataifa kwa Elimu (GPE II)

(iii) Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Sekondari Zanzibar (ZISP), Mpango wa Lishe Mashuleni (HGSFP)

(iv) Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP)

(v) Mradi ya Huduma za Jamii Mijini Zanzibar (ZUSP)

(vi) Mradi wa Uzalishaji wa Mpunga (ERPP)

(vii) Mradi wa Kudhibiti VVU, Kifua Kikuu na Ukoma Zanzibar (ZIHTLP)

(viii) Mradi wa kutokomeza Malaria Zanzibar (ZAMEP)

(ix) Mradi wa Uimarishaji wa Sekta ya Umeme Zanzibar

(x) Miradi ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Zanzibar (SWIOFish1-GEF GRANT) na (SWIOFish1-IDA Loan)

(xi) Mradi wa kusaidia Sekta ya Uchukuzi (TSSP)

(xii) Mradi wa ujenzi wa Dahalia ya wanafunzi wa kiume katika Skuli ya Sekondari ya Moh'd Juma Pindua, Mradi wa Ujenzi wa jengo la Mama na Mtoto katika Hospitali ya Chake Chake

(xiii) Mradi wa Uhifadhi wa Eneo la Kihistoria la Mkamandume

(xiv) Mradi wa Ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano wa Umoja ni Nguvu pamoja

(xv) Mradi wa Ujenzi wa Mahanga ya Kikosi Maalum cha KMKM Pemba.

Ukaguzi wa Miradi ya maendeleo umebaini dosari mbali mbali ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi na watekelezaji wa miradi ili kuboresha utendaji wao katika siku zijazo.

Dosari zilizobainika zinahusu masuala ya usimamizi wa mapato na matumizi ya fedha za bajeti, mifumo ya ndani, pamoja na kutokuzingatiwa kwa Sheria, Kanuni na miongozo mbali mbali iliyotumika katika usimamizi na utekelezaji wa miradi hiyo kama ifuatavyo;

Mradi wa Kuendeleza Elimu Mbadala Awamu ya II - Mradi uliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 5,423,960,019 lakini fedha halisi iliyotumika ni shilingi 11,380,969,247 na kupelekea ongezeko ya matumizi ya shilingi 5,957,009,228 sawa na asilima 110 la bajeti iliyoidhinishwa.

Mradi wa Ushirikiano wa Kimataifa wa Elimu (GPE II) - jumla ya shilingi 267,372,900 zimetumika katika utekelezaji wa shughuli za mradi kinyume na muongozo wa bajeti iliyoidhinishiwa.

Mradi wa Ushirikiano wa Kimataifa kwa Elimu (GPE II) - jumla ya shilingi 437,161,495 zilitumika lakini hazikuthibitishwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka, kufanyika kwa malipo yasiyokuwa na vielelezo yenye jumla ya shilingi 141,136,290, kucheleweshwa kufanyika ununuzi wa vifaa saidizi vyenye thamani ya shilingi 747,250,000 licha ya fedha hizo kutolewa kwa wakati.

Mradi wa Huduma za Jamii Mijini Zanzibar (ZUSP), jumla ya shilingi 1,736,773,216.56 zilipangwa kutumika kwa ajili ya uondoaji maji katika bwawa la Mwantenga lakini mradi huo haujatekelezwa licha ya fedha hizo kutolewa kwa wakati, kutokufanyakazi kwa mfumo wa maji taka katika jaa la Kibele uliogharimu jumla ya shilingi 1,246,124,300, jumla ya dola za Kimarekani 420,580 zimetumika kwa ununuzi wa vifaa vya kusagia taka katika jaa la

Kibele miezi tisa iliyopita lakini vifaa hivyo havijatumika wala kuhifadhiwa sehemu nzuri. Mradi wa Kudhibiti VVU, Kifua Kikuu na Ukoma Zanzibar - jumla ya shilingi 48,020,000 zimetumika kwa ununuzi wa dawa aina ya Methadone lakini dawa hizo hazijapokelewa wala hazipata maelezo kuhusu dawa hizo, jumla ya shilingi 196,902,972 zimelipwa kwa ununuzi wa mali za Mradi kwa wauzaji ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar.

Mradi wa Uimarishaji wa Sekta ya Umeme Zanzibar - jumla ya shilingi 127,721,006.80 zilitumika kwa zabuni ya ununuzi wa vifaa vya umeme lakini utaratibu wa utowaji wa zabuni haukufuatwa.

Mradi wa kusaidia Sekta ya Uchukuzi - jumla ya USD 166,469.25 zilitolewa ili kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara husika lakini fedha hizo hazikutumika kama ilivyokusudiwa, jumla ya shilingi 288,112,125 zilizotengwa kwa ulipaji wa Fidia kwa Wananchi lakini fidia hiyo haijalipwa licha ya kuwepo kwa ripoti ya Mtathmini Mkuu.

Mradi wa Ujenzi wa Dahalia ya wanafunzi wa kiume katika Skuli ya Sekondari ya Moh'd Juma Pindua - Kukosekana kwa vielelezo vya uwasilishaji wa fedha za Kodi (VAT) Serikalini shilingi 52,838,925.

Mradi wa ujenzi wa Mahanga ya KMKM - Malipo ya ujenzi wa Hanga la Wete yasiyokuwa na vielelezo shilingi 350,000,000, jumla ya shilingi 143,915,000 ni miongoni mwa fedha zilizotumika kununua vifaa vya ujenzi wa Mahanga ya Kiuyu Mbuyuni ambavyo havikupokelewa wala kutumika, kukosekana kwa kumbu kumbu za kifedha na ujenzi wa Mahanga ya Kiuyu Mbuyuni katika hatua ya awali hadi hatua ya gebo.

Ukumbi wa Mikutano wa Umoja ni Nguvu – Malipo yaliyokosekana kwa ukaguzi shilingi 38,394,260.17, kukosekana kwa vielelezo vya uwasilishawaji wa kodi ya zuio Serikalini shilingi 21,272,771.62, kutokukamilika kwa ujenzi wa Ukumbi uliogharimu shilingi 672,742,780, kutokufanyika kwa malipo ya ujenzi kwa mujibu wa Mkataba shilingi 23,911,583.56.

Mradi wa Uhifadhi wa Eneo la Kihistoria la Mkamandume Pemba - Kukosekana kwa vielelezo vya ulipwaji wa kodi ya VAT Serikalini Shilingi 56,058,851, Kutokulingana kwa bei ya ununuzi wa vifaa na bei halisi ya sokoni kwa thamani

ya shilingi 30,260,000, Kutokupatikana kwa thamani ya fedha iliyotumika katika ukarabati wa kisima cha Wivu kilichogharimu shilingi 116,661,400, jumla shilingi 350,371,000 zilitumika kwa ujenzi wa ukuta na uchimbaji wa msingi ili kupitisha maji chumvi lakini mafanikio yaliyokusudiwa ya uingiaji na utokaji wa maji chumvi hayakupatikana, kufanyika kwa malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 80,757,324, malipo ya kodi yasiyokuwa na vielelezo shilingi 77,462,950.

Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Mama la Mtoto katika Hospitali ya Chake Chake - Kuongezeka kwa gharama za ujenzi kwa shilingi 2,288,972,200 sawa na asilimia 157.86 ya makadirio kutoka makadirio ya awali ya shilingi 1,449,968,660 hadi kufikia shilingi 3,738,940,860, kutokulipwa kwa Fedha za Mshauri Elekezi shilingi 25,705,120 na kutokukamilika kwa mradi huo kwa muda uliobainisha katika mkataba.

Ukaguzi unashauri wasimamizi na watekelezaji wa miradi ya maendeleo kuwajibika ipasavyo ili ufanisi na malengo tarajiwa yaweze kufikiwa kikamilifu, aidha Serikali pamoja na washirika wa maendeleo wanashauriwa kutowa fedha za miradi hiyo kwa wakati ili kuepusha athari zinazoweza kusababishwa na uchelewaji wa fedha hizo.

# SURA YA KWANZA

# TAARIFA YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

## 1.0 UTANGULIZI

Ripoti ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa katika Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha mwaka 2020/2021. Ukaguzi huu umefanywa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo za Kitaifa na Kimataifa.

Ukaguzi huo umelenga kutoa picha halisi ya namna ya miradi mbali mbali ya Serikali inavyotekelezwa, ili kuhakikisha kwamba taratibu na Sheria kuhusu usimamizi katika utekelezaji wa miradi hiyo unatekelezwa kwa mujibu wa sheria zilizopo. Aidha, ukaguzi huo ulikua na lengo la kuhakikisha kwamba fedha na rasilimali za umma zinatumika kama ilivyokusudiwa. Ripoti hii inajumuisha miradi inayofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na washirika wa maendeleo.

## 1.1 UANZISHWAJI WA OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibu wa kukagua hesabu zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ukaguzi huo unafanyika kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Kifungu cha 112. Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar unajumuisha hesabu zote za Serikali kuu, Serikali za Mitaa, Mamlaka na Taasisi mbali mbali pamoja na Miradi mbali mbali ya maendeleo na baadae kutoa taarifa ya ukaguzi wa hesabu hizo kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Zanzibar.

Kutokana na mamlaka ya kikatiba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibu wa kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar matumizi yake yameidhinishwa kisheria ambapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibu wa kuidhinisha matumizi kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kufanya Ukaguzi wa hesabu hizo.

## 1.2 MAJUKUMU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Kifungu nambari 112 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa zake za ukaguzi huo kila mwaka. Taarifa hizo zitaelezea hali halisi za mapato na matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na utekelezaji wa sheria mbali mbali zikiwemo Sheria za fedha, Sheria za manunuzi na sheria nyenginezo.

Kwa mujibu wa Kifungu nambari 112 (3) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu anawajibika kufanya yafuatayo:-

"a) Kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, matumizi yake yameidhinishwa kisheria na iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe.

b) Kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yanatokana na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi, na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zilizohusika na matumizi ya fedha hizo na kwamba matumzi hayo yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo; na

c) Angalau mara moja kwa kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu za Mahkama zote za Zanzibar, hesabu za Tume au vyombo vyengine vilivyoanzishwa na Katiba hii na hesabu zozote zinazohusika na Baraza la Wawakilishi. "

Ukaguzi wa hesabu umefanywa kwa kuzingatia miongozo na vigezo mbali mbali vya ukaguzi ili kukidhi matarajio ya wadau wetu na wananchi kwa ujumla. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaendelea kufanya uchambuzi wa njia bora zaidi kwa kufanya ukaguzi utakaoleta tija na kuongeza wigo na maeneo yanayokaguliwa kwa lengo la kuimarisha utendaji na uwajibikaji katika sekta za umma.

## 1.3 UPEO NA MADHUMUNI YA UKAGUZI

Upeo wa ukaguzi uliofanyika kwa kila mradi ulihusisha mfumo wa taarifa za fedha, udhibiti wa ndani wa shughuli mbalimbali za mradi zilizokaguliwa, uzingatiaji wa sheria na kanuni ikiwa ni pamoja na kanuni za manunuzi na matakwa mengine maalumu yanayoongoza shughuli za miradi. Ukaguzi huu ulifanyika kwa kuzingatia sampuli, kwa hiyo upeo wa matokeo ya ukaguzi ulitokana na uwasilishaji wa kumbukumbu, nyaraka, na taarifa zilizoombwa kwa ajili ya ukaguzi husika.

Lengo kuu la kufanya ukaguzi ni kujiridhisha kwamba taarifa za fedha kwa ujumla wake hazina taarifa zisizo sahihi kutokana na udanganyifu au dosari na kwamba zimeandaliwa kwa mujibu wa mfumo wa utoaji taarifa wa kifedha .

## 1.4 VIWANGO VYA UKAGUZI VILIVYOTUMIKA

Ukaguzi umefanyika kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi vya Ofisi za Ukaguzi wa Umma (ISSAIs) zinazotolewa na Taasisi ya Kimataifa inayojumuisha Asasi kuu za Ukaguzi wa Hesabu (INTOSAI) , Jumuiya ya Asasi Kuu za Ukaguzi kwa Nchi za Afrika zinazozungumza Kiingereza (AFROSAI-E) pamoja na taratibu nyingine nilizoona zinafaa kutokana na mazingira husika. Viwango ambavyo vinatutaka katika ukaguzi wetu kuzingatia maadili katika kuandaa na kutekeleza ukaguzi kwa nia ya kupata uhakika kwamba taarifa za hesabu zipo sahihi na hazina makosa makubwa

## 1.5 MBINU ZA UKAGUZI ZILIZOTUMIKA

Mbinu zilizotumika katika ukaguzi ni pamoja na kutathmini kumbukumbu za uhasibu na taratibu zingine ili kukidhi malengo ya ukaguzi. Taratibu za ukaguzi zilijumuisha hatua zifuatazo:-

- Kupanga ukaguzi ili kutambua na kutathmini hatari za kuwa na taarifa zisizo sahihi, ama kutokana na udanganyifu au dosari; na kwa kuzingatia uelewa wa taasisi na mazingira yake, ikiwa ni pamoja na mifumo ya udhibiti wa ndani ya kila taasisi.
- Kupata uthibitisho sahihi iwapo kuna taarifa zisizo sahihi na kutekeleza hatua stahiki dhidi ya viashiria vyote vya hatari vilivyoainishwa.

- Kutembelea shughuli za miradi na kutathmini utendaji na utekelezaji wake.
- Kutathmini ili kuona iwapo sheria, kanuni na mahitaji maalumu ya miradi yamezingatiwa kikamilifu.
- Kutoa maoni juu ya taarifa za kifedha zilizokaguliwa.
- Kufuatilia utekelezaji wa matokeo ya ukaguzi wa mwaka uliopita na kuhakikisha kwamba hatua sahihi zimechukuliwa kuhusiana na masuala yote yaliyoainishwa.

# SURA YA PILI

## 2.0 UWASILISHAJI WA HESABU ZA MIRADI YA MAENDELEO

Kwa mujibu wa kifungu namba 119(1) cha sheria ya usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016 inazitaka Taasisi zote za Serikali zitayarishe na kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwaka, zinazojumuisha Mapato na matumizi ya Taasisi husika.

Tunatoa pongezi kwa Taasisi zenye kusimamia Miradi ya Maendeleo kwa jitihada walizochukuwa za kuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka kwa mujibu wa sheria.

Uwasilishwaji wa hesabu za Miradi ya Maendeleo kwa ajili ya ukaguzi wa mwaka 2020/2021 ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 1 : Uwasilishaji wa hesabu za Miradi ya Maendeleo**

| Na | Jina la Mradi | Tarehe iliyowasilishwa kwa ukaguzi |
|---|---|---|
| | **Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali** | |
| 1. | Mradi wa Kuendeleza Elimu Mbadala Awamu Ya II (ALSD II) | 30/9/2021 |
| 2. | Mradi wa Ujenzi na Ununuaji wa Vifaa kwa ajili ya Skuli za Sekondari Zanzibar – BADEA II | 30/9/2021 |
| 3. | Mradi wa Ushirikiano wa Kimataifa kwa Elimu GPE II | 30/9/2021 |
| 4. | Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Sekondari Zanzibar (ZISP) | 28/9/2021 |
| 5. | Mpango wa Lishe Mashuleni – (HGSFP) | 30/9/2021 |
| | **Wizara ya Fedha na Mipango** | |
| 6. | Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma- (PFMRP) | 30/9/2021 |
| 7. | Mradi ya Huduma za Jamii Mijini Zanzibar- (ZUSP) | |
| | **Wizara ya Kilimo na Mali Asili** | |
| 8. | Mradi wa Uzalishaji wa Mpunga- (ERPP) | 28/9/2021 |
| | **Wizara ya Afya** | |
| 9. | Mradi wa Kudhibiti VVU, Kifua Kikuu na Ukoma Zanzibar (ZIHTLP) | 29/9/2021 |
| 10. | Mradi wa kutokomeza Malaria Zanzibar- Zanzibar (ZAMEP) | - |
| | **Wizara ya Ardhi, Maji, Mazingira na Nishati** | |

| Na | Jina la Mradi | Tarehe iliyowasilishwa kwa ukaguzi |
|---|---|---|
| 11. | Mradi wa Uimarishaji wa Sekta ya Umeme Zanzibar | 29/9/2021 |
| **Wizara ya Uchumi wa Buluu** | | |
| 12. | Mradi wa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Zanzibar (SWIOFish1 - GEF GRANT) | 29/9/2021 |
| 13. | Mradi wa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Zanzibar (SWIOFish1 - IDA Loan | 29/9/2021 |
| **Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi** | | |
| 14. | Mradi wa kusaidia Sekta ya Uchukuzi (TSSP) | 30/9/2021 |

## 2.1 TATHMINI YA UFANISI WA MIRADI YA MAENDELEO

Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ilikagua utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo inayofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, pamoja na Washirika wa Maendeleo.

Ukaguzi umebaini baadhi ya miradi haikuweza kukamilika kwa wakati kutokana na sababu mbali mbali ikiwemo upatikanaji wa fedha kwa wakati ' Inashauriwa kuwa miradi yote iliyoidhinishwa inaingiziwa fedha kwa wakati na kuhakikisha kwamba fedha zinazotolewa kama zilivyopangwa ili kutoathiri utekelezaji wa miradi hiyo kwa kuwa ucheleweshaji wa upatikanaji wa fedha kunapelekea kutotekelezeka kwa miradi kama iliyokusudiwa.

## 2.2 DOSARI ZA UJUMLA ZILIZOBAINIKA KATIKA USIMAMIZI WA FEDHA

Katika utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ukaguzi umebaini uwepo mapungufu ambayo yamejitokeza katika usimamizi wa fedha kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kama ifuatavyo:-

- Ukaguzi umebaini mradi wa ALSD II ulianishwa bajeti ya fedha za maendeleo ya shilingi 5,423,960,019 ambapo kiasi cha shilingi 11,380,969,247 zilipokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Hivyo kupelekea kiasi cha shilingi 5,957,009,228 kutolewa zaidi ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa.
- Ukaguzi umebaini mradi wa Ushirikiano wa Kimataifa wa Elimu (GPE II) imeshindwa kutekelezwa licha ya Shilingi 267,372,900 kutumika.
- Ukaguzi umebaini uwepo wa matumizi ya mradi ya jumla ya shilingi 437,161,495 yaliyofanywa moja kwa moja na Wakala wa Ruzuku ambapo ukaguzi haukuweza kuthibitisha matumizi hayo.
- Ukaguzi umebaini uwepo wa ucheleweshaji wa mchakato wa ununuzi wa vifaa vya usaidizi vya Elimu Mjumuisho pamoja na vipuri vyake jumla ya shilingi 747,250,000 zilitengwa kwa ajili ya vifaa saidizi kwa wenye mahitaji maalum.
- Ukaguzi umebaini taarifa ya fedha ya mwaka 2020/2021 zimeripoti uwepo wa matumizi ya shilingi 141,136,290 ikiwa ni gharama ya usimamizi wa wakala wa ruzuku ambapo ukaguzi haukuweza kuthibitisha matumizi hayo.
- Ukaguzi umebaini hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 mradi ulikuwa na salio la jumla ya dola za kimarekani USD 3,734.74 ambazo hazikutumika kwa shughuli za mradi zilizopangwa kwa kipindi hicho.
- Ukaguzi umebaini uwepo wa Miradi ambayo haikutekelezwa (kazi ya kuondoa maji katika bwawa la Mwantenga) ambao uligharimu jumla ya shilingi 1,736,773,216.56 hadi mradi unamalizika .
- Ukaguzi ulitembelea jaa la Kibele na kubaini kuwa Mfumo wa maji taka (PCW) uliwekwa ambao uligharimu jumla ya shilingi 1,246,124,300 hadi kumalizika kwake haufanyi kazi ipasavyo kutokana na kuziba kwa mabomba.

- Ukaguzi ulitembelea eneo la jaa la Kibele na kubaini kwamba Wizara ya Fedha na Mipango ilinunua vifaa vya kusagia taka kwa ajili ya jaa Kibele ikiwemo Trekta la kilimo, mashine ya kugeuza, trela ya tanki la maji kwa gharama ya dola za Kimarekani 420,580 ambapo Msambazaji tayari ameshalipwa fedha ya vifaa hivyo zikiwemo gharama za ufungaji na mafunzo,lakini hadi ukaguzi unamalizika vifaa hivyo havikuweza kufanyakazi wala kuwekwa sehemu nzuri licha ya miezi tisa kupita tokea vilipopokelewa
- Ukaguzi umebaini mradi ZIHTLP umenunua dawa aina ya Methadone jumla ya shilingi 48,020,000 kutoka kwa Msambazaji K Brain Scientific kwa mujibu wa hati Namba 5774 ya tarehe 20 Novemba,2020 . Hadi ukaguzi unamalizika tarehe 5 Oktoba 2021, dawa hizo hazijapokelewa wala hakuna maelezo yoyote yaliotolewa kwa ukaguzi kuhusu dawa hizo.
- Ukaguzi umebaini mradi wa ZIHTLP ulifanya ununuzi wa mali za shilingi 196,902,972 kutoka kwa wauzaji ambao hawakuthibitishwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA)
- Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 127,721,006.80 zimetumiwa na mradi kwa ajili wa ununuzi wa Sergeflex 32 cable fault distance location bila ya kufuata mchakato wa kushindanisha zabuni kinyume na Kifungu cha 72(2) cha Sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2016.
- Ukaguzi umebaini Wizara ya Miundombinu, Mawasiliano na Uchukuzi imepokea jumla ya dola za kimarekani USD 166,469.25 kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumishi na Wizara.Kiasi hicho hakikutumika kama ilivyokusudiwa.
- Ukaguzi umebaini uwepo wa shilingi 288,112,125 kwa ajili ya kuwalipa Fidia Wananchi walioathirika na mradi (PAP) ,fedha hiyo haijalipwa licha ya uwepo wa ripoti ya Mtathmini Mkuu.

## 2.3 MAPENDEKEZO YA JUMLA

Ukaguzi unashauri uongozi unaosimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kuhakikisha unaweka misingi imara itakayowezesha kuongezeka kwa uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma.

- Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wanatakiwa kuhakikisha kwamba fedha zilizoidhinishwa zinatolewa kwa wakati ili kutekeleza miradi iliyokusudiwa hatimaye kuleta tija kwa jamii.
- Wasimamizi wa Mradi wanapaswa kuhakikisha kwamba manunuzi, kazi za ujenzi, bidhaa na huduma yanazingatia matakwa ya Sheria na Kanuni za Manunuzi na Uondoshaji wa mali za Umma Nambari 11 ya mwaka 2016 ili kuhakikisha thamani ya fedha, uwazi na mafanikio unakuwepo kwenye manunuzi yanayofanywa katika miradi.
- Wasimamizi wa miradi ya maendeleo wanashauriwa kuweka juhudi zaidi katika kuhakikisha kwamba mapendekezo ya ukaguzi yaliowasilishwa katika ripoti 2020/2021 yanashughulikiwa ipasavyo ili kuondoa uwezekano wa kujirudia kwa dosari hizo katika ukaguzi ujao.
- Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani vinapewa rasilimali za kutosha ili kuviongezea ufanisi katika utendaji,ili kuboresha utawala bora, uthibiti wa ndani pamoja na uongozi wa miradi ya maendeleo.

# SURA YA TATU

## 3.0 MIRADI ILIYOTEKELEZWA KATIKA SEKTA YA ELIMU

## 3.1 MRADI WA KUENDELEZA ELIMU MBADALA AWAMU YA II (ALSD II)

Mradi wa kuendeleza elimu mbadala awamu ya pili (Alternative Learning and Skills Development II - ALSD II) ni mradi uliofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ambao umesainiwa tarehe 12 Septemba, 2011 na kuanza utekelezaji wake rasmi tarehe 23 Machi, 2012 kwa Unguja na Pemba na ulitarajiwa kumalizaka tarehe 31 Disemba, 2020. Lengo kuu la mradi huu ni kuongeza ajira kwa vijana na kuboresha upatikanaji wa elimu za amali ikiwemo ufundi na biashara unaohitajika katika soko la ajira. Mradi huu unatekelezwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (MoEVT) Zanzibar kupitia kitengo cha uratibu wa Mradi (PCU) kwa ajili ya usimamizi na kuratibu shughuli za kila siku za mradi.

### 3.1.1 MALENGO YA MRADI

Malengo makuu ya mradi yamehusisha vipengele vikuu vitatu (3) kama vifuatavyo:-

- **Kipengele I: Vituo vya elimu mbadala na ukuzaji wa mafunzo ya amali .**

Kipengele hiki kitatoa msaada zaidi kupitia juhudi za serikali ili kutoa mafunzo mbadala kwa vijana waliowacha shule pamoja na wale wenye mahitaji maalum ambao hawajawahi kujiandikisha au kuacha shule kabla ya kumaliza elimu ya msingi.

- **Kipengele II: Kuimarisha uwezo wa Taasisi katika kutoa huduma**

Kipengele hiki kinalenga katika kuimarisha uwezo wa Taasisi zinazohusika moja kwa moja na ukuzaji wa elimu kwa vijana kupitia Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Kurume, Taasisi ya Maendeleo ya Utalii Zanzibar, Tume ya Kazi Zanzibar pamoja Uhamasishaji wa jamii, uvumbuzi na Ufuatiliaji huru (Community sensitization, innovation and independent monitaring).

- **Kipengele cha III: Usimamizi wa Mradi**

Kipengele hiki kinalenga kutoa elimu, pamoja na mafunzo ya kuimarisha usimamizi wa mradi, uendeshaji wa gharama na usimamizi wa mradi pamoja na ukaguzi wa mradi.

### 3.1.2 TAARIFA YA FEDHA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MRADI WA ALSD II

**Taarifa ya Mapato na Matumzi**

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Mradi wa kuendeleza elimu mbadala awamu ya II (ALSD II) ulikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 10,947,944,974 kutoka AfDB. Hadi kufikia 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 10,746,059,180.82 zimeingizwa na kutumika ambazo sawa na asilimia 98 ya makadirio.

**Mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar**

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Mradi wa kuendeleza elimu mbadala awamu ya II (ALSD II) ulikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,367,413,560 ikiwa ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hadi kufikia 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 2,111,159,000 zimeingizwa na kutumika ambazo ni sawa na asilimia 89 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 3.1.1.2 Kuwepo kwa ongezeko la fedha za mradi shilingi 5,957,009,228

Mradi wa ALSD II kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 uliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 5,423,960,019 ambapo imebainika kuwa kiasi cha shilingi 11,380,969,247 ziliingizwa na kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo na kupelekea kuwepo kwa ongezeko la shilingi 5,957,009,228 sawa na asilimia 110 ya fedha zilizoidhinishwa.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa matumizi yasiyoridhisha ya fedha pamoja na rasilimali za Umma ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mradi kuongeza umakini katika kufanya makisio

ya matumizi ya fedha ili iendane na hali halisi ya gharama za Utekelezaji wa mradi. Mchanganuo wa ongezeko la fedha za mradi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 2 : Kuwepo kwa ongezeko la fedha za mradi**

| Maelezo | Kiasi cha fedha kilicho kadiriwa (Tshs.) | Kiasi cha fedha kilichotumika (Tshs.) | Tofauti (Tshs.) |
|---|---|---|---|
| Huduma ya mshauri elekezi kwa KIST,ZITOD na VTA | 38,705,920 | 151,194,500 | (112,488,580) |
| Ujenzi wa Skuli, Makunduchi Unguja | 1,866,414,670 | 3,345,835,079.9 | (1,479,420,409.91) |
| Ujenzi wa Daya Pemba | 1,798,895,074 | 4,737,701,507 | (2,938,806,433) |
| Ujenzi wa jengo la KIST | 204,556,558 | 212,471,344.92 | (7,914,786.92) |
| Ugavi wa vifaa kwa ajili ya Daya na Makunduchi | - | 89,448,848 | (89,448,848) |
| Vifaa vya ZITOD | 166,174,217 | 269,862,410.52 | (103,688,193.52) |
| Replenishment | - | 488,842,023 | (488,842,023) |
| Mchango wa Serikali | 1,349,213,580 | 2,085,613,533.43 | (736,399,953.43) |
| **Jumla** | **5,423,960,019** | **11,380,969,247** | **(5,957,009,228)** |

## 3.2 MRADI WA UJENZI NA UNUNUZI WA VIFAA KWA AJILI YA SKULI ZA SEKONDARI ZANZIBAR

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA) Zanzibar imeingia mkataba na Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi Barani Afrika (BADEA) kwa ajili ya kufanyia marekebisho mfumo wake wa elimu tarehe 1 Aprili, 2020 na unatarajiwa kumalizika tarehe 31 Machi, 2023. Mradi wa Ujenzi na Ununuzi wa Vifaa kwa Ajili ya Skuli za Sekondari Zanzibar (The Contruction And Equiping Of Secondary Schools Projects) umetekelezwa kwa ajili ya ujenzi wa skuli za sekondari na usambazaji wa samani za Skuli na Mabasi ili kukidhi mahitaji ya elimu kwa umma. Mradi huo unajumuisha kazi za ujenzi wa skuli tatu katika maeneo ya Mfenesini Mjini Magharibi, Gamba kaskazini Unguja na kijiji cha Kifundi kisiwani Pemba, pamoja na ununuzi wa vifaa.

Lengo kuu la mradi huo ni kuifanya Zanzibar iweze kufikia mipango ya maendeleo endelevu kupitia katika nyanja ya elimu, ikiwa ni pamoja na utoaji wa fursa za elimu kwa wanafunzi wa maeneo yanayokabiliwa na upungufu wa Skuli za Sekondari.

### 3.2.1 TAARIFA YA FEDHA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MRADI WA BADEA II

**Taarifa ya Mapato na Matumzi**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Mradi wa BADEA II ulikadiriwa kupata mkopo wa jumla ya dola za Kimarekani USD 13,500,000 ambapo kati ya fedha hizo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipanga kuchangia jumla ya dola za Kimarekani USD 1,500,000. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi Barani Afrika ilitoa jumla ya dola za Kimarekani USD 26,880 sawa na shilingi 61,447,680.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 3.2.1.1 Ucheleweshaji wa kuidhinishwa kwa kibali cha Mshauri wa Michoro na Usanifu wa majengo

Katika ukaguzi uliyofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika uwepo wa ucheleweshaji wa ujenzi wa skuli tatu zilizotarajiwa kujengwa Mfenesini na Gamba kwa Unguja na Kifundi kisiwani Pemba chini ya usimamizi wa mradi wa BADEA II ambapo ujenzi huo ulitarajiwa kuanza mwezi wa Oktoba, 2021. Hali hiyo ilitokana na kucheweshwa kwa uhakiki wa kibali cha mshauri wa Michoro na Usanifu wa majengo jambo ambalo limepelekea kutotekelezeka kwa ujenzi wa skuli hizo kwa wakati.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Elimu kuwa makini katika kusimamia vyema utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa wakati na kuelewa kwamba ujenzi ndio kiini cha mkopo.

## 3.3 MRADI WA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA KWA ELIMU (GPE II)

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imekuwa ikitekeleza Mpango wa Ushirikiano wa Kimataifa wa Elimu (Global Partnership for Education – GPE II) unaofadhiliwa na Ushirikiano wa Kimataifa wa Elimu na unasimamiwa na Ubalozi wa Sweden kama Wakala wa Ruzuku kuanzia mwaka 2014 hadi mwaka 2016, kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa elimu kwa usawa na kuboresha umuhimu na ubora wa elimu katika sekta nzima ya elimu.

Utekelezaji wa Mradi wa awamu ya pili (GPE II) ulianza Julai, 2018 kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa elimu katika mfumo mzima kwa kuendeleza programu ya elimu-jumuishi na kutoa elimu bora kwa wanafunzi wote wa Zanzibar, Mradi huu unatarajiwa kufanya kazi kwa muda wa miaka minne kuanzia Aprili, 2018 hadi tarehe 30 Juni, 2022.

### 3.3.1 MALENGO YA MRADI

Lengo kuu la mradi ni kuwawezesha watoto wenye umri wa miaka 2 kupata elimu ya awali pamoja na watoto wasiojiweza hasa maskini wa vijijini na watoto walio na matatizo ya kimaumbile wanajifunza na kuweza kufikia ngazi zote za elimu ya awali, msingi na sekondari.

### 3.3.2 VIPENGELE VYA MRADI

Mradi uliratibu shughuli kupitia vipengele vitatu vifuatavyo:-

**Elimu ya Awali**

Kipengele hiki cha mradi wa GPE II ina iwezesha Idara kufanya kazi kwa kushirikiana na Idara nyengine za Wizara ambazo ni Idara ya TEHAMA katika Elimu, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Taasisi ya Elimu Zanzibar, Mkaguzi Mkuu wa Elimu, Baraza la Mitihani Zanzibar na Idara ya Elimu ya Ualimu.

**Elimu jumuishi**

Kipengele hiki kinaelekea kuongeza idadi ya skuli na walimu wanaokidhi viwango vya elimu jumuishi.

**Usimamizi na uratibu wa mradi**

Usimamizi wa miradi unaendelea na uratibu wa kila siku na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mradi. Yafuatayo yalipewa kipaumbele chini ya usimamizi:-

- Uongozi uliandaa na kufanyika warsha ya siku moja ya uhamasishaji wa mradi kwa wilaya nne; Magharibi B, Kaskazini B, Wete na Chake-Chake. Hii ilifuatia usambazaji wa vipeperushi vya mradi ambapo vipeperushi 1,000 vilichapishwa na kusambazwa kwa PO-RALGSD na Ofisi ya WEMA Pemba.
- Vikao vinne vya Kamati ya Uongozi wa Mradi kujadili maendeleo ya utekelezaji wa mradi vilifanyika. Mikutano hiyo iliidhinisha ripoti ya maendeleo ya robo mwaka na mipango ya robo mwaka ya miradi. Menejimenti pia ilifanya vikao sita na watekelezaji wakuu ili kujadili changamoto za utekelezaji wa mradi na kubadilishana mawazo juu ya njia ya kusonga mbele. Pamoja na Mkutano pia kuweka pamoja watekelezaji wote katika kuandaa kazi ya kila mwaka kwa mwaka ujao wa 2020/2021.
- Uongozi uliandaa mkutano wa mwaka wa mapitio ya pamoja ya sekta ya elimu mwezi Februari 2019. Mkutano huo ulihusisha wadau kutoka ndani na nje ya Zanzibar wakiwemo washirika wa maendeleo wanaosaidia elimu. Madhumuni ya mkutano wa AJESR ni kutathmini utendaji kazi wa sekta za elimu kwa kuzingatia Mpango wa Sekta ya Elimu. Washiriki walijadili na kukubaliana juu ya maazimio kumi na njia ya kusonga mbele kwa kuzingatia changamoto zilizojadiliwa. Ripoti ya kina ya mkutano wa AJESR ilitayarishwa na kuchangiwa na wadau.

### 3.3.3 TAARIFA YA FEDHA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MRADI

**Taarifa ya Mapato na Matumzi**

Mradi huu unafadhiliwa na "Global Partnership for Education" ambapo Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden (SIDA) lilitoa jumla ya dola za kimarekani 2,249,990 kwa Mradi wa GPE, kukiwa na salio la anzia la jumla ya Dola za kimarekani 211 na kufanya jumla ya dola za kimarekani 2,250,201.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 mradi ulitoa jumla ya dola za kimarekani 2,000,000 na kufikia jumla ya dola za kimarekani 4,550,000 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 3.3.3.1 Kukosekana kwa Ufanisi katika matumizi ya fedha

Katika kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2021 ukaguzi umebaini mradi ulikuwa na bakaa ya jumla ya USD 4,536.70 sawa na jumla ya shilingi 10,411,727 ambapo mradi huo ulibainika katika kipindi cha mwezi Agosti, 2020 ulipokea jumla ya USD 2,000,000 sawa na shilingi 4,629,965,298 kutoka Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Sweden (SIDA).

Ukaguzi umebaini kuwa mradi haukuwa na ufanisi mzuri wa matumizi ya asilimia 100 ukilinganisha na shughuli zilizopangwa. Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Elimu kufanya matumizi katika shughuli za mradi zilizopangwa kulingana na bajeti iliyoidhinishwa.

### 3.3.3.2 Utekelezaji wa Mradi kinyume na bajeti iliyopangwa

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi umebaini utekelezaji wa shughuli za mradi haukuwa wenye kuridhisha ambapo jumla ya shilingi 5,200,680,444.97 zilitumika sawa na asilimia 56 ya matumizi ukilinganishwa na fedha iliyotengwa ya shilingi 9,231,818,700 kwa utekelezaji wa shughuli za mradi katika kipindi cha mwaka husika ambapo kunaweza kusababisha kutokufikiwa kwa malengo ya utekelezaji wa mradi kwa kulingana na wakati uliopangwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kufanya usimamaizi wakina ili shughuli zote za mradi zilizokusudiwa zinatekelezwa kulingana na mpango wa bajeti ya mradi na kwamba fedha zote za mradi zilizopangwa zinatumika kama ilivyokususdiwa. Hali halisi ya utekelezaji wa mradi ni kama inavyoonekana hapo chini:-

**Jadweli Nambari 3 : Utekelezaji wa Mradi kinyume na bajeti iliyopangwa**

| Na | Vipengele | Kiasi cha fedhakilicho kadiriwa (Tshs) | Kiasi cha fedha kilichotumika (Tshs) | Tofauti ya fedha (Tshs) | Tofauti ya asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Elimu ya awali na Msingi | 6,696,983,000 | 4,122,160,027 | 2,574,822,973 | 61.5 |
| 2. | Elimu Jumuishi | 1,900,291,700 | 782,495,212 | 1,117,796,488 | 41 |
| 3. | Usimamizi na Utawala | 634,544,000 | 296,025,206 | 388,518,794 | 46.6 |
| | **Jumla** | **9,231,818,700** | **5,200,680,445** | **4,081,138,255** | 56 |

### 3.3.3.5 Kutokuthibitika kwa matumizi yaliyobainishwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka ya shilingi 437,161,495

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 437,161,495 zilitumika kwa ajili ya shughuli mbali mbali za mradi lakini ukaguzi haukuweza kuthibitisha matumizi yaliyoripotiwa katika taarifa ya fedha ya mwaka. Kufanya hivyo kunapelekea uwepo wa viashiria vya upotevu wa fedha na matumizi mabaya ya rasilimali za Umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuzingatia sheria, miongozo na kanuni zinazoongoza taratibu katika kufanya miamala ya fedha ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Fedha na Usimamizi na Rasilimali za Umma ya mwaka 2016.

### 3.3.3.6 Kutotekelezwa kwa shughuli za Mradi zilizopangwa shilingi 267,372,900

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi ulipitia taarifa ya mpango mwaka wa 2020/2021 ya mradi wa Ushirikiano wa Kimataifa wa Elimu (GPE II) na kubaini baadhi ya shughuli za mradi zilizopangwa kwa mwaka husika hazikutekelezwa kwa mujibu wa bajeti ambapo kunaweza kuathiri mabadiliko ya bajeti katika bidhaa na bei za huduma pamoja na shughuli za mradi zilizopangwa kutokufanyika kwa wakati

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha kwamba shughuli zote za mradi zinatekelezwa kwa wakati kwa mujibu wa kiasi cha fedha kilichokadiriwa. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 4 : Kutotekelezwa kwa Shughuli za Mradi zilizopangwa**

| Na | Shughuli iliyopangwa kufanywa kwa mujibu wa Mpango kazi wa Mradi | Kiasi cha fedha kilichokadiriwa (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Warsha katika kila wilaya ili kushauriana na wadau kuhusu mfumo na mwongozo wa ECE | 29,346,000 |
| 2. | Siku 3 za mafunzo ya kazini kwa ADES, ARASS ikijumuisha mtaalamu wa PPE, washauri wa masomo, walimu wakuu na mkaguzi wa Mpango wa Maendeleo ya Kitaaluma. | 106,570,000 |
| 3. | Majaribio ya program ya Uongozi katika skuli kumi 10 | 750,000 |
| 4. | Kuchapisha Nakala 1600 za Mafunzo ya Usimamizi yaliyoratibiwa | 8,000,000 |
| 5. | Machapisho ya watu wenye mahitaji maalum (Printing the inclusive) | 27,091,000 |
| 6. | Mshauri kukagua na kufuata ufanisi wa mafunzo | 95,615,900 |
| **Jumla** | | **267,372,900** |

### 3.3.3.5 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 141,136,290

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 141,136,290 zimetumika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ushirikiano wa kimataifa lakini vielelezo vya matumuzi hayo havikupatikana kwa ukaguzi ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo husika.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo matumizi yasiyoridhisha ya fedha za Umma ambapo ni kwenda kinyume na Kifungu Nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha kwamba malipo yote yanayofanyika yanawekewa vielelezo na kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi

#### 3.3.3.6 Kutotumika kwa fedha za mradi kwa wakati uliopangwa shilingi 362,246,648.52

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa bakaa ya dola za kimarekani 156,410 mwishoni mwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambazo ni sawa na shilingi 362,246,648.52 zilizopaswa kutumika kwa ajili ya shughuli za utekelezaji wa mradi. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuchelewa kumalizika kwa mradi kwa wakati ambapo kunaweza kuathiri maendeleo ya mradi huo kutokana na uwezekano wa kupanda kwa bei za bidhaa

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha kwamba mpango kazi wa  mradi unatekelezwa kulingana na bajeti ili kufikia lengo lililo kusudiwa.

## 3.4 MRADI WA UIMARISHAJI WA ELIMU YA SEKONDARI ZANZIBAR (ZISP)

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Sekondari Zanzibar (ZISP) umefadhiliwa na  Shirika la  Maendeleo ya Kimataifa (IDA) ambao unaboresha elimu ya Sekondari katika visiwa vya Zanzibar na kuweka mazingira mazuri ya kujifunzia na masomo yaliyokusudiwa.

Mradi huu unatarajiwa kuwanufaisha jumla ya watu 170,000 katika kipindi cha miaka mitano(5)  ambapo walengwa Wakuu ni wanafunzi wa darasa la juu la msingi na sekondari ya chini pamoja na kuwanufaisha Walimu, Walimu Wakuu na wafanyakazi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali .

### 3.4.1 VIPENGELE VYA MIRADI

Mradi una vipengele vinne kama ifuatavyo:-

**Kipengele cha 1:** Itahusu ufundishaji bora wa Hisabati, Sayansi na Kiingereza (Dola za Marekani milioni 7).

Kipengele hiki kitazingatia aina tatu za shughuli:-

- Kutoa mafunzo upya kwa walimu waliokazini waliochaguliwa ili kuongeza upatikanaji wa walimu wa Hisabati na Sayansi katika madarasa ya chini ya sekondari;

- Marekebisho ya usimamizi wa walimu ili kuimarisha uwajibikaji wa walimu na miundo ya motisha.

**Kipengele cha 2:** Uboreshaji wa uhuru wa Skuli na Mazingira ya Kujifunzia (Dola za Marekani milioni 9).

Kipengele hiki kitazingatia aina mbili za shughuli:-

- Uboreshaji wa Ruzuku ya Skuli ambao utazingatia namba ya wanafunzi walioandikishwa katika kiwango cha Sekondari.
- Utendaji - Ruzuku ya Ufaulu ambayo itazawadiwa kwa skuli zitakazoonesha kufanya vizuri katika mitihani yao ya darasa la 6 na kidato cha pili katika Hesabu ,Sayansi na Kingereza.

**Kipengele cha 3:** Vitovu vya Kuimarisha mafunzo ya Hisabati, Sayansi na Mafunzo ya Kiingereza (Dola za Marekani milioni 17).

Kipengele hiki kitalenga kusaidia utoaji wa nyenzo/rasilimali za kujifunzia kwa ajili ya mafanikio yaliyoboreshwa ya Hesabu ,Sayani na Kingereza ..

**Kipengele cha 4:** Mabadiliko ya Mifumo na Usimamizi wa Mradi (Dola za Marekani milioni 2).

Kipengele hiki kitalenga maeneo manne:

- Mageuzi ya mitihani;
- Mipango ya mifumo ya elimu;
- Kuimarisha mifumo ya data na kusaidia Mradi katika ufuatiliaji na tathmini (Hesabu na Kingereza).
- Msaada wa utekelezaji wa mradi.

### 3.4.2 TAARIFA YA FEDHA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MRADI

#### Taarifa ya Mapato na Matumizi

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Sekondari Zanzibar (ZISP) ulikadiriwa kupokea jumla ya USD 35,000,000 kutoka Shirika la Maendeleo ya Kimataifa (IDA) kwa ajili ya utekelezaji wa mradi kwa kipindi cha miaka mitano katika vipengele vitano kama vilivyoaninshwa katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 5 : Taarifa ya fedha za mradi**

| Na | Vipengele vya Mradi | Makadirio ya mradi yaliyopangwa (USD) | Kiasi cha fedha kilichokubaliwa na Mfadhili kutumika (USD) |
|---|---|---|---|
| 1. | Ufundishaji bora wa Hisabati, Sayansi na Kiingereza | 7,000,000 | 7,000,000 |
| 2. | Kuboresha uhuru wa skuli na mazingira ya kujifunzia | 8,000,000 | 8,000,000 |
| 3. | Kuimarisha Vitovu vya Masomo ya Hisabati, Sayansi na Kiingereza | 17,000,000 | 17,000,000 |
| 4. | Mabadiliko ya Mifumo na Usimamizi wa Miradi | 2,500,000 | 2,500,000 |
| 5. | Jukwaa la kujifunza la kielektroniki lilitengenezwa na kuendeshwa | 500,000 | 500,000 |
| **Jumla** | | **35,000,000** | **35,000,000** |

### 3.4.2.1 Ucheleweshwaji wa fedha kutoka kwa wafadhili dola za Marekani 5,009,650

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa usheleweshaji wa fedha za utekelezaji wa Mradi kutoka kwa wafadhili wa Mradi huo ambao ni Shirika la Maendeleo la Kimataifa-IDA ambapo jumla ya dola za Marekani 5,009,650 zilipokelewa tarehe 16 Disemba, 2020 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi wa ZISP jambo ambalo limepelekea baadhi ya shughuli za mradi kusita kwa muda wa miezi 6 kutokana na kutopatikana kwa fedha za utekelezaji wa mradi huo kwa wakati hali inayopelekea kuzorota kwa utekelezaji wa mradi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Elimu kuwashauri wafadhili wa mradi wachukuwe juhudi ya kuhakikisha kwamba fedha zote zilizokusudiwa kwa ajili ya utekelzaji wa mradi na kwa kuzingatia muda halisi uliopangwa zinapatikana kwa wakati ili kuepusha athari zinazoweza kujitikeza.

#### 3.4.2.2 Kukosekana kwa taarifa za matumizi ya fedha za mradi shilingi 697,564,125

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 697,564,125 zimelipwa kwa kutumia hati ya malipo yenye nambari 2/12 ya tarehe 21 Disemba, 2020 kwa ajili ya ruzuku katika madarasa ya Kidato cha kwanza, Kidato cha tatu na Kidato cha nne kwa skuli mbalimbali za Zanzibar lakini hadi ukaguzi unakamilika ripoti za matumizi ya fedha hizo hazikuweza kupatikana. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa upotevu wa fedha za Umma ambapo ni Kifungu Nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Elimu kupitia wasimamizi wa mradi kuhakikisha kwamba katika kipindi chote cha utekelezaji wa mradi panakuwepo na matumizi sahihi ya fedha na rasilimali za Umma kwa kuzingatia Sheria, Kanuni pamoja na miongozo mbali mbali ya fedha inayotolewa Kitaifa na Kimataifa ikiwa ni pamoja na kuongeza umakini katika uaandaaji wa ripoti mbali mbali za mradi.

#### 3.4.2.3 Kutotumika kwa fedha za mradi kwa wakati uliopangwa USD 3,734.74

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa bakaa ya dola za Kimarekani 3,734.74 mwishoni mwa mwaka wa fedha 2020/2021 zilizopaswa kutumika kwa ajili ya shughuli za utekelezaji wa mradi. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuchelewa kumalizika kwa mradi kwa wakati ambapo kunaweza kuathiri maendeleo ya mradi huo kutokana na uwezekano wa kupanda kwa bei za bidhaa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha kwamba mpango kazi wa mradi unatekelezwa kulingana na bajeti ili kufikia lengo lililo kusudiwa.

### 3.4.2.4 Dosari zilizobainika katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi Kituo Maalum cha Sayansi

Katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa mradi wa kituo maalum cha sayansi kilichopo Mkwajuni Kaskazini Unguja kupitia mradi wa ZISP ukaguzi umebaini dosari mbalimbali kama ifuatavyo:-

- Kitokuzungushiwa uzio ili kuzuwia uvamizi wa maeneo pamoja na kuepusha uharibifu unaoweza kujitokeza kwa kutokuwepo kizuizi katika uingiaji wa maeneo hayo.
- Maeneo ya koridoo ya kituo hicho yanaonekana kutuwama maji wakati wa mvua hali ambayo imesababishwa na hali halisi ya ujenzi wa jengo.

Hali halisi ya ujenzi wa kituo ni kama inavyoonekana katika picha hapo chini:-



*Kituo maalum cha sayansi Mkwajuni-hakikuwekewa uzio*



*Kituo maalum cha sayansi Mkwajuni-Matuwamo ya maji na miundo mbinu ya umeme*

## 3.5 MPANGO WA LISHE MASHULENI (HGSFP)

Katika mwaka 2020/2021, kutokana na ugatuzi wa madaraka kwa elimu ya Awali na Msingi, Mpango wa utekelezaji wa programu ya kusambaza chakula mashuleni (Home Grown School Feeding Program - HGSFP) ulikuwa chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ambapo ilitoa tenda kwa vikundi vya wakulima kwa ajili ya kusambaza chakula katika shule zilizopo chini ya mradi na kufanya malipo kwa wakulima hao kuanzia Agosti, 2020 hadi Disemba, 2020. Mradi huu unamuda wa miaka mitatu (3) kuanzia mwaka wa fedha 2019/2020 mpaka 2022/2023.

### 3.5.1 VIPAUMBELE VYA MRADI

Wizara imeanzisha mradi wa HGSFP ili kukidhi mahitaji ya elimu ya umma kwa ujumla, ambapo kupitia mradi huo unahakikisha jumla ya skuli 27 za msingi ambazo zinaboresha uandikishaji wa wanafunzi, kubakia na kuondoa utoro, kuimarisha lishe ya wanafunzi pamoja na mapato kwa wakulima wadogo ili kuimarika kwa ufaulu wa wanafunzi kitaaluma.

### 3.5.2 LENGO LA MRADI

Lengo kuu la mradi huu ni:-

- Kusaidia watoto walio katika mazingira magumu kuhudhuria shule na kuweza kupanua uwezo wao wa kujifunza kupitia chakula cha lishe.
- Kuboresha uandikishaji, uhifadhi, ufaulu wa kielimu kwa wanafunzi wa shule ya msingi.
- Kuongeza kipato cha wakulima wadogo.

### 3.5.3 TAARIFA YA FEDHA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MRADI

**Taarifa ya Mapato na Matumzi**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, ukaguzi umebaini mradi ulikadiriwa kupokea jumla ya dola za kimarekani 722,468 kutoka Mashirika ya Maendeleo (Table Fortwo (TfT) International na Pertnership children development (PCD). Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mradi wa HGSFP ulipokea jumla ya dola za kimarekani 263,445.23 sawa na asilimia 36.5 ya makadirio.

## MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI

### 3.5.3.1 Fedha iliyokosa maelezo ya matumizi dola za kimarekani USD 121,720.36

Ukaguzi umebaini mradi wa HGSFP umetoa fedha kupeleka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa jumla ya dola za kimarekani USD 121,720.36 zilzolipwa kupitia hati ya malipo nambari 5/10 ya tarehe 26/10/2020 lakini hadi ukaguzi unakamilika maelezo ya matumizi ya fedha hizo hayakuweza kupatikana. Kufanya hivyo kunapelekea uwepo wa viashira vya ubadhirifu katika matumizi ya fedha na rasilimali za Umma ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mradi kuhakikisha inaweka udhibiti mzuri wa matumizi kwa shughuli za mradi pamoja na kutoa maelezo ya kina juu ya matumizi ya fedha zilizotumika kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi ili kuepusha tuhuma zinazoashiria kutokuwepo kwa matumizi sahihi ya fedha

### 3.5.3.2 Malipo yasiyokuwa na vielelezo ya dola za kimarekani USD 6,535

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya USD 6,535 zimetumika kupitia hati namba 3/8 ya tarehe 30 Agosti, 2020 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ushirikiano wa kimataifa lakini vielelezo vya matumizi hayo havikupatikana kwa ukaguzi ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo ya matumizi husika.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo matumizi yasiyoridhisha ya fedha za Umma ambapo ni kwenda kinyume na Kifungu Nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha kwamba malipo yote yanayofanyika yanawekewa vielelezo pamoja na kuwasilisha matumizi na vielelezo vyake kwa ajili ya ukaguzi.

## 3.6 MRADI WA UJENZI WA DAHALIA YA WANAUME KATIKA SKULI YA SEKONDARI YA MOH'D JUMA PINDUA - PEMBA

Mradi wa ujenzi wa dahalia ya wanaume katika Skuli ya Sekondari ya Moh'd Juma Pindua ambao umetekelezwa kwa ushirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Ubalozi wa Japan kwa lengo la kuondosha changamoto ya kutokuwepo kwa Dahalia rasmi ya wanafunzi wa kiume ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakiishi katika mazingira yasioridhisha kutokana na tatizo la kutokuwepo kwa makaazi rasmi ya wanafunzi hao katika maeneo ya skuli hiyo.

### 3.6.1 TAARIFA YA FEDHA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MRADI

**Taarifa ya Mapato na Matumzi**

Baraza la Mji Mkoani limeingia Mkataba wa ujenzi na Kampuni ya Ujenzi ya M&J wenye nambari ya kumbukumbu BMM/U.H/82/VOL.1/3 kwa thamani ya shilingi 353,535,658.02 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za mradi huo ambapo kiasi cha shilingi 56,660,000 zimechangiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kiasi cha shilingi 294,571,138.81 zimechangiwa na Ubalozi wa Japan nchini Tanzania.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 3.6.1.1 Kutokuwasilishwa kwa makato ya kodi ya zuio shilingi 52,838,925

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 52,838,925 ni fedha za makato ya kodi ya zuio ambayo hayakuwasilishwa na Baraza la Mji Mkoani katika mamlaka za kodi husika (ZRB) yaliyotokana na kazi za ujenzi wa Dahalia kwa mujibu wa hati za malipo husika.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi hiyo ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha kwamba malipo ya fedha zinazotokana na utekelezaji wa miradi yanafanyika kulingana na matakwa ya sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali iliyopo.

Mchanganuo wa malipo ya makato ya kodi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 6 : Kutokuwasilishwa kwa makato ya kodi ya zuio**

| Tarehe | Maelezo | Kiasi cha fedha kilicholipwa kabla ya kodi (Tshs) | Kodi iliyokatwa (VAT 18% to ZRB) | Kiasi cha fedha kilicholipwa baada ya kodi (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 04/03/2020 | Malipo ya fedha kwa Kampuni ya M&J kwa ajili ya Ujenzi wa Dahalia ya wanaume katika Skuli ya Sekondari ya Moh'd Juma Pindua | 17,319,458.85 | 2,641,951.35 | 14,207,827.26 |
| 25/06/2019 | | 79,985,524.15 | 12,201,181.65 | 65,615,243.54 |
| 09/04/2019 | | 54,144,477 | 8,259,327 | 45,885,150 |
| 1/10/2019 | | 42,231,138 | 6,442,038 | 34,643,848 |
| 26/11/2019 | | 28,884,807 | 4,406,157 | 23,695,333 |
| 21/08/2019 | | 47,242,952 | 7,206,552 | 38,755,235 |
| 24/05/2019 | | 24,240,000 | 3,697,650 | 20,131,650 |
| 21/05/2019 | | 52,340,000 | 7,984,068 | 43,468,813 |
| **Jumla** | | **346,388,357** | **52,838,925** | **286,403,099.8** |

### 3.6.1.2 Kutokutayarisha na kuwasilisha taarifa za hesabu za miradi

Kwa mujibu wa kifungu Nambari 119(1) cha sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa fedha za Umma ya mwaka 2016 inawataka wakuu wa taasisi kutayarisha taarifa za mapato na matumizi na kuziwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kukamilika kwa matumizi.

Ukaguzi umebaini Baraza la Mji Mkoani limetekeleza Mradi wa ujenzi wa Dahalia ya wanafunzi wa kiume katika Skuli ya Sekondari ya Moh'd Juma Pindua katika eneo la Mkanyageni Wilaya ya Mkoani ambapo kwa mujibu wa taratibu za kisheria Baraza hilo linatakiwa kutayarisha na kuwasilisha taarifa za mapato na matumizi zinazohusiana na utekelezaji wa mradi huo kwa lengo la kukaguliwa na kutolewa ushauri wa kitaalamu,hadi ukaguzi unakamilika taarifa hizo hazikuwasilishwa jambo ambalo limenyima fursa ya kuweza kufahamu fedha halisi iliyopatikana na kutumika katika shughuli za uendeshaji na utekelezaji wa mradi huo.

### 3.6.1.3 Ujenzi wa dahalia kinyume na makubaliano ya mkataba

Baraza la Mji Mkoani limeingia mkataba wa ujenzi wa Dahalia iliojengwa katika Skuli ya Sekondari ya Moh'd Juma Pindua iliyopo Wilaya ya Mkoani Pemba lakini baadhi ya vipengele katika BOQ haviendani na uhalisia wa ujenzi ulivyofanyika.

Kufanya ujenzi usioendana na B.O.Q ya Mkataba kunaweza kupelekea kuongezeka kwa gharama za ujenzi, ambapo ni kwenda kinyume na makubaliano ya mkataba pamoja na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha kwamba miradi yote inapaswa kusimamiwa kwa mashirikiano ya karibu na mkandarasi wa ujenzi ili utekelezaji wa mradi huo uende sambamba na makubaliano ya mkataba wa ujenzi. Mchanganuo wa kazi za ujenzi zilizofanyika kinyume na BOQ ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 7 : Ujenzi wa Dahalia kinyume na makubaliano ya mkataba**

| Na | Kazi iliyofanywa | Kiasi cha fedha Fedha kilicholipwa (Tshs) | Baadhi ya dosari zilizobainika |
|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa paa na Silingi (Roofing and Ceiling) | 32,877,500 | Bati zisizozidi 350 zimetumika kuezekea dahalia hiyo ambapo hazifikii idadi ya bati 540 zilizostahiki kununuliwa na kutumika kwa mujibu wa B.O.Q |
| 2. | Utiaji wa madirisha na Milango (Doors and Windows) | 25,670,000 | Madirisha yametengenezwa kwa vyuma badala ya mbao ambapo ni kinyume na B.O.Q ya ujenzi huo. |
| 3. | Kazi za Umeme (Electrical works) | 21,098,000 | Taa aina ya Florescent light 16 pcs ambazo zimeingizwa kwenye B.O.Q hazikuonekana katika jengo husika |

| Na | Kazi iliyofanywa | Kiasi cha fedha Fedha kilicholipwa (Tshs) | Baadhi ya dosari zilizobainika |
|---|---|---|---|
| 4. | Mfumo wa maji safi na maji taka (Plumbing and Drainage) | 14,175,000 | Thamani ya ununuzi wa tanki la kuhifadhia maji la lita 2000 lenye thamani ya shilingi 4,700,000 kwa mujibu wa B.O.Q ni kubwa ukilinganisha na bei husika za tanki hizo |
| 5. | Malipo ya Kodi (Tax Payments) (18%VAT) | 58,186,350 | Hati za malipo ya kodi pamoja na baadhi ya vielelezo vya ulipaji kodi hizo vimekosekana kwa ukaguzi |
| 6. | Malipo ambayo yalistahiki kubakia bila kulipwa kwa muda ulioelekezwa kisheria (Retention money) | 35,353,565 | Malipo yote ya Mkandarasi yamelipwa kabla ya kipindi cha majaribio kukamilika. |

# SURA YA NNE

## 4.0 MIRADI ILIYOTEKELEZWA KATIKA SEKTA ZA FEDHA NA MIPANGO MIJI

## 4.1 MRADI WA MABORESHO YA USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA (PFMRP)

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, IMF, UNDP na DFID, kuanzia mwaka wa fedha 2002/2003 imefanya tafiti kadhaa ambazo zinalenga kubainisha maeneo yenye udhaifu kupitia Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma – (Public Finance Management Programme (PFMRP)).

Tafiti zilizofanyika ni pamoja na kufanya; tathmini ya Uwajibikaji wa Fedha Nchini (CFAA), Mapitio ya Matumizi ya Umma (PER), Mapitio ya Matumizi ya Umma na Mapitio ya Uwajibikaji wa Kifedha (PEFAR), Memoranda ya Uchumi wa Nchi, Sekta ya Karafuu Zanzibar, pamoja na Ripoti ya Tathmini ya Manunuzi ya Nchi (CPAR), na Tathmini ya Masuala ya Serikali za Mitaa. Tafiti hizi zilileta Mageuzi makubwa matatu, ambayo ni Mageuzi ya Usimamizi wa Uchumi na Fedha, Maboresho ya Taasisi na Rasilimali Watu na Maboresho ya Utawala Bora.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2005/2006 hadi 2010/2011 NORAD ilifanya utafiti kuhusu hali ya Usimamizi wa Fedha za Umma Zanzibar kwa madhumuni ya kutathmini mipango inayoendelea ya kuboresha Mfumo wa Usimamizi wa Fedha za Umma Zanzibar.

Katika utafiti uliyofanywa 2015 na DFID kuhusu tathmini ya vihatarishi ulibaini uboreshaji wa utekelezaji wa bajeti, usimamizi wa mapato na ukaguzi wa ndani, huku kukiwa na changamoto katika manunuzi, usimamizi wa kodi na mishahara pamoja na utawala wa rasilimali watu.

Awamu ya nne ya Mpango huo ilianza mwezi Julai, 2012 ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara yake ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar ilifanya mchakato wa kuleta mageuzi ya fedha zake za Umma chini ya mpango wa maboresho ya usimamizi wa fedha za umma (PFMRP) ambao unalenga kuboresha maeneo yafuatayo:

i) Usimamizi wa mapato;
ii) Bajeti na mipango;
iii) Utekelezaji wa Bajeti, uwazi na uwajibikaji
iv) Udhibiti na usimamizi wa bajeti katika taasisi mbalimbali za Serikali.

### 4.1.1 MALENGO YA MRADI

Lengo kuu la mradi ni kuipa Wizara ya Fedha na Mipango uwezo wa kutekeleza majukumu yake ya usimamizi wa fedha za umma kwa ufanisi. Mradi unalenga yafuatayo:-

- Kupitisha mbinu za hali ya juu za Usimamizi wa Fedha za Umma kuhusiana na taratibu za uhasibu, usimamizi wa fedha taslimu, na usimamizi wa madeni ya umma, kuimarisha ukaguzi wa ndani, na mfumo wa mishahara kwa uwazi na uwajibikaji.
- Kufanya maandalizi ya bajeti kwa wakati, kuboresha ubora wa bajeti na kufanya utafiti wa mapato, kutayarisha taarifa za utekelezaji wa bajeti na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mara kwa mara ya bajeti kupitia mapitio ya matumizi ya Umma.
- Mradi uweze kudumisha msingi wa uingizwaji wa taarifa za rasilimali za kigeni, kufuatilia utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na wafadhili, na kuandaa ripoti za mara kwa mara kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa miradi.
- Kuwajengea uzoefu bora kwa kufuata taratibu za manunuzi ya Serikali, kuelewa Sheria mpya ya ununuzi na kuitekeleza kwa ufanisi, kuweka kumbukumbu za mali za umma ipasavyo na thamani yake.
- Kuimarisha uwajibikaji na uwazi katika matumizi ya rasilimali za umma na Serikali;
- Kuongeza uwezo maalum katika kukusanya mapato ya ndani

### 4.1.2 TAARIFA YA FEDHA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MRADI

**Taarifa ya Mapato na Matumzi**

Mradi wa PFMRP ulikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 3,596,586,531 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mradi umetumia kiasi cha shilingi 1,430,544,872 sawa na asilimia 40 na kupelekea kuwepo kwa kiasi cha fedha isiyotumika yenye jumla ya shilingi 2,166,041,659 ambayo ni sawa na asilimia 60 ya makadirio. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyonekana hapo chini:-

**Jadweli Nambari 8 : Makadirio ya mapato na matumzi ya Mradi wa PFMRP**

| Maelezo | Kiasi cha fedha (Tshs) |
|---|---|
| Salio la kuanzia, 1 Julai,2020 | 1,977,560,242 |
| **Fedha zilizopokelewa:** | |
| Shirika la maendeleo(DFID) | 1,619,026,289 |
| Mchango wa serikali | 0 |
| Jumla ya fedha iliyopokelewa | 1,619,026,289 |
| **Jumla ya fedha iliyopatikana** | **3,596,586,531** |
| Matumizi kwa 2020/2021 | 1,430,544,872 |
| **Salio la mwisho 30 Juni,2021** | **2,166,041,659** |

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 4.1.2.1 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 38,415,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 38,415,000 zimetumika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa PFMRP lakini vielelezo vya matumizi ya fedha hizo havikupatikana kwa ukaguzi ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo ya matumizi husika.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo matumizi yasiyoridhisha ya fedha za Umma ambapo ni kwenda kinyume na Kifungu Nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha kwamba malipo yote yanawekewa vielelezo na kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 9 : Malipo yasiyokuwa na vielelezo**

| Tarehe | Utekelezaji wa shughuli ya mradi | Idara iliyohusika | Kiasi<br>Cha fedha kilichotumika (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 09.03.21 | Mafunzo kwa ajili ya kuwajengea uwezo kwa PDEs (wafanyakazi wa PMUs) juu ya miongozo ya ununuzi | ZPPDA | 29,085,000 |
| 08.07.20 | Kusaidia uratibu wa programu Zanzibar ifikapo Juni,2021 | PFMRP | 5,120,000 |
| 14.08.20 | Kusaidia uratibu wa programu Zanzibar ifikapo Juni,2021 | PFMRP | 4,210,000 |
| **Jumla** | | | **38,415,000** |

## 4.2 MRADI WA HUDUMA ZA JAMII MIJINI ZANZIBAR (ZUSP)

Mradi wa Huduma za Jamii Mijini Zanzibar (Zanzibar Urban Service Project -ZUSP) ni mradi unaosaidia utoaji wa huduma za msingi za miundombinu, uimarishaji wa taasisi na uhifadhi wa urithi wa kitamaduni.

Lengo la Maendeleo ya Mradi (PDO), ulirekebisha mfumo wa matokeo (RF), na kuongeza tarehe ya kufunga mikopo kutoka tarehe 30 Juni, 2016 hadi 31 Desemba 2020 ambapo mradi uliengezwa muda hadi kufikia tarehe 31 Mei 2021.

Walengwa wakuu wa Mradi wa Huduma za Miji Zanzibar (ZUSP) ni Baraza la Manispaa Zanzibar (ZMC) na Mabaraza ya Miji mitatu ya Pemba (Mabaraza ya Miji ya Wete, Chake Chake na Mkoani); Timu ya Usimamizi wa Miradi ambayo iko chini ya Wizara ya Fedha na Mipango; Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe (STCDA) na Idara ya Mipango Miji na Vijijini (DoURP) ambazo ziko chini ya Wizara ya Ardhi.

### 4.2.1 VIPENGELE VYA MRADI

ZUSP AF ina vipengele vikuu vitatu (3) kama ifuatavyo :-

**Kipengele cha 1:** Uimarishaji wa Taasisi na Maendeleo ya Miundombinu katika Eneo la Baraza la Manispaa Zanzibar (ZMC) (Dola za Marekani milioni 35.5).

Kipengele hiki kitazingatia ZMC katika Kisiwa cha Unguja na kitajumuisha vipengele vidogo kama ifuatavyo:-

- Uwekezaji katika usafi wa mazingira mijini, ikijumuisha ukusanyaji wa taka ngumu, usafirishaji, uhamishaji na uendelezaji wa dampo la taka na vifaa vya matibabu ya uchafu wa maji taka;
- Uboreshaji na uendelezaji upya wa eneo la Ng'ambo, ikijumuisha miundombinu ya kimsingi, maeneo mapya ya kijani kibichi na maeneo ya burudani, usaidizi wa uhifadhi wa urithi wa kitamaduni, na maendeleo ya masoko ya umma;
- Kusaidia fedha za manispaa ya ZMC kwa kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya vyanzo vyake (OSR) kuwa ya kisasa na kuendeleza mipango mipya ya PPP;
- Kukamilisha na kuongeza kazi chini ya mradi wa awali, ikiwa ni pamoja na mifereji ya maji ya dhoruba na taa za barabarani, kwa kuzingatia manufaa yao muhimu ya kimazingira na kijamii kwa jumuiya za mitaa;
- Msaada wa uimarishaji wa kitaasisi kwa RGoZ na ZMC juu ya mkakati wa usimamizi wa taka ngumu, usimamizi wa mali, mfumo wa habari, na ushirikishwaji wa jamii;
- Gharama ya makazi mapya inayohusishwa na kazi za mifereji ya maji ya dhoruba iliyofadhiliwa chini ya mradi wa asili.

**Kipengele cha 2**: Msaada kwa Mabaraza ya Miji Kisiwani Pemba (Dola za Marekani milioni 5.0). Sehemu ya 2 inajumuisha;

- Kuongeza uwekezaji mdogo katika utoaji wa miundombinu ya kimsingi kama vile taa za barabarani, njia za waenda kwa miguu, na masoko ya ndani; na

- Msaada wa uimarishaji wa kitaasisi kwa Mabaraza matatu ya miji Kisiwani Pemba kuhusu mipango miji, usimamizi wa mali, usimamizi wa fedha, mfumo wa taarifa na ushirikishwaji wa jamii.

**Kipengele cha 3:** Usimamizi wa Mradi (Dola za Marekani milioni 3.5). Sehemu hii inatoa msaada kwa PMT kwa upanuzi wa usimamizi wa mradi wa mradi asilia na AF, ikijumuisha ufuatiliaji wa mara kwa mara wa shughuli za mradi, ufuatiliaji na ukaguzi wa ulinzi, ufuatiliaji na tathmini ya matokeo, usimamizi wa uaminifu na ukaguzi, mawasiliano na gharama za uendeshaji wa ofisi. Pia itarahisisha wizara nyingine zinazotekeleza na idara zinazohusika na vipengele vidogo maalum kutekeleza na kuratibu shughuli zao husika. Aidha, itasaidia utambuzi na upembuzi yakinifu kwa ajili ya bomba la uendeshaji mijini hapo baadaye Zanzibar.

### 4.2.2 MALENGO YA MRADI

Madhumuni ya Ufadhili wa Ziada wa ZUSP ni kuboresha upatikanaji wa huduma za mijini na kuhifadhi urithi wa kitamaduni wa Zanzibar. Ufadhili wa ziada wa ZUSP ulikadiriwa kugharimu jumla Dola za Marekani milioni 55 kutoka Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA), fedha hiyo itatumika katika kipindi cha mradi wa miaka mitatu kuanzia Agosti ,2016 hadi Desemba, 2020.

### 4.2.3 VYANZO VYA FEDHA VYA MRADI

Mradi ulikuwa na jumla ya USD 15,781149.05 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ikijumuisha salio la kuanzia la USD 2,598,659.96. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 kulikuwa na bakaa ya kiasi cha dola za kimarekani USD 1,637,818.31, hii inaashiria kuwa Mradi umetumia kiasi cha dola za kimarekani USD. 14,143,330.74 sawa na asilimia 90. Fedha isiyotumika ya dola za kimarekani USD 1,637,818.31 itatumika kwa ajili ya kazi zilizoidhinishwa na hazikufanyika katika kipindi cha mwaka husika ambazo zitajumuishwa katika utekelezaji wa mwaka unaofuata. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyonekana hapo chini:-

**Jadweli Nambari 10 : Taarifa za fedha za mradi**

| Maelezo | Kiasi cha fedha kilichotumika (USD) |
|---|---|
| Salio anzia 1 Julai,2020 | 2,598,659.96 |
| **Fedha zilizopokelewa:** | |
| Jumuiya ya Maendeleo ya Kimataifa (IDA) | 13,182,489.08 |
| Mchango wa serikali | 0 |
| Jumla ya fedha iliyopokelewa | 13,182,489.08 |
| **Jumla ya fedha iliyopatikana** | **15,781149.05** |
| Matumizi kwa 2020/2021 | 14,143,330.74 |
| Salio la mwisho 30Juni,2021 | 1,637,818.31 |

## 4.2.4 TAARIFA YA FEDHA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MRADI

### Taarifa ya Mapato na Matumzi

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ,ukaguzi umebaini mradi ulikadiriwa kupokea jumla ya USD 15,000,000 kutoka Shirika ya Maendeleo ya Kimataifa (IDA). Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mradi wa ZUSP ulipokea jumla ya dola za kimarekani 13,182,489.08 sawa na asilimia 88 ya makadirio kukiwa na upungufu wa dola za kimarekani 1,817,510.92 sawa na asilimia 12 ya makadirio .

### MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI

### 4.2.4.1 Kutokutekelezwa kwa Mradi wa Uondoaji wa Maji katika Bwawa la Mwantenga shilingi 1,736,773,216.56

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 1,736,773,216.56 zilipaswa kutumika katika utekelzaji wa mradi wa uondoaji wa maji katika Bwawa la Mwantenga katika awamu ya kwanza, lakini utekelezaji wa mradi huo katika awamu iliyopangwa haukufanyika hali iliyopelekea kupangwa kufanyika katika awamu ya pili ambayo pia haukufanyika licha ya fedha za utekelzaji wa mradi huo kutolewa kwa wakati.

Kufanya hivyo kunaweza kukupelekea kuwepo kwa viashiria vya kufanyika kwa ubadhirifu wa fedha za Umma pamoja na uwezekano wa kuathithiri makaazi ya wananchi wa maeneo hayo katika nyakati za mvua kubwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa Zanzibar (ZMC) kuhakikisha unafanya ufuatiliaji wa fedha za utekelezaji wa miradi inayopangwa ili miradi hiyo iweze kufanyika ili kuweza kupunguza athari ambazo zinaweza kujitokeza kutokana na kutokufanyika kwa miradi hiyo. Hali halisi ya bwawa la Mwantenga ni kama inavyoonekana katika picha hapo chini:-



*Bwawa la Mwantenga*

### 4.2.4.2 Kutokufanyakazi kwa mfumo wa maji taka katika jaa la Kibele shilingi 1,246,124,300

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa jaa la Kibele ambalo limewekewa mfumo wa maji taka (PCW) wenye jumla ya shilingi 1,246,124,300 lakini hadi ukaguzi unakamilika imebainika kuziba kwa mabomba yanayopitisha maji hayo na kupelekea mfumo huo kutokufanya kazi.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa matumizi yasiyoridhisha ya fedha za Umma ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Manispaa kuhakikisha unasimamia ipasavyo miradi inayotekelezwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ya kuanzishwa kwa miradi hiyo. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika picha ya hapo chini:-



*Kutokufanyakazi kwa mfumo wa maji taka katika jaa la Kibele*

### 4.2.4.3 Kutokutumika kwa vifaa vya usagaji wa taka vilivyonunuliwa USD 420,580

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Fedha na Mipango imetumia jumla ya USD 420,580 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kusagia taka, gharama za ufungaji pamoja na mafunzo ya kuvitumia vifaa hivyo katika jaa la Kibele lakini hadi ukaguzi huu unakamilika vifaa vilivyonunuliwa na kupokelewa miezi tisa iliyopita ambavyo ni trekta la kilimo, mashine ya kugeuza na trela ya tanki la maji bado havijaanza kutumika kama ilivyokusudiwa.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa matumizi yasiyoridhisha ya fedha za Umma ambapo pia ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa Zanzibar kuhakikisha Sheria, Kanuni na miongozo ya ununuzi na utumiaji wa vifaa vilivyonunuliwa inafuatwa kikamilifu. Hali halisi ya vifaa vilivyonunuliwa ni kama inavyoonekana katika picha hapo chini:-



*Kutokukutumika kwa vifaa vya usagaji wa taka vilivyonunuliwa*



#### 4.2.4.4 Kutokutumika kwa mfumo wa Usimamizi wa fedha USD 6,276

Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar imeingia makubaliano ya mkataba na M/S Core Soft Limited ya Zanzibar kwa thamani dola za Kimarekani 56,404 kwa ajili ya usambazaji wa toleo jipya la mfumo wa usimamizi wa fedha (NAV system) katika Mradi wa ZUSP ambapo malipo ya fedha hizo yalifanywa kupitia hati za malipo nambari PV/PBZ/F/20 ya tarehe 21/9/20 yenye thamni ya dola za Kimarekani 2,500 na hati nambari PV/PBZ/F/20 ya tarehe 21/8/30 yenye thamani ya dola za Kimarekani 3,776

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokufanyakazi kwa mfumo wa usimamizi wa fedha na kupelekea taarifa za uhasibu za Mradi huo kuandaliwa kwa fomu ya excel.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha za Umma ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa Zanzibar kuhakikisha Sheria, Kanuni na miongozo mbali mbali inafuatwa kikamilifu ikiwa ni pamoja na kusimamia makubaliano yaliyofikiwa katika matumizi ya mfumo wa usimamizi wa fedha wa NAV System ili kuepusha matumizi ya fedha yasiyokuwa na tija kwa Serikali na jamii kwa ujumla.

## 4.3 MRADI WA UJENZI WA UKUMBI WA MIKUTANO WA UMOJA NI NGUVU - PEMBA

Mradi wa Ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano wa Umoja ni Nguvu ni mradi ambao umesimamiwa na Baraza la Mji Mkoani na umetekelezwa kutokana na agizo la Rais mstaafu wa Zanzibar Mhe. Dkt. Ali Moh'd Shein kuhakikisha kwamba Baraza la Mji Mkoani linajenga ukumbi wa mikutano ambao utaweza kuondosha changamoto zinazojitokeza katika kipindi cha kufanya mikutano na kuepuka kuingia gharama za kukodi ukumbi katika maeneo yasiokuwa rasmi.

### 4.3.1 MALENGO YA MRADI

Lengo la kuanzishwa kwa mradi huu ni pamoja na kupunguza changamoto za upatikanaji wa ukumbi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mikutano zinazohitaji matumizi ya ukumbi wenye ubora na uwepo wa nafasi yenye kujitosheleza pia kukamilika kwa ukumbi uliokusudiwa ni moja ya chanzo cha upatikanaji wa mapato ya Baraza la Mji Mkoani, kutokana na ukodishwaji wa ukumbi huo kwa ajili ya shughuli mbali mbali za kijamii.

### 4.3.2 TAARIFA ZA FEDHA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MRADI

**Taarifa ya Mapato na Matumizi**

Mradi huu umetekelezwa kwa kutumia wakandarasi wawili katika awamu mbili tofauti kama ifuatavyo:-

- Zenji Building ambaye alisaini mkataba wenye namba ya kumbu kumbu SMZ/BMM/Q/2018-2019/002 kwa jumla ya shilingi 286,604,890 pamoja na VAT ambapo katika mkataba huo mkandarasi alitakiwa kuanza ujenzi kwa hatua za awali hadi katika hatua za uwezekaji.
- Chuo cha Mafunzo ambaye alisaini mkataba wenye namba ya kumbu kumbu SMZ/BMM/DP/2018-2019-02 kwa jumla ya shilingi 386,137,890 pamoja na VAT ambapo katika mkataba huo mkandarasi alitakiwa kuanza ujenzi kwa hatua za umaliziaji hadi kukamilika kwa kazi za ujenzi na kukabidhi ukumbi kwa ajili ya matumizi.

### MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI

#### 4.3.2.1 Mambo yaliyobainika katika ujenzi wa ukumbi wa Umoja ni Nguvu

Kazi za ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano wa Umoja ni Nguvu zilitekelezwa na wakandarasi ambao ni Zenji Building pamoja na Chuo cha Mafunzo katika vipindi vya awamu mbili tofauti ambapo katika hatua za ujenzi huo mambo mbali mbali yalibainika kama ifuatavyo:-

- Kutokufuatwa kwa utaratibu wa utowaji wa zabuni ya kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa ukumbi

- Kutokufuatwa kwa utaratibu wa utoaji wa zabuni ya kuwapata wakandarasi katika ujenzi wa uzio
- Kutokuwepo kwa vipengele vya adhabu ndani ya mikataba ya ujenzi.
- Kutokufuatwa kwa utaratibu katika hatua za kumpata mshauri elekezi.
- Kutokuwepo kwa uthibitisho wa makubaliano ya nyongeza ya kazi.
- Kukosekana kwa vyeti vya malipo (certificate of completion).

#### 4.3.2.2 Kutokukamilika kwa kazi za ujenzi wa ukumbi

Barara la Mji Mkoani limeingia mikataba ya ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano yenye jumla ya shilingi 672,742,780 na Wakandarasi ambao ni Zenji Building na Chuo cha Mafunzo kwa awamu mbili tofauti kwa mkataba nambari SMZ/BMM/Q/2018-2019/002 wenye jumla ya shilingi 286,604,890 pamoja na kodi na mkataba nambari SMZ/BMM/DP/2018-2019/02 wenye jumla ya shilingi 386,137,890 pamoja na kodi.

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Chuo cha Mafunzo ambae ni mkandarasi wa awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi alipaswa kukamilisha kazi aliyopangiwa ndani ya tarehe 13/12/2019 lakini hadi ukaguzi unakamilika mkandarasi huyo ameshindwa kukamilisha ujenzi na hivyo kupelekea mradi huo kutokamilika kwa wakati, ambapo imebainika kwamba baadhi ya kazi zenye thamani ya shilingi 100,000,000 zimeshindwa kukamilishwa licha ya mkandarasi huyo kulipwa fedha zote zilizoainishwa katika mkataba hali ambayo imesababisha kutokupatikana kwa tija inayotokana na malengo ya kuanzishwa kwa ujenzi huo.

Aidha ukaguzi umeshindwa kuona vielelezo vya kuomba na kukubaliwa kuongezewa muda wa utekelezaji wa mkataba wa mradi huo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha kwamba miradi yote wanayopaswa kuisimamia wanashirikiana kwa pamoja na wakandarasi ili utekelezaji wa miradi hiyo uende sambamba na mikataba ya ujenzi.

#### 4.3.2.3 Ujenzi wa Ukumbi kinyume na makubaliano ya mkataba

Baraza la Mji Mkoani limeingia mkataba wa ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano wa Umoja ni Nguvu uliojengwa katika Wilaya ya Mkoani Pemba lakini baadhi ya vipengele katika BOQ haviendani na uhalisia wa ujenzi ulivyofanyika.

Kufanya ujenzi usioendana na B.O.Q ya Mkataba kunaweza kupelekea kuongezeka kwa gharama za ujenzi, ambapo ni kwenda kinyume na makubaliano ya mkataba pamoja na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha kwamba miradi yote wanayopaswa kuisimamia wanashirikiana kwa pamoja na wakandarasi ili utekelezaji wa miradi hiyo uende sambamba na makubaliano ya mikataba ya ujenzi. Mchanganuo wa kazi za ujenzi zilizofanyika kinyume na BOQ ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 11: Ujenzi wa Ukumbi kinyume na makubaliano ya mkataba**

| Na | Maelezo ya kazi za ujenzi | Kazi zilizoainishwa katika mkataba | Kazi halisi zilizotekelezwa | Tofauti |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ununuzi wa Milango Mikubwa (Zanzibar Doors) | Mlango 1 | Milango 10 | Milango 9 |
| 2. | Urefu na upana wa ukumbi | Urefu mita 34 upana mita 15 | Urefu mita 38 Upana mita 19.4 | Urefu mita 4 na upana mita 4.4 |
| 3. | Ununuzi wa Jipsumboard | 550pcs | 300pcs | 250pcs |
| 4. | Ununuzi wa Cornices | 420pcs | 250pcs | 170pcs |
| 5. | Ujenzi wa Uzio wa thamani ya shilingi 87,775,475 | Haumo | Umejengwa | Kujengwa |

### 4.3.2.4 Kutokukatwa kwa kodi ya zuio shilingi 19,333,234.56

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 19,333,234.56 ni fedha za kodi ambazo hazikukatwa na Baraza la Mji Mkoani kwa ajili ya kazi za ujenzi wa ukumbi wa Mikutano wa Umoja ni Nguvu kulingana na mikataba ya ujenzi huo ambapo kupitia mikataba hiyo jumla ya makato ya kodi ya zuio yaliyostahiki kukatwa wakandarasi ni shilingi 138,796,470.36 lakini makato halisi yaliyofanyika kupitia hati za malipo ni shilingi 119,463,236.2 na kupelekea uwepo wa tofauti ya makato ya kodi ya zuio kama ilivyobainishwa hapo juu.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi hiyo ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha kwamba malipo ya fedha zinazotokana na utekelezaji wa miradi yanafanyika kulingana na matakwa ya sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali iliyopo. Mchanganuo wa malipo ya kodi ya zuio ni kama inavyoonekana katika majadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 12: Kodi iliyostahiki kulipwa Serikalini kwa mujibu wa mkataba**

| Mkandarasi | Nambari ya Mkataba | Malipo Kabla ya Kodi | Malipo Yanayostahiki Kulipwa Mkandarasi | Kodi ya VAT ya 18% Inayostahiki Kulipwa ZRB (A) | Kodi ya Bidhaa ya 2% ya (60%) na Huduma ya 5% ya 40% Inayostahiki Kulipwa TRA (B) |
|---|---|---|---|---|---|
| Zenji Building Construction | SMZ/ BMM /Q / 2018 - 2019/002 (Ujenzi wa Ukumbi wa Umoja ni Nguvu) | 286,604,890 | 227,445,497.68 | 51,588,880.2 | 7,570,512.12 |
| Chuo Cha Mafunzo | SMZ/BMM/ DP/2018-2019/02 (Ujenzi wa Ukumbi wa Umoja ni Nguvu) | 386,137,890 | 306,500,811.56 | 69,504,820.2 | 10,132,258.24 |
| **Jumla** | | **672,742,780** | **533,946,309.24** | **121,093,700.4** | **17,702,770.36** |
| **Jumla (A+B)** | | | | **138,796,470.76** | |

**Jadweli Nambari 13:Kodi iliokatwa kwa mujibu wa hati za malipo**

| Hati Namba | Hundi Namba | Aliyelipwa | Malipo Kabla ya Kodi (A) | Malipo Baada ya Kodi (B) |
|---|---|---|---|---|
| 2/6 ya 03/06/2019 | T.O | Zenji Building | 143,302,445 | 119,013,895 |
| 84/7 ya 26/07/2019 | | | 94,911,136.35 | 77,924,932 |
| 33/9 ya 02/09/2019 | | | 47,200,000 | 38,720,000 |
| 68/2 ya 24/02/2020 | | Magereza | 227,821,355 | 183,485,003 |
| 21/7 ya 22/07/2020 | | | 137,821,355.10 | 112,449,225.25 |
| 1/8 ya 22/07/2020 | | Wakala wa Majengo (ZBA) | 4,655,000 | 4,655,000 |
| **Jumla** | | | **655,711,291.45** | **536,248,055.25** |
| **Kodi iliokatwa kwa mujibu wa hati za malipo (A-B)** | | | **119,463,236.2** | |

**Jadweli Nambari 14: Kodi halisi iliyowasilishwa**

| Hati Namba | Hundi Namba | Jina la Mtoa Huduma | Kodi ya VAT ya 18% Iliyolipwa ZRB (A) | Kodi ya Bidhaa ya 2% ya (60%) na Huduma na 5% ya 40% Iliyolipwa TRA (B) |
|---|---|---|---|---|
| 4/6 ya 03/06/2019 | 003404 | Zenji Building | 21,859,695 | - |
| 73/08 ya 09/08/2019 | 003576 | | 14,490,173.34 | - |
| 17/7 ya 22/07/2019 | 004158 | Chuo cha Mafunzo | 55,662,390 | - |
| 13/8 ya 07/08/2020 | 004186 | | - | 6,178,206.24 |
| **Jumla** | | | **92,012,258.34** | **6,178,206.24** |
| **Jumla ya kodi iliyolipwa (A+B)** | | | **98,190,464.58** | |

### 4.3.2.5 Kutokuwasilishwa kwa makato ya kodi ya zuio shilingi 21,272,771.62

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 21,272,771.62 ni fedha za makato ya kodi ya zuio ambayo hayakuwasilishwa na Baraza la Mji Mkoani katika mamlaka za kodi husika yaliyotokana na kazi za ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano wa Umoja ni Nguvu.

Kwa mujibu wa hati za malipo husika, fedha walizokatwa wakandarasi wa ujenzi huo ni jumla ya shilingi 119,463,236.2 ambazo zilitakiwa kuwasilishwa katika mamlaka husika za kodi, lakini kodi halisi iliyowasilishwa ni shilingi 98,190,464.58 na kupelekea uwepo wa tofauti ya makato ya kodi ya zuio ambayo hayakuwasilishwa.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi hiyo ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha kwamba malipo ya fedha zinazotokana na utekelezaji wa miradi yanafanyika kulingana na matakwa ya sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali iliyopo. Mchanganuo wa malipo ya kodi ya zuio ambayo hayakuwasilishwa Serikalini ni kama inavyoonekana katika majadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 15:Kodi iliokatwa kwa mujibu wa hati za malipo

| Hati Namba | Hundi Namba | Aliyelipwa | Malipo Kabla ya Kodi (A) | Malipo Baada ya Kodi (B) |
|---|---|---|---|---|
| 2/6 ya 03/06/2019 | T.O | Zenji Building | 143,302,445 | 119,013,895 |
| 84/7 ya 26/07/2019 | | | 94,911,136.35 | 77,924,932 |
| 33/9 ya 02/09/2019 | | | 47,200,000 | 38,720,000 |
| 68/2 ya 24/02/2020 | | Magereza | 227,821,355 | 183,485,003 |
| 21/7 ya 22/07/2020 | | | 137,821,355.10 | 112,449,225.25 |
| 1/8 ya 22/07/2020 | | Wakala wa Majengo (ZBA) | 4,655,000 | 4,655,000 |
| **Jumla** | | | **655,711,291.45** | **536,248,055.25** |
| **Kodi iliokatwa kwa mujibu wa hati za malipo (A-B)** | | | **119,463,236.2** | |

### Jadweli Nambari 16: Kodi halisi iliyowasilishwa

| Hati Namba | Hundi Namba | Jina la Mtoa Huduma | Kodi ya VAT ya 18% Iliyolipwa ZRB (A) | Kodi ya Bidhaa ya 2% ya (60%) na Huduma na 5% ya 40% Iliyolipwa TRA (B) |
|---|---|---|---|---|
| 4/6 ya 03/06/2019 | 003404 | Zenji Building | 21,859,695 | - |
| 73/08 ya 09/08/2019 | 003576 | | 14,490,173.34 | - |
| 17/7 ya 22/07/2019 | 004158 | Chuo cha Mafunzo | 55,662,390 | - |
| 13/8 ya 07/08/2020 | 004186 | | - | 6,178,206.24 |
| **Jumla** | | | **92,012,258.34** | **6,178,206.24** |
| **Jumla ya kodi iliyolipwa (A+B)** | | | **98,190,464.58** | |

### 4.3.2.6 Uwepo wa malipo ya ziada kwa mkandarasi shilingi 8,212,936.32

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 8,212,936.32 ni fedha za malipo ya ziada aliyolipwa mkandarasi wa ujenzi Zenji Construction Co. Ltd kwa ajili ya ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano wa Umoja ni Nguvu. Kwa mujibu wa mkataba mkandarasi huyo alistahiki kulipwa jumla ya shilingi 227,445,497.68 baada ya kodi, lakini fedha halisi alizolipwa ni shilingi 235,658,434 na kupelekea uwepo wa tofauti ya malipo ya ziada kama yalivyobainishwa hapo juu.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi hiyo ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha kwamba malipo ya fedha zinazotokana na utekelezaji wa miradi yanafanyika kulingana na matakwa ya sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali iliyopo.

### 4.3.2.7 Kutokufanyika kwa malipo yatokanayo na ujenzi shilingi 23,911,583.56

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 23,911,583.56 ni fedha ambazo zilizopaswa kulipwa kwa ajili ya kazi za ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano wa Umoja ni Nguvu katika Wilaya ya Mkoani Pemba. Kwa mujibu wa mkataba wa ujenzi mkandarasi ambaye ni Chuo cha Mafunzo alistahiki kulipwa jumla ya shilingi 306,500,811.56 malipo baada ya kodi,lakini fedha halisi alizolipwa ni shilingi 295,934,228 na kupelekea uwepo wa tofauti ya shilingi 10,566,583.56. Aidha malipo ya mshauri elekezi kwa mujibu wa mkataba wa ujenzi ni shilingi 18,000,000 lakini fedha halisi alizolipwa ni shilingi 4,655,000 na kupelekea uwepo wa tofauti ya shilingi 13,345,000 hali ambayo inaweza kusababisha kukosekana kwa ufanisi katika usimamizi na ufuatiliaji wa kazi za ujenzi, pamoja na kwamba katika ufuatiliaji wa mwenendo wa utekelezaji wa mradi na ufanisi wa uingizwaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa ukumbi pamoja na malipo stahiki kwa mshauri elekezi imebainika kwamba fedha zote zilizostahiki kwa ajili ya ujenzi huo zimeingizwa na kutumika kwa asilimia 100 na kwa kuzingatia wakati uliopangwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha kwamba malipo ya fedha zinazotokana na utekelezaji wa miradi yanafanyika kulingana na matakwa ya sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali iliyopo.

#### 4.3.2.8 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 4,655,000

Katika ukaguzi uliyofanyika imebainika kuwepo kwa malipo yenye jumla ya shilingi 4,655,000 zilizolipwa na Baraza la Mji Mkoani kwa Mshauri Elekezi wa Ujenzi wa ukumbi wa Umoja ni Nguvu uliopo katika Wilaya Mkoani Pemba ambapo malipo hayo yamefanyika kwa kupitia hati ya malipo nambari 1/8 ya tarehe 22/7/2020 lakini vielelezo husika havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha malipo yote yanayofanyika ni lazima yaambatanishwa na vielelezo husika ili kuendana na matakwa ya sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali iliyopo.

#### 4.3.2.9 Kukosekana kwa hati za malipo kwa ajili ya ukaguzi shilingi 38,394,260.17

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Barara la Mji Mkoani limeingiziwa jumla ya shilingi 672,742,780 kwa ajili ya Ujenzi wa Ukumbi wa Umoja ni Nguvu kutoka Wizara ya Nchi (OR) Fedha na Mipango Pemba ambapo katika ufuatiliaji wa fedha hizo imebainika fedha halisi zilizoandaliwa hati za malipo na kukaguliwa ni shilingi 634,348,519.83 hivyo kupelekea uwepo wa tofauti ya fedha jumla ya shilingi 38,394,260.17 ambazo hati za malipo pamoja na vielelezo vinavyothibitisha kufanyika kwa malipo hayo zimekosekana kwa ajili ya ukaguzi na kupelekea kushindwa kuthibitisha uhalali wa malipo hayo, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha malipo yote yanayofanyika ni lazima yaambatanishwe na vielelezo husika ili kuendana na matakwa ya sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali iliyopo. Mchanganuo wa malipo yaliofanyika ni kama inavyoonekana hapo chini:-

**Jadweli Nambari 17 : Malipo ya fedha yaliokosekana kwa ukaguzi**

| Maelezo | Kiasi cha Fedha kilicholipwa (Tshs) |
|---|---|
| **Fedha zilizoingizwa (A)** | **672,742,780** |
| **Fedha zilizotumika** | |
| Zenji Building Construction Limited | 235,568,827 |
| Chuo cha Mafunzo | 295,934,228.25 |
| Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) | 92,012,258.34 |
| Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) | 6,178,206.24 |
| Wakala wa Majengo (ZBA) | 4,655,000 |
| **Jumla ya fedha zilizotumika (B)** | **634,348,519.83** |
| **Fedha zilizokosekana kwa ukaguzi (A-B)** | **38,394,260.17** |

## 4.4 MIRADI YA UJENZI WA MAHANGA YA KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) - PEMBA

Ukaguzi wa Hesabu za Miradi ya Ujenzi wa Mahanga ya Kulalia Wapiganaji wa Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo (KMKM) Pemba kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za ukaguzi wa mahesabu. Matokeo ya kazi hii yanatokana na ukaguzi wa kumbukumbu za Hesabu za Miradi pamoja na shughuli za Miradi hiyo pamoja na mfumo wa tathmini wa udhibiti wa ndani wa Mradi (Internal Control) ambao unahitaji uangalizi wa Uongozi wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo ambacho ndio msimamizi wa Miradi hiyo.

### 4.4.1 MALENGO YA MRADI

Lengo kuu la kuanzishwa kwa Miradi ya Ujenzi wa Mahanga ya kulalia Wapiganaji wa Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo (KMKM) ni kuboresha makaazi ya wapiganaji kwa kuwapatia makaazi maalum, pamoja na kuwezesha utoaji wa huduma za baharini kwa wakati.

Pamoja na uwepo wa malengo hayo ukaguzi umefanyika ili kuweza kutathmini hatua ya utekelezaji wa lengo hilo kwa kutembelea maeneo mbali mbali na kujionea hali halisi ya ujenzi na utekelezaji wa mradi huo ili kupima ufanisi na tija kwa malengo ya mradi huo. Katika maeneo yaliyotekelezwa mradi huo na ambayo mradi upo katika hali nzuri na umekamilika na unatumika ni eneo la Hanga la Kiuyu Mbuyuni liliopo Wilaya ya Micheweni, na ujenzi wa hanga katika eneo la Wete umefikia katika hali ya kuridhisha na limeshaezekwa na hivyo kutokukamilika kwa ajili ya matumizi.

### 4.4.2 TAARIFA ZA FEDHA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MRADI

**Taarifa ya Mapato na Matumizi**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya shilingi 350,459,000 zilitumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa mahanga ya Kiuyu Mbuyuni kutoka hatua ya uwezekaji hadi hatua ya mapambo na shilingi 350,000,000 ziliingizwa na kutumika kwa ajili ya ujenzi wa hanga la Wete kuanzia hatua ya awali hadi kukamilika kwa mradi.

### 4.4.3 UTEKELEZAJI WA MRADI WA MAHANGA KIUYU MBUYUNI NA WETE

Katika utekelezaji wa mradi huo ulianza kwa hatua ya muendelezo kuanzia sehemu ya juu kwa thamani ya shilingi 350,459,000 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali vya kuweza kumalizia hatua uliobakia,dosari iliobainika katika ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa taarifa za fedha zilitumika katika utekelezaji wa ujenzi wa hanga la Wete pamoja na vielelezo husika vya ujenzi huo katika hatua za awali hadi kufikia hatua ya gebo.
- Kukosekana kwa michoro ya majengo hayo jambo ambalo limepelekea kushindwa kujiridhisha na kulinganisha juu ya thamani ya fedha iliyotumika kulingana na aina ya mchoro wenyewe,hata hivyo ukaguzi haukuweza kupatiwa ripoti ya upembuzi yakinifu ambayo itatoa dira ya thamani halisi ya fedha na kiwango cha ujenzi wenyewe.
- Katika utekelezaji wa mradi huo ukaguzi haukuweza kupatiwa nyaraka za uthibitisho wa utolewaji wa zabuni ili kuweza kupima thamani halisi ya fedha iliyotumika na aina ya ujenzi wenyewe ulivyo kwa kukosekana ulinganisho wa bei. Hata hivyo ukaguzi haukuweza kupatiwa taarifa za kifedha (bank statement) zinazohusiana na matumizi ya vifaa vya mradi huo.
- Kukosekana kwa ripoti ya mshauri elekezi ambayo itaonyesha aina ya nyumba zinazopaswa kujengwa pamoja na thamani halisi ya ujenzi huo na kupelekea kupatikana kwa ripoti ya utekelezaji kwa lengo la kupima ufanisi wa mradi.

- Kukosekana kwa taarifa za kumbu kumbu za vifa vilivyonunuliwa na kutumika kwa ajili ya ujenzi vyenye thamani za shilingi 350,459,000 hali ambayo imepelekea kutokujua vifaa vilivyonunuliwa,vifaa vilivyopokewa pamoja na vifaa vilivyotumika.

Kutokana na kubainika kwa dosari hizo kunapelekea kushindwa kujiridhisha juu ya matumizi halisi ya fedha yaliofanywa ambapo kunaweza kujitokeza kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha za umma. Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kuhakiksha unazifanyia kazi dosari zote zilizobainishwa kwa lengo la kupatikana kwa tija ya matumizi ya fedha na rasilimali za umma.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

**4.4.3.1 Malipo ya ujenzi wa hanga la Wete yasiyokuwa na vielelezo shilingi 350,000,000**

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimefanya ujenzi wa hanga la kulalia wapiganaji lililopo Wete, ambapo fedha za ujenzi huo zimeingizwa katika Hesabu ya Kamanda ya KMKM Zanzibar kutoka (OR) Fedha na Mipango Zanzibar.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 70,000,000 zilihaulishwa kutoka Hesabu ya Kamanda ya KMKM Zanzibar kwenda Hesabu ya Kamanda ya KMKM Pemba na kutumika kwa ajili ya ujenzi wa hatua ya msingi, uwekaji wa jamvi pamoja na kunyanyua matufali hadi kufikia hatua ya uwezekaji (gebo) na jumla ya shilingi 280,000,000 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya uwezekaji, upigaji wa palasta na vifaa vya umaliziaji wa jengo (finishing).

Aidha imebainika kuwepo kwa hati nambari D04PV2000000317 ya tarehe 29/04/2021 yenye jumla ya shilingi 350,000,000 inayohusu malipo kwa ajili ya ujenzi wa hanga ya kulalia wapiganaji wa Kikosi cha KMKM Wete Pemba ambapo vielelezo vyote vinavyohusika na malipo hayo vimekosekana kwa ukaguzi.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea thamani ya ujenzi huo pamoja uhalali wa malipo yaliyofanyika kutokupatikana ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Hali halisi ya hanga hilo ni kama inavyoonekana katika picha iliyopo hapo chini:-




*Ujenzi wa hanga la kulalia wapiganaji wa KMKM Wete*

#### 4.4.3.2 Malipo ya ujenzi wa mahanga yasiyokuwa na vielelezo

Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo kimefanya ujenzi wa mahanga ya kulalia wapiganaji wake katika eneo la Kiuyu Mbuyuni kupitia hatua tano tofauti ambazo ni, hatua ya kwanza na ya pili inahusu kuanza kwa matayarisho ya ujenzi, ujenzi wa foundation hadi hatua ya gebo ambapo kumbu kumbu za kifedha pamoja vielelezo vya ujenzi vinavyohusiana na hatua hizo havikupatikana kwa ukaguzi, hali iliyopelekea kutokujuwa fedha halisi iliyotumika ili kuweza kupima thamani halisi ya ujenzi kulingana na hatua hizo, na hatua ya tatu hadi ya tano zinahusu uwezekaji, utiaji wa milango na madirisha pamoja na umaliziaji na mapambo, ambazo vifaa vya ujenzi vilivyotumika vimenunuliwa kupitia zabuni iliyokabidhiwa Kampuni ya Mzalendo Hardware General Supplier na ujenzi husika kufanywa na KMKM kupitia wapiganaji wake.

Katika ukaguzi uliofanyika unaohusiana na ujenzi kuanzia hatua ya tatu hadi hatua ya tano imebainika kuwepo kwa jumla ya shilingi 339,805,555 zilizolipwa kupitia hati nambari D04PV2000000074 ya tarehe 08/09/2020 aliyolipwa Mzalendo Hardware General Supplier kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi ambapo vielelezo vilivyoambatanishwa na hati hiyo ambavyo ni stakabadhi ya malipo nambari 005 pamoja na ankara ya malipo nambari 002 vinaonesha kulipwa jumla ya shilingi 350,459,000 fedha ambayo ni kinyume na hati husika ya malipo, hali inayopelekea kutokujuwa fedha halisi iliyolipwa pamoja na uhalali wa malipo yaliyofanywa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivyo ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa vifaa vilivyonunuliwa ni kama inavyoonekana katika ankara za malipo hapo chini:-



MZALENDO HARDWARE GENERAL SUPPLIER
Tel: +255 777 860 230
BUBUBU - ZANZIBAR
TIN No: 142 - 416 - 220


Date 08/09/2020 INVOICE No: 0002

To: KMKM

| Qty | Particulars | @ | Amount |
|---|---|---|---|
| Pc 958 | 100mm high granite floor tiles skirting wall | 9000 | 8,577,000 |
| [illegible] | Plastic ware Weather Guard Paint | 250,000 | 27,500,000 |
| Roll 63 | 2.5mm2 wire for electrical installation | 90,000 | 5,670,000 |
| Pc 95 | Panasonic fans | 150,000 | 12,850,000 |
| Pcs 290 | Metal boxes | 2000 | 580,000 |
| Pcs 290 | Switch sockets | 12,000 | 3,480,000 |
| Pc 180 | Ceiling lamps | 35,000 | 6,300,000 |
| Pcs 631 | Conduits | 1,000 | 631,000 |
| Pcs 3500 | Concrete block | 2500 | 8,750,000 |
| Trips 3 | Course Aggregates | 500,000 | 1,500,000 |
| | | | 350,459,000 |
| | | Total | 350,459,000/= |

Amount in Word: MILIONI MIA TATU NA HAMSINI LAKI NNE NA HAMSINI NA TISA ELFU TU

Signature



RECEIPT
[MZ]ALENDO HARDWARE GENERAL SUPPLIER
+255 777 860 230
BUBUBU - ZANZIBAR
TIN No: 142 - 416 - 220

9/09/2020 No: 0005

Received from m/s: KMKM

The sum of: MILIONI MIA TATU HAMSINI LAKI NNE HAMSINI NA TISA ELFU TU!

Being payment for: VIFAA VYA UJENZI

Cheque No: TT

USD: 350,459,000/=

MZALENDO HARDWARE GENERAL SUPPLIER · TIN 142-416-220 · TEL 0777 860230 · ZANZIBAR

Signature

*Ankara ya malipo ya ujenzi wa hanga* *Stakabadhi ya malipo ya ujenzi wa hanga*

### 4.4.3.3 Kutokutayarisha na kuwasilisha taarifa za hesabu za miradi

Kwa mujibu wa kifungu Nambari 119(1) cha sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa fedha za Umma ya mwaka 2016 inawataka wakuu wa taasisi kutayarisha taarifa za mapato na matumizi na kuziwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kukamilika kwa matumizi.

Ukaguzi umebaini Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimetekeleza Miradi wa ujenzi wa Mahanga ya kulalia wapiganaji wake katika eneo la Wete na Kiuyu Mbuyuni ambapo kwa mujibu wa taratibu za kisheria Kikosi hicho kinatakiwa kutayarisha na Kuwasilisha Taarifa za matumizi zinazohusiana na utekelezaji wa mradi huo kwa lengo la kukaguliwa na kutolewa ushauri wa kitaalamu.

Hadi ukaguzi unakamilika taarifa hizo hazikuwasilishwa jambo ambalo limenyima fursa ya kuweza kufahamu fedha halisi iliyopatikana na kutumika katika shughuli za uendeshaji na utekelezaji wa mradi huo.

#### 4.4.3.4 Ununuzi wa vifaa vya ujenzi ambavyo havikuonekana kwa ukaguzi shilingi 143,915,000

Kwa mujibu wa mkataba wa makubaliano wenye kumbu kumbu namba KM/HQ/01J/06/2020 uliosainiwa baina ya Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo (KMKM) na kampuni ya Mzalendo Hardware General Supplies ya Bububu Zanzibar kwa thamani ya shilingi 350,459,000 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa Mahanga ya kulalia wapiganaji wa kikosi hicho.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa vifaa vya ujenzi vilivyonunuliwa kupitia Ankara ya Malipo (Invoice) iliobainika wakati wa ukaguzi yenye thamani ya shilingi 350,459,000 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali kwa matumizi ya ujenzi huo.

Hadi ukaguzi unakamilika vifaa vyenye thamani ya shilingi 143,915,000 havikuweza kuonekana kupokelewa pamoja na kutumika kama ilivyokusudiwa katika utekelezaji wa ujenzi huo jambo ambalo linapelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma pamoja na ukiukwaji wa misingi ya kisheria. Mchanganuo wa vifaa hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli la hapo chini:-

## Jadweli Nambari 18 : Ununuzi wa vifaa vya Ujenzi

| Namba | Aina ya Kifaa | Idadi ya vifaa vilivyonunuliwa kupitia Ankara | Idadi ya vifaa vilivyotumika | Idadi ya vifaa ambavyo havikuonekana | Kiasi cha fedha kilicholipwa (shs) | Thamani ya vifaa ambavyo havikuonekana (shs) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Shata za milango ya mbao | 46pcs | 10pcs | 36pcs | 500,000 | 18,000,000 |
| 2. | | 12pcs | - | 12pcs | 450,000 | 5,400,000 |
| 3. | Frem za milango za mbao | 60pcs | 17pcs | 43pcs | 285,000 | 12,255,000 |
| 4. | Feni za Panasonic | 95pcs | - | 95pcs | 130,000 | 12,350,000 |
| 5. | Taa za umeme (Ceiling lamps) | 180pcs | - | 180pcs | 35,000 | 6,300,000 |
| 6. | Tiles (600x600) mm | 891boxes | 400bxs | 441bxs | 40,000 | 17,640,000 |
| 7. | 100mm high granite floor tiles skirting wall | 953pcs | 800pcs | 153pcs | 9,000 | 1,377,000 |
| 8. | Concrete block | 3,500pcs | - | 3,500pcs | 2,500 | 8,750,000 |
| 9. | Switch Sockets | 290pcs | 118pcs | 172pcs | 12,000 | 2,064,000 |
| 10. | 1,200mm x 2,400mm Gypsum Boards | 600pcs | 350pcs | 250pcs | 22,500 | 5,625,000 |
| 11. | Decorative cornices 2.5m long. | 1,171pcs | 320pcs | 851pcs | 4,000 | 3,404,000 |
| 12. | Saruji | 2,550bags | 1,000bags | 1,550bags | 15,000 | 23,250,000 |
| 13. | Wash ware Weather Guard Pains | 110Bucket | 50bucket | 60bucket | 250,000 | 15,000,000 |
| 14. | 10 lorry sand trips | 55trips | 30trips | 25trips | 500,000 | 12,500,000 |
| **Jumla** | | | | | | **143,915,000** |

#### 4.4.3.5 Malipo ya fedha yaliyokosekana kujulikana matumizi yake shilingi 10,653,445

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kupitia hati ya malipo kuwa jumla ya shilingi 339,805,555 zimelipwa kwa Kampuni ya Mzalendo Hardware General Supplier kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya Ujenzi wa Mahanga ya kulalia Wapiganaji wa Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo (KMKM), ambapo ukaguzi umebaini kupitia barua ya maombi ya malipo, Ankara ya malipo (Invoice) nambaro 002 na stakabadhi za malipo nambari 005 kuwa jumla ya malipo aliyolipwa mfanyabiashara huyo shilingi 350,459,000 na kupelekea kuwepo utofauti wa shilingi 10,653,445 ambazo hazikuweza kufahamika matumizi yake pamoja na kukosekana vielelezo halisi vinavyothibitisha uwepo wa matumizi ya fedha hizo jambo ambalo tumeshindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa matumizi hayo.

Kufanya hivyo kunaweza kukapelekea kujitokeza upotevu wa fedha za umma pamoja na kwenda kinyume na kifungu nambari 34(2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Hali halisi ya muonekano wa utekelezaji wa mradi huo ni kama inavyobainika hapo chini:-

**Picha ya mradi wa Ujenzi wa Mahanga ya Kulalia Wapiganaji wa Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo Pemba.**



*Hanga nambari 2*



*Hanga nambari 1*



*Hospital*



*Jiko*



*Msikiti*



*Mesi*



*Quarter gurd*



*Nyumba ya Mkuu wa Kambi*

## SURA YA TANO

# 5.0 MIRADI ILIYOTEKELEZWA KATIKA SEKTA YA UCHUMI WA BULUU, KILIMO NA MAMBO YA KALE

## 5.1 MRADI WA MAMLAKA YA UVUVI WA BAHARI KUU ZANZIBAR (SWIOFish1 - GEF GRANT)

Mradi wa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Zanzibar (South West Indian Ocean Fisheries - SWIOFish1 : GEF Grant) ni programu ya awamu 3 ya miaka 15 ambayo inasaidia ushirikiano wa kikanda wa usimamizi wa uvuvi. Mkataba wa ufadhili wa mradi ni kati ya Benki ya Maendeleo ya Kimataifa (Benki ya Dunia) na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ulitiwa saini tarehe 12 Machi 2015 na kutangazwa rasmi kuanza kutumika tarehe 22 Juni 2015. Mradi huu ulitarajiwa kumalizika tarehe 30 Septemba, 2021 lakini muda wa Mradi uliongezwa hadi tarehe 30 Septemba, 2022. Kiasi cha fedha kilichopangwa kutumika katika utekalezaji wa mradi kwa kipindi hiki ni jumla ya dola za Kimarekani 1,977,000.5

Katika mradi huu wanufaika wakubwa ni pamoja na jumuiya za wavuvi ufugaji wa mwambao ambapo ni wavuvi wa kujikimu, kaya ambazo uvuvi ni sehemu muhimu ya maisha ya vijijini, wavuvi wadogo wadogo pamoja na wakulima wa mwani.

Mambo muhimu ya kuzingatia katika utekelezaji wa mradi huu ni kama ifuatavyo:-

**Ushirikiano wa Kikanda ulioimarishwa**

Kipengele hiki kinasaidia utoaji wa manufaa ya kikanda kwa umma kupitia uratibu na ushirikiano wa kikanda katika usimamizi na maendeleo endelevu ya uvuvi katika nchi za SWIO, zinazo fadhiliwa na mradi

**Kipaumbele cha uboreshaji wa uvuvi**

Kipengele hiki kinalenga sera, mikakati, taasisi na mifumo ya kisheria ya sekta ya umma inayohitajika ili kuboresha usimamizi na utendaji wa uvuvi kipaumbele, pamoja na afya ya mazingira ya bahari ya kikanda na kustahamili mabadiliko ya hali ya hewa. Shughuli zake zinalenga kuelewa msingi wa rasilimali, na kujenga uwezo wa kibinadamu na wa kitaasisi unaohitajika kutekeleza sera za uvuvi na mipango ya usimamizi juu ya samaki aina ya jodari.

**Kuongezeka kwa Manufaa ya Kiuchumi kutoka kwa Uvuvi wa Kipaumbele**

Kipengele hiki kinalenga kuwezesha sekta binafsi nchini kuwekeza na kuzalisha, na uwekezaji wa umma ambao ni muhimu kwa sekta ya kibinafsi. Kipengele hiki kitaboresha mazingira ya biashara ya kitaifa, kusaidia sekta binafsi inayowajibika na kuandaa upembuzi yakinifu na miundo ya uwekezaji kwa ajili ya uwekezaji unaowezekana siku zijazo.

### 5.1.1 USIMAMIZI NA URATIBU WA MRADI

Kipengele hiki kinasaidia uratibu na utekelezaji wa Mradi wa kikanda, utekelezaji na usimamizi wa ngazi ya taifa, na ufuatiliaji na tathmini katika ngazi ya kikanda na taifa. Inafanya kazi kupitia Kamati za Uendeshaji za Mikoa na Kitaifa 'Regional and National Steering Committees' na Vitengo vya Utekelezaji vya Mikoa 'Regional and Project Implementation Units' katika ngazi ya mkoa na taifa.

### 5.1.2 LENGO LA MRADI

Mradi wa SWIOFish umepangwa kutekelezwa kwa lengo la kuongeza faida endelevu za kiuchumi zinazotokana na uvuvi wa baharini katika bahari ya hindi Kusini Magharibi 'South West Indian Ocean' (SWIO) ambapo madhumuni ya Maendeleo ya Mradi na Malengo ya Kimazingira Duniani kwa Awamu ya 1 ni kuboresha ufanisi wa usimamizi wa uvuvi uliopewa kipaumbele katika ngazi ya kikanda, kitaifa na jamii, na inalenga zaidi kuboresha utawala wa uvuvi.

### 5.1.3 UFADHILI WA MRADI

Mradi huu unafadhiliwa kwa asilimia 100 na Benki ya Dunia kwa nambari GEF GRANT 019021 ambapo fedha zake hupokelewa moja kwa moja kutoka Benki ya Dunia kupitia akaunti yake maalum iliyofunguliwa katika Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ Ltd).

Katika mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya Dola za Kimarekani 902,279.86 ziliombwa kupitia mradi huo. Mchanganuo wa maombi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 19 :Fedha zilizoombwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi**

| Tarehe ya maombi | Nambari ya maombi | Aina ya Maombi | Kiwango cha Dola ya Marekani kilichoingizwa (USD) |
|---|---|---|---|
| 03-Aug-2020 | DSFA/GEF/26 | Reimbursement – SOE | 70,018.14 |
| 24-Aug-2020 | DSFA/GEF/27 | Reimbursement – SOE | 154,071.38 |
| 09-Oct-2020 | DSFA/GEF/28 | Reimbursement – SOE | 162,903.19 |
| 25-Nov-2020 | DSFA/GEF/29 | Reimbursement – SOE | 106,187.80 |
| 17-Dec-2020 | DSFA/GEF/30 | Reimbursement – SOE | 162,454.52 |
| 14-May-2021 | DSFA/GEF/31 | Reimbursement – SOE | 182,750.14 |
| 14-May-2021 | DSFA/GEF/32 | Reimbursement – SOE | 33,778.61 |
| 14-May-2021 | DSFA/GEF/33 | Reimbursement – SOE | 30,116.08 |
| 18-Jun-2021 | DSFA/GEF/34 | Reimbursement – SOE | - |
| **Jumla** | | | **902,279.86** |

## MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI

### 5.1.3.1 Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 1,189,815,582

Kwa mujibu wa kifungu cha 23 (1) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Umma nambari 11 ya 2016 mtu, kampuni au taasisi haitashiriki katika manunuzi ya umma isipokuwa mtu huyo, kampuni au taasisi imesajiliwa kama msambazaji chini ya Sheria, vinginevyo kampuni hiyo imekataliwa na haitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Mradi ulifanya manunuzi kwa watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA).

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na kifungu cha 23 (1) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa unasimamia ipaswavyo manunuzi yanafanywa chini ya utekelezaji wa miradi kwa mujibu wa Sheria, kanuni na miongozo iliyopo ili kuepusha upatikanaji wa watoa huduma ambao hawafai katika usambazaji wa bidhaa na utoaji wa huduma zinazotakikana katika miradi ya Serikali.

Mchanganuo wa watoa huduma hao ni kama inavyonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 20 : Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa**

| Na | Jina la Mtoa Huduma | Huduma Inayotolewa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | RASHID M. SHARIF | Malipo yaliyofanywa kuhusiana na usaidizi wa mfumo kwa mfumo wa taarifa za uvuvi | 13,923,833 |
| 2. | Institute of Marine Sciences | Malipo kuhusiana na huduma za ushauri kuhusu kipengele cha Oceanographic kinachoathiri samaki aina ya Jodari | 220,356,794 |
| 3. | Dar es salaam Merchant Group ltd | Malipo ya huduma za Ushauri kuchukua wasifu wa Kiuchumi wa Jodari kama rasilimali za Uvuvi | 117,387,738 |
| 4. | FT Technology (T) Limited | Malipo yaliyofanywa kuhusiana na matengenezo na usakinishaji wa programu ya leseni | 3,990,000 |
| 5. | Tanzania Fisheries Research Institute | Malipo yanayotolewa kwa asilimia 20 ya huduma za ushauri kwa ajili ya utafiti wa Biolojia na Ikolojia | 295,771,374 |
| 6. | TanWings Aviation (T) Ltd | Malipo kwa ajili ya kuwezesha ujumbe wa Doria ya Anga katika Ukanda wa Pekee wa Kiuchumi wa Tanzania | 352,887,976 |
| 7. | Mzumbe University | Malipo ya Kuwezesha awamu ya kwanza ya ailimia 20 ya huduma za ushauri kwa ajili ya Maendeleo ya Mpango wa Biashara wa Mamlaka ya bahari kuu. | 185,497,866.67 |
| **Jumla** | | | **1,189,815,582** |

#### 5.1.3.2 Mafanikio mabaya ya matokeo ya haraka ya mradi

Kwa mujibu wa matokeo ya mradi (Project Result's Matrix), ifikapo mwaka wa 6 wa kipindi cha mradi (yaani mwaka wa fedha 2020/2021) mradi ulitarajiwa kuwa umepata matokeo kadhaa ya haraka yenye lengo la kuwa na matokeo chanya katika uvuvi wa kipaumbele uliochaguliwa.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa matokeo ya mradi yalioainishwa kwa mwaka wa 2020/2021 kama ilivyopatikana kutoka kitengo cha usimamizi na ufatiliaji kuwepo kwa mapungufu kati ya matokeo yanayotarajiwa ya mradi na matokeo halisi ya mradi ambapo inaonesha takwimu halisi ya utekelezaji wa malengo ya mradi ya kipindi cha miaka sita ambayo siyakuridhisha, hali hiyo inaweza kuathiri utimilifu wa manufaa yanayotarajiwa katika uvuvi wa kipaumbele uliochaguliwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kwamba utekelezaji wa shughuli zilizopangwa katika miradi zinatekelezwa kwa mujibu wa mipango iliyopo ili kuweza kupata matokeo mazuri ya mradi kwa maslahi ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mchanganuo wa mafanikio ya matokeo ya haraka ya mradi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 21 : Mafanikio mabaya ya matokeo ya haraka ya mradi**

| Na | Viashiria | Malengo yaliyopangwa kwa kipindi cha miaka sita (6) | Utekelezaji halisi wa malengo kwa kipindi cha miaka sita (6) |
|---|---|---|---|
| 1. | Idadi ya wanufaika wa moja kwa moja wa mradi ambao asilimia kubwa ni wanawake | 65,000 | 1,000 |
| 2. | Hatua za usimamizi bora za uvuvi zilizochukuliwa kama matokeo ya usaidizi wa mradi | 5 | 2 |
| 3. | Usimamizi wa ujuzi wa uvuvi wa uendeshaji | 12 | 3 |

## 5.2 MRADI WA MAMLAKA YA UVUVI WA BAHARI KUU ZANZIBAR (SWIOFish1 – IDA)

Mradi wa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Zanzibar (South West Indian Ocean Fisheries - SWIOFish1 : IDA) ni programu yenye awamu 3 ya miaka 15 ambayo inasaidia ushirikiano wa kikanda wa usimamizi wa uvuvi ambao Tanzania iko katika kundi la kwanza la Nchi kupokea fedha. Mkataba wa ufadhili wa mradi kati ya Benki ya Maendeleo ya Kimataifa (Benki ya Dunia) na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulitiwa saini tarehe 12 Machi 2015 na kuanza kutumika tarehe 22 Juni 2015 ambapo muda wa kukamilisha utekelezaji mradi ni 30 Septemba, 2022.

### 5.2.1 LENGO LA MRADI

Lengo kuu la mradi ni 'kuongeza faida endelevu za kiuchumi zinazotokana na uvuvi wa baharini, na uwiano wa manufaa hayo yanayobaki ndani ya eneo.' Madhumuni ya Maendeleo ya Mradi kwa Awamu ya 1 ni 'kuboresha ufanisi wa usimamizi wa kuchaguliwa kwa kipaumbele cha uvuvi katika ngazi ya kikanda, kitaifa na jamii' na inalenga zaidi kuboresha utawala wa uvuvi. Maendeleo na malengo ya kimataifa ya Mradi ni kuboresha ufanisi wa usimamizi wa uvuvi uliopewa kipaumbele katika ngazi ya kikanda, kitaifa na jamii.Walengwa wakuu ni wavuvi wa kujikimu, kaya ambazo uvuvi ni sehemu muhimu ya maisha ya vijijini, wavuvi wadogo na wakulima wa mwani.

### 5.2.2 VIPENGELE VYA MRADI

Mradi wa SWIOFish1 una vipengele vinne vya utekelezaji kama ifuatavyo:-

**Kipengele cha 1: Ushirikiano wa Kikanda ulioimarishwa**

Kipengele hiki kinasaidia utoaji wa manufaa ya kikanda kwa umma kupitia uratibu na ushirikiano wa kikanda katika usimamizi na maendeleo endelevu ya uvuvi katika nchi za SWIO.

**Kipengele cha 2: Utawala Bora wa Uvuvi wa Kipaumbele**

Kipengele hiki kinalenga sera, mikakati, taasisi na mifumo ya kisheria ya sekta ya umma inayohitajika ili kuboresha usimamizi na utendaji wa uvuvi wa kipaumbele, pamoja na mazingira ya bahari ya kikanda na kustahimili mabadiliko ya hali ya hewa.

Shughuli zake zinalenga kuelewa msingi wa rasilimali, na kujenga uwezo wa kibinadamu na wa kitaasisi unaohitajika kutekeleza sera za uvuvi na mipango ya usimamizi juu ya samaki aina ya jodari.

**Kipengele cha 3: Kuongezeka kwa Manufaa ya Kiuchumi kutoka kwa Uvuvi wa Kipaumbele**

Kipengele hiki kinalenga kuwezesha tija na uwekezaji wa sekta binafsi nchini, na uwekezaji wa umma ambao ni muhimu kwa sekta ya kibinafsi yenye uwezo. Kipengele hiki kitaboresha mazingira ya biashara ya kitaifa, kusaidia sekta binafsi inayowajibika na kuandaa upembuzi yakinifu na miundo ya uwekezaji wa miundo msingi kwa ajili ya uwekezaji unaowezekana siku zijazo.

**Kipengele cha 4: Usimamizi na Uratibu wa Mradi**

Kipengele hiki kinasaidia uratibu na utekelezaji wa Mradi wa kikanda, utekelezaji na usimamizi wa ngazi ya nchi, na ufuatiliaji na tathmini katika ngazi ya kikanda na nchi. Inafanya kazi kupitia Kamati za Uendeshaji za Mikoa na Kitaifa 'Regional and National Steering Committees' (RSC/PIUs) na Vitengo vya Utekelezaji vya Mikoa na Miradi 'Regional and Project Implementation Units' (RMU/PIUs) katika ngazi ya mkoa na nchi.

### 5.2.3 TAARIFA YA FEDHA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MRADI

**Taarifa ya Mapato na Matumzi**

Mradi wa SWIOFish unafadhiliwa kwa njia ya mkopo na Benki ya Dunia kwa asilimia 100 ambapo katika mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya Dola za Kimarekani 322,430.38 ziliingizwa kwa ajili ya utekelezaji mradi huo. Mchanganuo wa maombi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 22 : Fedha zilizoombwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi**

| Tarehe ya maombi | Namba ya Maombi | Aina ya maombi | Kiasi cha dola za kimarekani Zilizoombwa (USD) |
|---|---|---|---|
| 22-Jan-2021 | DSFA/IDA/16 | Reimbursement – SOE | 115,550.37 |
| 10-Mar-2021 | DSFA/IDA/17 | Reimbursement – SOE | 206,880.01 |
| **Jumla** | | | **322,430.38** |

## MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI

### 5.2.3.1 Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na mamlaka ya ununuzi na uondoaji wa mali za umma shilingi 235,846,775 na USD 6,000

Kwa mujibu wa kifungu cha 23 (1) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Umma Na. 11 ya 2016, mtu, kampuni au taasisi haitashiriki katika manunuzi ya umma isipokuwa mtu huyo, kampuni au taasisi imesajiliwa kama msambazaji chini ya Sheria, vinginevyo kampuni hiyo imekataliwa na haitazingatiwa na taasisi ya ununuzi. Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Mradi ulifanya manunuzi kwa kutumia watoa huduma mbali mbali ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA) hali inayopelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi pamoja na gharama za usajili.

Ukaguzi unashauri uongozi wa mradi uhakikishe kuwa manunuzi yote yanafanyika kwa wazabuni waliosajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa mali za Umma ili kuepusha kufanya biashara na watoa huduma ambao hawaisaidii serikali katika upatikanaji wa mapato. Mchanganuo wa malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa ni kama inavyonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 23 : Malipo kwa Wafanya watoa huduma ambao hawakusajiliwa**

| Na | Jina la mtoa huduma | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs/USD) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1. | Ena's Lik Decoration | Shilingi 2,500,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya kuwezesha gharama za kukodisha |
| 2. | Terabyte Solutions Co.Ltd | Shilingi 7,369,600 | Malipo ya fedha kwa ajili ya vifaa vya uhamasishaji |
| 3. | Zeccon Company Limited | Shilingi 208,750,942 | Malipo ya fedha kwa ajili ujenzi wa Slipway kwa |
| 4. | Mohammed Kombo Maalim | Shilingi 12,860,625 | Malipo ya huduma za ushauri katika Mtaalamu wa Ulinzi wa Mazingira |
| 5. | Salvatory Faustine Lyakurwa | Shilingi 4,365,608 | Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma za ushauri |
| 6. | Zanzibar Telecom plc | Dola za Kimarekani 6,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma za mtandao |

#### 5.2.3.2 Kutokutekelezwa kwa baadhi ya shughuli za mradi USD 20,217

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya dola za Kimarekani 20,217 ni fedha ambazo zingepaswa kutumika kwa ajili ya utekelzaji wa shughuli mbali mbali za mradi lakini hadi ukaguzi unakamilika baadhi ya shughuli hizo hazikuweza kutekelezwa hali inayoweza kupelekea uwezekano wa kuongezeka kwa gharama zinazotokana na ongezeko la bei za vitu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mradi wa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Zanzibar uhakikishe shughuli za mradi zilizopangwa na zinafanyika kwa wakati kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa ili kufikia lengo la mradi lililokusudiwa.

Mchanganuo wa baadhi ya Shughuli za mradi ambazo hazikutekelezwa ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 24 : Kutokutekelezwa kwa baadhi ya shughuli za mradi**

| Namba ya shughuli ya mradi | Shughuli ya mradi | Kiasi cha fedha zilizotengwa (USD) |
|---|---|---|
| 4.2.3.7 | Tathmini ya mwisho (Bara, Zanzibar, Mamlaka ya bahari kuu) | 15,000 |
| 4.2.3.8 | Warsha za mashauriano | 5,217.39 |
| **Jumla** | | **20,217** |

## 5.3 MRADI WA UZALISHAJI WA MPUNGA (ERPP)

Wizara ya Kilimo Hifadhi ya Chakula na Ushirika ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano ya Tanzania pamoja na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Zanzibar wanatekeleza Mradi wa Kuendeleza Uzalishaji wa Mpunga (ERPP) kwa ufadhili wa Mpango wa Kilimo na Usalama wa Chakula Duniani (GAFSP). Lengo la mradi huu ni kuongeza tija katika uzalishaji wa mpunga katika maeneo yaliyolengwa.

### 5.3.1 WANUFAIKA WA MRADI

Walengwa wa mradi huu ni kaya za wakulima wadogo wadogo wapatao 33,069 ambapo mradi ulichagua Tanzania Bara ( Kaya 24,372) na Zanzibar (Kaya 8,697). Kulingana na sensa ya watu na makaazi ya mwaka 2012

### 5.3.2 VIPENGELE VYA MRADI

Mradi wa Uzalishaji wa Mpunga una vipengele vitatu (3) kama ifuatavyo:-

**Kipengele cha 1:** Mifumo endelevu ya Mbegu (Dola za Marekani milioni 1.11).

Sehemu hii itazingatia vipengele vidogo vitatu kama ifuatavyo:-

- Maandamano ya shambani.
- Kukuza uzalishaji endelevu na Utoaji wa aina zinazopendekezwa.
- Kuimarisha udhibiti wa ubora wa mbegu.

**Kipengele cha 2:** Kuboresha uzalishaji wa mazao kwa umwagiliaji bora na usimamizi wa mazao (Dola za Marekani milioni 3.7).

Kipengele hiki kitazingatia vipengele vidogo vifuatavyo:-

- Upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji.
- Kukuza matumizi ya mbinu bora za kilimo.

**Kipengele cha 3**: Usimamizi na Uratibu wa Mradi : (Dola za Marekani milioni 1.6)

### 5.3.3 TAARIFA YA FEDHA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MRADI

**Taarifa ya Mapato na Matumzi**

Mradi wa Uzalishaji wa Mpunga kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulikadiriwa kutumia jumla ya dola za Kimarekani 722,963.02 zilizofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB). Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya dola za Kimarekani 704,574.35 zilitumika sawa na asilimia 97 ya makadirio. Mchanganuo wa upatikanaji na utumiaji wa fedha za mradi huo ni kama inavyonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 25 : Taarifa ya fedha za mradi**

| Maelezo | Kiasi cha fedha kilichotumika (USD) | Kiasi cha fedha kilichotumika (Tshs) |
|---|---|---|
| Salio anzia 1 Julai,2020 | 506,523.01 | 741,048,229.24 |
| **Fedha zilizopokelewa:** | | |
| Benki ya Dunia (WB) | 216,439.92 | 498,244,695.84 |
| Mchango wa serikali | - | 403,013,168.66 |
| Jumla ya fedha iliyopokelewa | 216,439.92 | 901257864.5 |
| **Jumla ya fedha iliyopatikana** | **722,963.02** | 1,642,306,093.74 |
| Matumizi kwa 2020/2021 | 704,574.35 | 1,629,673,093.74 |
| Salio la mwisho 30Juni,2021 | 18,388.67 | 12,633,000 |

## MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI

### 5.3.3.1 Utekelezaji wa Mradi kinyume na Bajeti

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mradi wa ERPP uliingiziwa jumla ya dola za Kimarekani 722,963.02 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zilizopangwa, lakini dosri ilyobainika na ukaguzi ni kufanyika kwa matumizi ya fedha za mradi huo kinyume na bajeti.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuathirika kwa baadhi ya shughuli za utekelezaji wa mradi ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mradi wa ERPP kuhakikisha kwamba kazi za utekelezaji wa mradi zinafanyika kwa mujibu wa bajeti iliyopangwa ili kuepusha uwezekano wa kufanyika kwa matumizi yasiyolingana na mipango ya awali. Mchanganuo wa matumizi ya fedha za mradi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 26 : Utekelezaji wa Mradi kinyume na Bajeti**

| Na | Maelezo | Kiasi cha fedha kilichoidhinishwa (USD) | Kiasi cha fedha kilichotumika (USD) | Tofauti ya matumizi (USD) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji | 150,000 | 277,625.75 | (127,625) | 85 |
| 2. | Mafunzo ya ndani ya nchi kwa wafanyakazi | 10,000 | 2,454 | 7,546 | 75 |
| 3. | Mafunzo ya nje ya nchi kwa wafanyakazi | 15,000 | 21,822.94 | (6,822) | 45 |
| 4. | Kufanya mikutano ya uongozi | 3,000 | | 3,000 | 100 |

## 5.4 MRADI WA UHIFADHI WA ENEO LA KIHISTORIA LA MKAMANDUME PEMBA

Mradi wa ujenzi wa maeneo ya kihistoria Mkamandume umetekelezwa kwa ufadhili wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asilimia 100. Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale – Zanzibar iliingia mkataba na kampuni ya Shamjo Company Limited kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha utoaji wa huduma pamoja na ukarabati wa maeneo ya kihistoria ya Mkamandume kwa kiasi cha shilingi 1,407,718,711 ambapo mkataba wa awali wenye kumbukumbu namba SMZ/JOI/W/RS/18/2018-2019 uliosainiwa tarehe 26/2/2019 ukiwa na thamani ya shilingi 529,409,124 pamoja na VAT.

Aidha, mkataba wa pili wenye kumbukumbu namba SMZ/JOI/W/RS/21/2019-2020 uliosainiwa tarehe 14/10/2019 ukiwa na thamani ya shilingi 878,309,587 pamoja na VAT ulihusisha utekelezaji wa mradi huu katika vipindi vya awamu mbili tofauti kama ifuatavyo:-

Awamu ya kwanza ilihusisha ujenzi wa nyumba ya utoaji wa huduma katika eneo la kihistoria la Mkamandume (facility building constraction) kwa gharama ya shilingi 367,496,913 pamoja na VAT na awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi huo ilihusisha ukarabati wa eneo halisi la kihistoria la Mkamandume (Rehabilation of Mkamandume historical site) kwa gharama ya shilingi 507,812,674 pamoja na VAT.

### 5.4.1 MALENGO YA UTEKELEZAJI WA MRADI

Mradi wa ujenzi wa maeneo ya kihistoria Mkamandume umetekelezwa ukiwa na malengo mbali mbali yanayohusu uboreshaji wa eneo pamoja na kuongeza vivutio vya watalii wanaokwenda kutembelea katika eneo hilo. Katika utekelezaji wa mradi huo malengo mahsusi ni kama ifuatavyo:-

- Kuifanya Zanzibar inufaike zaidi kiuchumi bila ya kuharibu mila na utamaduni wa asili.
- Kuhakikisha mazingira ya Zanzibar yanabaki salama pamoja na kuimarika kwa huduma za utalii.
- Kuifanya Zanzibar iwe ni mafikio (destination) bora zaidi kwa watalii wa daraja la juu.
- Kusimamia utalii ili kuweza kukukua pamoja na kupanga mipango madhubuti ya kuimarisha huduma za utalii.

### MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI

#### 5.4.1.1 Kukosekana kwa daftari la kuhifadhia kumbukumbu za mali za kudumu

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba inamiliki mali mbali mbali za kudumu yakiwemo maeneo ya kihistoria katika kisiwa cha Pemba lakini daftari la kuhifadhia kumbu kumbu za mali hizo limekosekana kwa ukaguzi hali ambayo inapelekea kushindwa kuthibitisha uwepo na uhifadhi wa maeneo ya kihistoria katika kisiwa cha Pemba.

Kutokuwepo kwa daftari la kuhifandhia kumbukumbu za mali za kudumu ni kwenda kinyume na kifungu namba 29 (2) cha sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unaanzisha na kulitumia daftari la kuhifadhia kumbukumbu za mali za kudumu kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo mbali mbali iliyopo.

#### 5.4.1.2 Kukosekana kwa vielelezo vya ulipwaji wa kodi ya VAT kwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRB) Shilingi 56,058,851.

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba imeingia mkataba na Shamjo Company Ltd kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha utoaji wa huduma katika maeneo ya kihistoria Mkamandume kwa mkataba nambari SMZ/JOI/W/RS/21/2019-2020 wa tarehe 14/10/2019. Kwa mujibu ya makubaliano ya mkataba na Bill of Quantity (BOQ), malipo ya kodi ya 18% VAT kwa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) ni shilingi 56,058,851 kutoka shilingi 311,438,062 za gharama ya ujenzi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebanika kukosekana kwa vielelezo vyenye jumla ya shilingi 56,058,851 ambazo zimelipwa kwa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kwa ajili ya ulipaji wa kodi ya ongezeko la thamani VAT itokanayo na ujenzi wa kituo cha utoaji wa huduma katika eneo la kihistoria Mkamandume. Hali iliyopelekea kufanya maombi ya vielelezo hivyo kwa barua yenye kumbu kumbu namba AUD/PUMK.IV/VOL.2 ya tarehe 16/12/2021 kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Pemba hata hivyo vielelezo husika havikuweza kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuhakikisha kwamba malipo yote yanayofanyika yanaambatanishwa na vielelezo vya malipo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Mchanganuo wa malipo yasiyokuwa na vielelezo ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 27 : Malipo ya kodi ya VAT yasiokuwa na vielelezo**

| Na | Maelezo | Kiasi cha fedha Kilicholipwa (Tshs.) |
|---|---|---|
| 1. | Substructure | 37,309,000.00 |
| 2. | Frames | 18,344,600.00 |
| 3. | Walls and partitions | 26,130,000.00 |
| 4. | Roof | 41,228,000.00 |
| 5. | Doors | 11,100,000.00 |
| 6. | Windows | 10,600,000.00 |
| 7. | Finishes | 27,448,500.00 |

| Na | Maelezo | Kiasi cha fedha Kilicholipwa (Tshs.) |
|---|---|---|
| 8. | Painting and decoration | 8,752,000.00 |
| 9. | Plumbing and drainage installation | 51,130,000.00 |
| 10. | Electrical installation | 23,235,000.00 |
| | **Jumla ndogo (A)** | **255,771,100.00** |
| 11. | Preliminaries (2% of sub total a) | 5,105,542.00 |
| 12. | Allow for 10% of sub total a as consultancy fee | 25,527,710.00 |
| 13. | Allow for provision sums for works unforeseen that could occur during implementation of the construction works (10% of sub total a) | 25,527,710.00 |
| | **Jumla ndogo (B)** | **311,438,062.00** |
| 14. | **Kodi ya asilimia 18 ya jumla ndogo (B)** | **56,058,851.00** |

### 5.4.1.3 Kukosekana kwa Taarifa za Malipo ya Mshauri Elekezi shilingi 25,527,710

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba imeingia mkataba na Shamjo Company Ltd kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha utoaji wa huduma katika eneo la kihistoria la Mkamandume kwa mkataba nambari SMZ/JOI/W/RS/21/2019-2020 wa tarehe 14/10/2019.

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba AUD/PUMK.IV./VOL.2 ya tarehe 16/12/2021 iliyoitaka Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba kuwasilisha taarifa za malipo yote yaliyotumika kwa mradi wa maeneo ya kihistoria Mkamandume katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Pemba kwa ukaguzi lakini taarifa hizo hadi ukaguzi unakamika hazikuweza kuwasilishwa hivyo kutia shaka juu ya malipo ya shilingi 25,527,710 ya mshauri elekezi yaliyofanyika.

Kukosekana kwa taarifa za malipo ya mshauri elekezi kwa ukaguzi ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba kuhakikisha kwamba taarifa zote zinazotokana na malipo yaliyofanyika zinaambatanishwa katika hati za malipo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali

wa malipo hayo.

### 5.4.1.4 Kukosekana kwa Taarifa za Uhifadhi wa fedha za mfuko wa Dharura (Unforeseen Event Fund) shilingi 25,527,710

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba imeingia mkataba na Shamjo Company Ltd kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha utoaji wa huduma katika eneo la kihistoria la Mkamandume kwa mkataba nambari SMZ/JOI/W/RS/21/2019-2020 wa tarehe 14/10/2019.

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba AUD/PUMK.IV./VOL.2 ya tarehe 16/12/2021 iliyoitaka Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale–Pemba kuwasilisha taarifa za malipo yote yaliyotumika kwa mradi wa maeneo ya kihistoria ya Mkamandume katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali–Pemba kwa ukaguzi lakini taarifa hizo hadi ukaguzi unakamika hazikuweza kuwasilishwa hivyo kutia shaka juu ya matumizi ya shilingi 25,527,710 pamoja na utaratibu uliotumika katika uhifadhi na utumiaji wa fedha za Mfuko wa dharura.

Kukosekana kwa taarifa za malipo ya mshauri elekezi kwa ukaguzi ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba kuhakikisha kwamba taarifa zote zinazotokana na malipo yaliyofanyika zinaambatanishwa katika hati za malipo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

### 5.4.1.5 Kutokulingana kwa bei ya ununuzi wa vifaa ukilinganisha na bei halisi ya sokoni shilingi 30,260,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba ilifanya malipo yenye jumla ya shilingi 30,260,000 kwa ajili ya ununuzi ya vifaa mbali mbali vya ujenzi wa kituo cha kutolea huduma kilichojengwa katika eneo la Mkamandume lakini manunuzi ya vifaa hivyo hayakuzingatia thamani halisi kwa wakati huo ambapo imebainika kwamba vifaa hivyo vingeweza kununuliwa kwa jumla ya shilingi 15,160,000 na kupelekea

kupunguwa kwa gharama za jumla kwa thamani ya shilingi 15,100,000 ambazo zingeweza kutumika kwa ajili ya kazi nyengine.

Kufanya hivyo inapelekea uwepo wa matumizi mabaya ya fedha za Serikali yasiyozingatia hali ya uchumi, ufanisi na malengo halisi ya utekelezaji wa mradi ambapo ni kwenda kinyume na kifungu 5(1) cha Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2021.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba ukishirikiana na kamati ya ufundi ya tathmini ya zabuni (technical evaluation committee) kuhakikisha kwamba upembuzi yakinifu unafanyika ili kuweza kupata taarifa sahihi za bei za vifaa vinavyohitajika katika utekelezaji wa mradi kwa lengo la kuepusha manunuzi ya vifaa kwa bei za juu ikilinganishwa na bei halisi zinazopatikana sokoni katika kipindi cha wakati husika. Mchanganuo wa ununuzi wa vifaa hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 28 : Kutokulingana kwa bei ya ununuzi wa vifaa ukilinganisha na bei halisi ya sokoni**

| Na | Aina kifaa | Idadi | Jumla ya fedha zilizolipwa (Tshs.) | Jumla ya fedha kwa bei ya soko (Tshs.) | Tofauti ya Jumla (Tshs.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Main switch | 1 | 480,000 | 100,000 | 380,000 |
| 2. | Mafeni | 6 | 1,080,000 | 660,000 | 420,000 |
| 3. | Simtank (5,000 ltrs) | 2 | 7,000,000 | 2,400,000 | 4,600,000 |
| 4. | Madirisha (1500 x 1700 mm) | 4 | 4,800,000 | 2,400,000 | 2,400,000 |
| 5. | Madirisha (1500 x 700 mm) | 6 | 3,000,000 | 1,800,000 | 1,200,000 |
| 6. | Madirisha (800 x 700 mm) | 8 | 2,800,000 | 1,200,000 | 1,600,000 |
| 7. | Milango (1000 x 2600 mm) | 2 | 1,900,000 | 1,400,000 | 500,000 |
| 8. | Milango (900 x 2600 mm) | 4 | 3,600,000 | 2,000,000 | 1,600,000 |
| 9. | Milango (750 x 2600 mm) | 8 | 5,600,000 | 3,200,000 | 2,400,000 |
| **Jumla** | | | **30,260,000** | **15,160,000** | **15,100,000** |

### 5.4.1.6 Kutokuonekana kwa vifaa vilivyonunuliwa shilingi 15,130,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba mkandarasi wa ujenzi alifanya manunuzi ya vifaa vyenye thamani ya shilingi 15,130,000 ambavyo vilikusudiwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kituo cha

utoaji wa huduma katika eneo la kihistoria la Mkamandume lakini vifaa hivyo havikuonekana kwa ajili ya ukaguzi.

Kufanya hivyo kunapelekea uwezekano wa kuwepo kwa upotevu wa vifaa vilivyonunuliwa hali inayopelekea kuwepo kwa viashiria vya ubadhirifu wa mali pamoja na bidhaa zilizonunuliwa ambapo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba kuhakikisha kwamba vifaa vyote vinavyonunuliwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi vinakuwepo na kutumika kama ilivyoainishwa katika mkataba wa ujenzi kwa lengo la kufanya matumizi ya vifaa yanayoendana na hali ya uchumi, ufanisi na malengo halisi ya utekelezaji wa mradi. Mchanganuo wa vifaa hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 29 : Vifaa vilivyonunuliwa ambavyo havikuonekana**

| Na | Aina kifaa | Idadi ya vifaa vilivyonunuliwa | Idadi ya vifaa vilivyoonekana | Tofauti ya vifaa ambavyo havikuonekana | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Security lights | 10 | 0 | 10 | 430,000 |
| 2. | Milango ya mbao | 14 | 9 | 5 | 5,150,000 |
| 3. | Madirisha | 18 | 11 | 7 | 2,550,000 |
| 4. | Simtank (5,000 ltrs) | 2 | 0 | 2 | 7,000,000 |
| **Jumla** | | | | | **15,130,000** |

### 5.4.1.7 Dosari iliyobainika katika uchimbaji wa msingi wa upitishaji wa maji chumvi pamoja na ujenzi wa ukuta shilingi 350,371,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 350,371,000 zimetumika kwa ajili ya uchimbaji wa msingi wa upitishaji wa maji chumvi pamoja na ujenzi wa kuta pembezoni mwa msingi huo katika eneo la kihistoria la Mkamandume kwa lengo la kuwezesha maji chumvi kuingia na kutoka katika msingi huo ili kuonyesha uhalisia wa kihistoria wa eneo la Mkamandume lakini dosari iliyobainika ni kwamba lengo lililokusudiwa halikufikiwa kutokana na kutokuingia na kutoka kwa maji hayo kama ilivyokuwa katika muonekano wa

asili wa eneo hilo pamoja na makubaliano katika mkataba wa ukarabati wa eneo la kihistoria la Mkamandume.

Katika kufanya ufuatiliaji wa uchimbaji wa msingi wa upitishaji wa maji chumvi pamoja na ujenzi wa kuta pembezoni mwa msingi huo imebainika kwamba gharama zilizotumika ni kubwa na hivyo kutokuendana na thamani halisi ya kazi iliyofanyika kwa kutokuzingatiwa kwa hali ya uchumi, ufanisi wa kazi iliyokusudiwa pamoja na malengo halisi yaliyopangwa katika utekelezaji wa mradi huo.

Kufanya hivyo kunapelekea uwezekano wa kuwepo kwa upotevu wa fedha za Serikali hali inayopelekea kuwepo kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha ambapo ni kwenda kinyume na kifungu 5(1) cha Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2021.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba kuhakikisha kwamba malengo yaliyopangwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi yanasimamiwa na kutekelezwa kama ilivyoainishwa katika mkataba wa ujenzi kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar na Taifa kwa ujumla. Hali halisi ya utekelezaji wa mradi katika eneo lililokusudiwa kuingia na kutoka kwa maji chumvi ni kama inavyoonekana hapo chini:-



*Uchimbaji wa msingi wa upitishaji wa maji chumvi - Mkamandume*

### 5.4.1.8 Dosari iliyobainika katika malipo ya fedha za ukarabati wa kisima cha wivu shilingi 116,661,400

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 116,661,400 zimetumika kwa ajili ya ukarabati wa kisima cha wivu katika eneo la kihistoria la Mkamandume ili kuboresha muonekana mzuri na halisi wa kisima hicho

lakini dosari iliyobainika ni kwamba thamani halisi ya fedha zilizotumika katika ukarabati wa kisima hicho hailingani na hali halisi ya kisima kilichofanyiwa ukarabati.

Katika kufanya ufuatiliaji wa ukarabati huo imebainika kwamba gharama zilizotumika ni kubwa na hivyo kutokuendana na thamani halisi ya ukarabati uliofanyika kwa kutokuzingatiwa kwa hali ya uchumi, ufanisi wa kazi iliyokusudiwa pamoja na malengo halisi yaliyopangwa katika utekelezaji wa mradi huo

Kufanya hivyo kunapelekea uwezekano wa kuwepo kwa upotevu wa fedha za Serikali hali inayopelekea kuwepo kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha ambapo ni kwenda kinyume na kifungu 5(1) cha Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma  ya mwaka 2021.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba kuhakikisha kwamba utekelezaji wa ukarabaiti wa eneo husika unafanyika kulingana na uhalisia kwa mujibu wa mipango na malengo yaliyokusudiwa kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar na Taifa kwa ujumla. Hali halisi ya utekelezaji wa mradi katika eneo lililokusudiwa la ukarabati wa kisima cha wivu ni kama inavyoonekana hapo chini:-



*Ukarabati wa kisima cha wivu - Mkamandume*

### 5.4.1.9 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 80,757,324

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale–Pemba imeingia mkataba na Shamjo

Company Ltd kwa ajili ya uchimbaji wa msingi wa upitishaji wa maji chumvi pamoja na ujenzi wa kuta pembezoni mwa msingi huo katika eneo la kihistoria la Mkamandume kwa mkataba nambari SMZ/JOI/W/RS/18/2018/2019 wa tarehe 26/02/2019.

Katika ukaguzi uliofanyika imebaika kukosekana kwa vielelezo vyenye jumla ya shilingi 80,757,324 ambazo zimelipwa kwa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kwa ajili ya ulipaji wa kodi ya ongezeko la thamani VAT itokanayo na uchimbaji wa msingi pamoja na ukarabati wa ukuta katika eneo la kihistoria Mkamandume. Kutokana na hali hiyo Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Pemba ilifanya juhudi maalumu katika kuhakikisha kwamba vielelezo vyote muhimu vinapatikana kwa kuandika barua rasmi yenye kumbu kumbu namba AUD/PUMK.IV/VOL.2 ya tarehe 16/12/2021 lakini pamoja na juhudi hizo vielelezo husika havikuweza kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuhakikisha kwamba malipo yote yanayofanyika yanaambatanishwa na vielelezo vya malipo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Mchanganuo wa malipo yasiyokuwa na vielelezo ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 30 : Malipo ya kodi ya VAT yasiokuwa na vielelezo**

| Na | Maelezo | Kiasi cha fedha kiliocholipwa (Tshs.) |
|---|---|---|
| 1. | Side walls old fort | 183,950,000 |
| 2. | Jelous well | 20,710,000 |
| 3. | Historical stair case | 8,472,000 |
| 4. | Artificial sea channel | 172,200,000 |
| 5. | Signposts | 4,800,000 |
| | **Jumla ndogo (A)** | **390,132,000** |
| 6. | Allow for proviosonal sums for works unforeseen that coud occure during implementation of the renovation works. | 58,519,800 |
| | **Jumla ndogo (B)** | **448,651,800** |
| 7. | **Kodi ya asilimia 18 ya jumla ndogo (B)** | **80,757,324** |
| | **Jumla Kuu** | **529,409,124.00** |

### 5.4.1.10 Udhibiti na utunzaji wa majengo usioridhisha

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika udhibiti na utunzaji wa majengo yaliyomo katika eneo la kihistoria la Mkamandume hauridhishi ambapo majengo hayo yameonekana kutokuwa katika hali nzuri na baadhi ya majengo hayo kuanguka hali ambayo imepoteza uhalisia na historia ya majengo halisi katika eneo la Mkamandume.


Kutokuyatunza vizuri majengo hayo kunaweza kupelekea kukosekana kwa umadhubuti, kuanguka, kushuka thamani na hatimaye kukosekana kwa tija iliyokusudiwa ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa mapato yatokanayo na uingiaji wa watalii katika maeneo hayo kwa lengo la kuona na kujifunza historia ya Mkamandume.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba kuhakikisha kwamba malengo yaliyopangwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi yanasimamiwa na kutekelezwa kama ilivyoainishwa katika mkataba wa ujenzi kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar na Taifa kwa ujumla.

Aidha, ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba kuhakikisha unayatangaza maeneo ya utalii wa ndani pamoja na utalii wa nje ili kuhakikisha kunapatikanwa kwa mapato ambayo yatasaida kufanya ukarabati wa majengo kwa lengo la kuhakikisha historia ya utalii inabakia katika uhalisia wake kwa maslahi ya vizazi vijavyo.

Hali halisi ya maeneo ya kihistoria yanavyoanguka na kupoteza taswira ya uwepo wake bila ya kufanyiwa ukarabati kwa muda mrefu ni kama inavyoonekana hapo chini:-

*Majengo yaliyoanguka kutokana udhibiti na utunzaji usioridhisha – Mkamandume*

### 5.4.1.11 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 77,462,950

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba imeingia mkataba na Shamjo Company Ltd kwa ajili ya ukarabati wa eneo la kihistoria la Mkamandume kwa mkataba nambari SMZ/JOI/W/RS/21/2019-2020 wa tarehe 14/11/2019.

Katika ukaguzi uliofanyika imebaika kukosekana kwa vielelezo vyenye jumla ya shilingi 77,462,950 ambazo zimelipwa kwa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kwa ajili ya ulipaji wa kodi ya ongezeko la thamani VAT itokanayo na ukarabati wa eneo la kihistoria la Mkamandume. Kutokana na hali hiyo Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Pemba ilifanya juhudi maalumu katika kuhakikisha kwamba vielelezo vyote muhimu vinapatikana kwa kuandika barua rasmi yenye kumbu kumbu namba AUD/PUMK.IV/VOL.2 ya tarehe 16/12/2021 lakini pamoja na juhudi hizo vielelezo husika havikuweza kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuhakikisha kwamba malipo yote yanayofanyika yanaambatanishwa na vielelezo vya malipo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.Mchanganuo wa malipo ya kodi yasiyokuwa na vielelezo ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 31:Malipo ya kodi ya VAT yasiokuwa na vielelezo**

| Na | Maelezo | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) |
|---|---|---|
| | **Jumla ndogo (A)** | **341,547,422** |
| 1. | Preliminaries (3% of sub total) | 10,246,422 |
| 2. | Allow for 8% of sub total 1 as consultancy fee | 27,323,792 |
| 3. | Prime cost and Provisional sums for works unforeseen that could occur during implementation of the renovation works sub total 1. | 51,232,110 |
| | **Jumla ndogo (B)** | **430,349,724** |
| 4. | **Asilimia 18 ya kodi ya VAT ya jumla ndogo (B)** | **77,462,950** |
| | **Jumla kuu** | **507,812,674** |

## 5.5 MRADI WA MATUKIO KATIKA SEHEMU MBALIMBALI ZA UTALII ZANZIBAR

Kutokana na nia ya Serikali ya kuboresha maeneo ya utalii kuwa ni kivutio ambacho kitapelekea kuingizia Serikali pato litokanalo na huduma za utalii zinazoendeshwa sehemu mbalimbali katika kisiwa cha Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi ulifanya ziara ya matembezi katika sehemu mbalimbali zenye vivutio vya utalii ambavyo kwa namna moja au nyengine vimetelekezwa au vimesahauliwa kabisa na havifanyi kazi kwa muda mrefu jambo ambalo kama vitafanyiwa maboresho kuna uwezekano mkubwa wa kupatikana fedha zitokanazo na vianzio hivyo ambazo zitasaidia kuendesha shughuli mbali mbali ndani ya Zanzibar na kupelekea kupatikana kwa tija iliyokusudiwa.

Miongoni mwa maeneo yaliotembelewa na kutolewa ushauri wa maboresho kwa lengo la upatikanaji wa fedha zitokanazo na maeneo hayo ni kama zifuatavyo:-

- Maeneo ya magofu yalioko upande wa Kusini na Kaskazini Unguja.
- Maeneo ya mapango na mahodhi yalioko Maruhubi, hodhi la Hamamni, Gofu la Bihole, Pango la Pete pamoja na mengineyo.

Kutokana na hali hiyo utelekezwaji wa sehemu hizo zilipoteza haiba yake na mandhari ya sehemu hizo zilivyo jambo ambalo limepelekea kwa baadhi ya maeneo kuanza kuvamiwa na wananchi kwa kuanzishwa makaazi ya kudumu na wengineo kufanya shughuli za kijamii ikiwemo kukata mikoko, kuchoma mkaa pamoja na kufanya mambo mengineyo.

Aidha, ukaguzi umebaini baadhi ya maeneo mengine kufanyiwa uharibifu wa makusudi kutokana na ufahamu mdogo walionao baadhi ya wananchi juu ya umuhimu wa uhifadhi wa maeneo ya utalii, ambapo maeneo hayo huingizia Serikali mapato yatokanayo na fedha za kigeni kwa ajili ya uwendeshaji wa shughuli mbalimbali za Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa wizara yenye dhamana kufanya utaratibu wa makusudi wa kuyapitia mara kwa mara majengo na maeneo hayo ili kuwahi kuchukua hatua za mapema kuzifanyia kazi athari zinazoweza kutokea na kuzichukulia hatua kabla majengo hayo hayajaanguka na kupoteza haiba ya muonekano wake jambo ambalo litapelekea kupatikana kwa hasara na kuikosesha mapato Serikali.

Kasoro zifuatazo zimebainika katika ukaguzi huo na hatua za haraka zinahitajika kuchukuliwa ili kurekebisha kasoro hizo zisiendelee kuathiri na badala yake kuendana na malengo ya Serikali yatokanayo na uwepo wa utalii Zanzibar kama chanzo kikuu cha upatikanaji wa fedha. Miongoni mwa dosari na mapendekezo ya utatuzi wa dosari hizo ni kama ifuatavyo:-

## Jadweli Nambari 32 : Dosari zilizobainika katika vyanzo vya mapato ya utalii

| Na | Sehemu zilizotembelewa | Yaliyobainika | Ushauri |
|---|---|---|---|
| 1. | Sultani Berge | Hii ni sehemu iliyohifadhiwa Jahazi la Kifalme hapo Malindi, kwa kipindi hiki Jahazi hili lipo tu limehifadhiwa haliingizi chochote Serikalini.<br><br>Pia kuna baadhi ya vifaa vya jahazi havikuweza kuonekana kama vile Makasia, Nanga na Kamba yake, Tanga na Mlingoti wake, na usukani wa Jahazi hiyo. | a) Vifaa ambavyo havikuonekana vitafutwe na vijulikane wapi vilipo ili kuepuka kusambaratika na kupotea kwa vifaa hivyo, ili uhalisia wa jahazi hilo usije ukapotea<br>b) Wizara ifikirie na ijiandae kwa makusudi mazima kulitafutia eneo muafaka jahazi hili kwa kulitumia liwe makumbusho kwa wageni na wenyeji kwa kiingilio ili liingize mapato serikalini |
| 2. | Hodhi la Hamamni | Eneo liko vizuri linahitaji ukarabati mdogo mdogo tu ili liwe vizuri zaidi.<br><br>Kwa upande wa wafanyakazi tatizo ni lugha wanazotumia ni mbili tu Kiswahili na Kiingereza. | a) Sehemu ambazo zimeanza kuleta athari zishughulikiwe mapema ili zisije zikaleta athari kubwa hapo baadae.<br>b) Kama upo uwezekano wa kusomeshwa kwa lugha nyengine kwa wafanyakazi kutokana na mahitaji wanayoyaona wao wafikiriwe kwa hilo. |

| Na | Sehemu zilizotembelewa | Yaliyobainika | Ushauri |
|---|---|---|---|
| 3. | Gofu la Bi Khole | Eneo lipo vizuri, linavutia na kupendeza.<br><br>Kasoro iliyokuwepo ni kukosekana kwa vyoo vya wafanyakazi na wageni, vyoo vilianzishwa kujengwa lakini hadi leo havijamalizika na hapo palipojengwa tayari pameanza kuharibika.<br><br>Kuna eneo zuri la ufukwe lililokuwepo sehemu ya bahari, eneo hili kwa sasa wageni na wenyeji wameanza kulitumia na kuwa ni sehemu ya mapumziko, lakini kwa Idara ya Makumbusho haiingizi kipato chochote Serikalini ingawa inatumia wafanyakazi wake kwa kulinda magari ya watu wanaoenda kupumzika, na kulisafisha eneo hilo baada ya uchafuzi unaofanywa na wapumzikaji hao, eneo hilo pia lina ukosefu wa maji. | a) Ifanyike juhudi ya makusudi choo kilichoanzwa kujengwa kimalizwe haraka ili kuepusha uharibifu zaidi usiendelee.<br><br>b) Wizara ifanye mazingatio kwa ulinzi wa gari japo kwa kulipia kiwango kidogo pamoja na watu wanaokwenda kupumzika pale kwa ajili ya kuongeza makusanyo yanayopatikana katika eneo hili.<br><br>c) Maji mwazo yalikuwepo kwa hiyo ifanyike jitihada za kuirejesha huduma hiyo kama mwanzo ili wageni wapate kuyatumia kwa matumizi mbalimbali.<br><br>d) Kufanyike jitihada ya kujenga vibanda vya mwemvuli kwa ajili ya kupumzika wageni wanaofika katika maeneo hayo na kupata vinywaji laini iwe ni kivutio kwa wanaotembelea hapo. |

| Na | Sehemu zilizotembelewa | Yaliyobainika | Ushauri |
|---|---|---|---|
| 4. | Pango la Pete | Ukosefu wa maji.<br><br>Kwenye Pango kunahitaji kujengwa ngazi ndogo ambayo itawarahisishia wageni wanao tembelea sehemu hiyo kuingia ndani kwa urahisi, kukosekana kwa ngazi hiyo ndogo kunasababisha wageni kutokutembelea sehemu hiyo, wananchi wa Pete walikuwa wametengeneza mpango wa kuwa wageni wote wanaotembelea Msitu wa Hifadhi ya Jozani watembelee na Pango hili kwa ajili ya kuiongezea mapato Serikali, na mpango huu ulianza vyema na mapato yaliingia vizuri tu Serikalini lakini kwa sasa umesita kutokana na kukosekana kwa ngazi hiyo,<br><br>Sehemu inayokusudiwa kufanywa Makumbusho ni ndogo mno ni kijichumba kidogo tu kabla ya mpango huu haujaanza Wizara itafakari Zaidi kuhusiana na mpango huu.<br><br>Hakuna vitendea kazi kwa wafanyakazi kama viti na meza pamoja na tochi za kuingilia kwenye Pango, na ukosefu wa umeme | a) Wizara ifanye jitihada ya kupeleka maji eneo hili kwa ajili ya matumizi ya wafanyakazi pamoja na wageni wanaotembelea sehemu hiyo.<br><br>b) Wizara ijenge ngazi katika eneo la kuingilia ndani ya pango hili kwa haraka sana ili itumike kwa wageni na kuiongezea mapato Serikali kukosekana kwa ngazi hii kunapelekea kuikosesha mapato Serikali.<br><br>c) Uongozi wa Wizara ukaiangalie sehemu inayotaka kufanywa makumbusho kwa mazingatio Zaidi.<br><br>d) Wafanyakazi wapatiwe vitendea kazi kwa kupatikana ufanisi Zaidi<br><br>e) Ufanywe utaratibu wa kupelekwa umeme katika Afisi zilizopo hapo Pete. |

| Na | Sehemu zilizotembelewa | Yaliyobainika | Ushauri |
|---|---|---|---|
| 5. | Makumbusho ya Unguja Ukuu | Jengo la Makumbusho liko hatarini hapo baadae kumong'onyoka na kuharibika hii inatokana na maji ya bahari yanayokuja kwa kasi na ni maji ya mvua yanayotiririka kutokea juu ya kilima na kuelekea baharini kwa kasi na kusababisha shimo upande wa kusini wa jengo hilo, ambapo kwa sasa shimo hilo limeanza kugeuzwa jaa na kuanza kutiwa taka. | a) Jitihada za makusudi zifanyike kuyazuwia au kuyapunguza kasi maji ya bahari yanayoendelea kumega ardhi ili kuepusha kufanya hivo.<br>b) Shimo liliopo upande wa kusini ambalo limegeuzwa jaa kwa sasa, ujengwe mtaro au kumwaga zege ili maji yawe yanapita bila ya kuleta athari yeyote ile. Pakiendelea kuwa hivihvi palivyo mvua za masika zijazo zitalisomba jaa lote liliopo hapo na kuzidi kuendelea shimo hilo hadi kwenye nyumba na kupelekea kubomoka kwa jengo hilo kidogo kidogo. |
| 6. | Mji wa Kale Unguja Ukuu | Hakuna kilichoonekana | - |
| 7. | Gofu la Mwinyi Mkuu Dunga | Kuko sawa hakuna tatizo | Matunzo na usafi Zaidi viwe endelevu. |
| 8. | Gofu la Maruhubi | Geti kuu la kuingilia ndani hapako vizuri, gari ndogo zinashindwa kupita kwa ajili ya kuingia ndani.<br>Hapana ofisi ya kukaa na kufanyia kazi wafanyakazi.<br>Hapana choo cha kutumia wafanyakazi na wageni wanaotembelea sehemu hiyo.<br>Hakuna maji safi na salama.<br>Gofu limeanza kuharibika na lina nyufa baadhi ya sehemu.<br>Eneo sio salama lina mwitu na vichaka si safi. | a) Kwenye geti kunahitaji matengenezo ya dharura kwani kwa hali ilivo baadhi ya wageni na madereva baada ya kuiona hali ilivo hughairi kuingia na kukosa mapato kwa Serikali.<br>b) Kujengwe ofisi hata kama chumba kimoja tu kwa ajili ya wafanyakazi wa hapo.<br>c) Kujengwe vyoo kwa ajili ya wafanyakazi na wageni wanaotembelea hapo.<br>d) Maji safi na salama yapatikane kwa ajili ya matumizi ya Kibinaadamu.<br>e) Nyufa zilizoanza kujitokeza zifanyiwe marekebisho kabla athari Zaidi haijajitokeza.<br>f) Eneo lisafishwe liwe safi na hata dawa za kuulia magugu zinaweza kutumika. |
| 9. | Makumbusho ya Kibweni | Eneo liko vizuri halina tatizo | a) Matunzo na usafi vizidi kuendelea na kuimarishwa ili eneo lisije likapoteza uwezo wake. |

| Na | Sehemu zilizotembelewa | Yaliyobainika | Ushauri |
|---|---|---|---|
| 10. | Hodhi la Kidichi | Njia mbaya kutoka barabara kuu hadi kwenye Hodhi.<br><br>Ukosefu wa vyoo na maji safi na salama.<br><br>Afisi pamoja na stoo.<br><br>Uvamizi wa eneo la Hamamu na kujengwa nyumba ya miti na udongo. | a) Ijengwe ngazi pembezoni mwa barabara kuu ya kupandia kuelekea kwenye Hodhi iachwe kutumika njia inayotumika sasa kwani gharama zake za matengenezo ya njia ni kubwa ukilinganisha na ngazi<br>b) Pajengwe Afisi, vyoo, Stoo pamoja na upelekejiwa maji safi.<br>c) Sehemu ya eneo la Hamamu limevamiwa na kujengwa nyumba ya miti na udongo na mwananchi, mwananchi huyo hana lengo zuri kwa serikali.<br>d) Tunashauri uongozi wa Wizara ukutane na uongozi wa Wizara ya Ardhi na Makaazi pamoja na uongozi wa manispaa ya Magharibi A kulitafutia ufumbuzi suala hili haraka sana iwezekenavyo kabla halijafikia hatua mbaya ya mgogoro huu. |
| 11. | Hodhi la Kizimbani | Hali inaonesha sio shuwari katika Hodhi la Kizimbani Kuna Mvutano kati ya Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale na TAASISI YA KILIMO KIZIMBANI juu ya Umiliki wa Eneo hili.<br><br>Kwenye hodhi hakufikiki na wala hakuingiliki kwa sababuTasisi ya Kilimo Kizimbzni wamepanda vipando vyao hadi chini ya ukuta wa Hodhi na chakusikitisha Zaidi wamepanda Miti ya kudumu kama vile miembe mibalungi, michenza na michungwa ambayo baada ya muda mfupi ujao mizizi ya miti hiyo itapasua kuta za hodhi hilo na kuanguka na kupotea kabisa kwa Kumbukumbu na Historia ya sehemu hiyo. | a) Hatua za dharura na za haraka zinatakiwa zichukuliwe ili kuinusuru hali hii yamgogoro uliokuwepo.<br>b) Tunashauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ukutane na uongozi wa Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Mali ya Asili na Mifugo ili kulizungumzia suala hili na kulipatia ufumbuzi wa Haraka kabla ya Hodhi hili halijaharibika na kupotea kabisa.<br>c) Iwekwe eneo ambalo liwe wazi ili kuruhusu wageni walifikie Hodhi hilo kwa matembezi. |
| 12. | Manga Pwani Cave | Kutokuwepo maji safi na salama na ukosefu wa choo. | a) Kujengwe vyoo kwa ajili ya wageni na wenyeji.<br>b) Yapelekwe maji safi na salama kwa ajili ya matumizi yakibinaadamu. |

| Na | Sehemu zilizotembelewa | Yaliyobainika | Ushauri |
|---|---|---|---|
| 13. | Kisima cha Chini Kwa chini Manga Pwani | Kutokuwepo kwa ofisi hadi wafanyakazi kufikia hatua ya kubadilisha kwa matumizi ya choo na kufanya ofisi choo hicho.<br><br>Ukosefu wa vyoo na maji safi na salama kwa matumizi ya kibinaadamu.<br><br>Ile sehemu ya Kisima chenyewe usalama kwa binaadamu na wanyama ni mdogo yanaweza yakatokea maafa wakati wowote ule. | a) Kujengwe ofisi kwa ajili ya matumizi ya wafanyakazi ili waepukane na kukaa chooni.<br>b) Kujengwe vyoo kwa ajili ya wageni na wafanyakazi.<br>c) Kuwekwe uzio ile sehemu ya Kisima tu na sio eneo lote kwa ajili ya kuzuia na kuepusha maafa kwa binaadamu na wanyama. |
| 14. | Gofu la Fukuchani | Ngazi ya kupandia juu inayotumiwa na wageni ni mbovu na haifai kabisa kwani ni ya miti na tayari misumari yake imeanza kuachia.<br><br>Hakuna maji safi na salama, na maji wanayotumia kwa ajili ya chooni si salama kwa matumizi ya kibinaadamu kwani wanachota kwenye shimo linalofugiwa Kasa ambayo yanaweza kumuambukiza mtumiaji maradhi. | a) Ijengwe ngazi ya kudumu na katika sehemu ambayo imetengwa kwa ajili ya ngazi, na wageni waache kutumia ngazi ya miti ambayo inatumika hivi sasa kwa ajili ya kuepusha ajali na maafa kwa wageni wanaotembelea eneo hilo.<br>b) Kupelekwe maji safi na salama kwa ajili ya matumizi ya Kibinaadamu. Na maji yanayotumika hivisasa kutoka katika shimo linalofugiwa Kasa yasitumike kwa ajili ya matumizi ya kibinaadamu. |
| 15. | Pango la (Mvuleni) | Sehemu iko vizuri na inapendeza sana, ila kunatatizo la kutokuwekwa (kununuliwa) umeme kwa wakati na hufikia hadi siku sita umeme haujawekwa na hii upeleke kutokufanywa usafi kwa wakati. | a) Jitihada zifanyike za kuweka umeme wa kutosha kwa ajili ye kupandishia maji ya kufanyia usafi. |
| 16. | Pango la Kuumbi Kajengwa (Jambiani) | Njia ya kutokea Barabara kuu hadi kwenye Pango ni mbovu na haipitiki. | a) Njia itengenezwe angalau kwa uwe-kaji wa Kifusi ili kurahisisha kwa gari kufika eneo hilo bila ya pingamizi. |

| Na | Sehemu zilizotembelewa | Yaliyobainika | Ushauri |
|---|---|---|---|
| 17. | Gofu la Mtoni (Kasri) | Gofu liko vizuri na liko safi linapendeza na kuvutia. | Kutokana na kuwa na eneo kubwa la Gofu hili ukaguzi unashauri eneo hilo litumike kwa kuwaweka wajasiriamali angalau siku mbili kwa wiki ili wafanye biashara zinazohusiana na utalii, bila ya kuathiri mazingira ya eneo hilo pia suala la usafi lizingatiwe zaidi, kwani usafi ni afya na usafi utazidi kuvutia kwa wageni wa ndani na nje kulitembelea eneo hilo. |

Hali halisi ya baadhi ya magofu hayo ni kama inavyoonekana katika picha zifuatazo:-



*Gofu la Fukuchani*



*Kasri la Mtoni*



*Gofu la Hamami Kizimbani*

### 5.5.1.1 Kutokuwepo kwa hatimiliki za baadhi ya maeneo ya utalii

Katika ziara iliyofanywa ya ukaguzi wa matukio ya kutembelea maeneo ya kitalii ukaguzi ulipata fursa ya kutembelea Wizara yenye dhamana ya Utalii na kufanya mazungumzo mbalimbali ikiwemo kuomba baadhi ya nyaraka ili kuweza kuwashauri juu ya namna bora ya kutekeleza majukumu yao ikiwemo kusimamia maeneo ya utalii na kuyahuisha yaliyotelekezwa na yasio fanya kazi kabisa.

Katika mazungumzo hayo ukaguzi uliomba kupatiwa hatimiliki za maeneo 17 na kubaini baadhi yao yakiwa katika haiba nzuri na yenye kuvutia wageni na baadhi yao yakiwa yametelekezwa na hayapo katika hali inayoridhisha.

Wizara ilitutupatia hatimiliki za maeneo 8 tu kati ya 17 tulioyaomba ambapo hadi unakamilika ukaguzi wa hatimiliki maeneyo 9 yakuweza kuonekana hatimiliki zake jambo ambalo limepelekea ukaguzi kushindwa kutoa ushauri wa kina kutokana na kutokujuwa kuwa maeneo hayo ni ya Serikali au ni maeneo ya makaazi ya wananchi. Miongoni mwa hatimiliki za maeneo tuliopatiwa kwa ukaguzi ni kama inavyoonekana hapo chini:-

**Maeneo ambayo hati zimepatikana kwa ukaguzi**

1. Mangapwani. (Cave)
2. Kizimbani Dole.
3. Pete
4. Mangapwani (Kisima cha chini kwa chini)
5. Fukuchani.
6. Mvuleni.
7. Dunga Kiembeni (Mwinyimkuu).
8. Makunduchi Kajengwa.

**Maeneo ambayo hati hazijapatikana kwa ukaguzi**

1. Hodhi la Hamamni.
2. Hodhi la Kidichi.
3. Gofu la Maruhubi
4. Gofu la Mtoni (Kasri)
5. Gofu la Bihole.
6. Mji wa Kale Unguja Ukuu.
7. Makumbusho ya Unguja Ukuu.

Katika maeneo kumi na saba (17) yaliyokaguliwa ukaguzi umebaini maeneo mawili tu ndiyo mipaka yake imeonekana ambayo ni eneo la Kisima cha Chini kwa Chini Manga Pwani na eneo la Hodhi la Kidichi. Aidha eneo la Sultani Burge na Makumbusho ya Kibweni hayahitaji hati miliki kwa kuwa yameazimwa kutoka kwenye taasisi nyengine za Serikali.

Kutokuwa na alama (Beacon) katika maeneo ya magofu hayo kunaweza kupelekea uvamizi wa wananchi unaotokana na ujenzi holela katika maeneo ya makumbusho ya kitalii. Ukaguzi unaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kufanya mambo yafuatayo:-

a) Wizara ihakikishe inafanya jitihada za makusudi kuyatembelea na kuyaekea alama maalum maeneo yote yanayomilikiwa na Serikali ili kuepusha kujitokeza kwa uvamizi wa maeneo hayo.

b) Wizara kuhakikisha inatengeneza mazingira mazuri ambayo yatapelekea kufikika katika maeneo hayo jambo ambalo litaongeza kipato cha Serikali kinachotokana na ada za tozo ya utalii.

c) Wizara ihakikishe inachukuwa jitihada za makusudi kuyafanyia ukarabati maeneo yote ambayo hayapo katika mtazamo mzuri wa kivutio cha utalii na yale ambayo yana muonekano mzuri yafanyiwe matangazo maalum (promotion) ya kuyatangaza ili kuongeza utalii wa ndani kwa wazawa pamoja na utalii wa nje kwa wageni kwa lengo la kuongeza mapato.

d) Kuna sehemu kama Gofu la Maruhubi, Gofu la Mtoni na Gofu la Fukuchani ni maeneo ambayo yana sehemu kubwa ambayo inaweza ikatumika kwa mambo mengine kama vile kutenga siku maalum na kuwapeleka wajasiriamali kufanya biashara zao ndogo ndogo kwa lengo la kukuza utalii wa ndani.

e) Wizara kuhakikisha inaruhusu biashara ndogo ndogo za wamachinga ambao watakua na fursa za kufanya biashara kwa wageni ambao watakuwa wanafika katika maeneo hayo kwa lengo la kukuza kipato kwa wafanya biashara wadogo wadogo (wamachinga).

f) Uongozi wa Wizara uwatumie wafanyakazi waliomo vituoni kwa kubuni vianzio vipya vya mapato kwani wao ndio wanaokuwepo kwa muda mrefu katika maeneo hayo na kujuwa mahitaji ya wageni wanaotembelea sehemu hizo.

g) Ili ionekane Wizara iko tayari kukuza pato la taifa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi MKuu wa Hesabu za Serikali iko tayari kutoa mafunzo elekezi ya mbinu na namna bora ya kuanzishwa vianzio vipya vya ukusanyaji wa mapato ikiwemo mbinu za kudhibiti uvujaji wa mapato ya Serikali.

#### 5.5.1.2 Kukosekana kwa ripoti ya upembuzi yakinifu ya Ukarabati wa Majengo

Kutokana na mabadiliko ya gharama za ujenzi kuonekana zinapanda siku hadi siku na kwa vile gharama kubwa hutumika katika ukarabati wa majengo ya kale unaofanywa na wizara ukaguzi uliomba kupatiwa ripoti ya upembuzi yakinifu ili iweze kujiridhisha juu ya hatua ya ujenzi unavyoendelea pamoja na kutoa ushauri utakaopelekea kupunguza kwa matumizi ya gharama za ujenzi na kutumia ujenzi wenye gharama nafuu ambapo utakuwa ni kivutio kizuri cha watalii jambo ambalo limepelekea ukaguzi kushindwa kupatiwa ripoti ya upembuzi yakinifu.

Aidha, kutokana na wizara kutumia gharama kubwa kwa ajili ya kuendeleza nyumba zake za kihistoria kutokana na kuimarisha vivutio vya utalii ukaguzi ulitaka kujua hatua zinazochukuliwa kabla ya kuanzwa hatua za ukarabati wa majengo ya kihistoria na kukutana na wahandisi wa Wizara ambao wanashughulikia ujenzi huo na kuhojiana nao juu ya hali ya ujenzi ulivyoanza na ulipofikia na jinsi gani ujenzi huo unavyofuata utaratibu husika.

Aidha wahandisi hao walieleza kwamba taratibu au hatua za ujenzi zipo za aina tano (5) ambazo ni:-

(i) Makubaliano (Inception Phase)

(ii) Awamu ya Uratibu (Planning Phase)

(iii) Utekelezaji (Excution Phase)

(iv) Ufuatiliaji, Uchambuzi na Ufanisi (Monitoring, Evaluation and Performnace)

(v) Hatua ya ukamilishaji (Closure Phase.)

Baada ya kupata uchambuzi huo wa hatua za ujenzi ukaguzi ulibaini kwamba Wizara hawazitekelezi hatua hizo isipokuwa hatua ya tatu tu Utekelezaji (Excution Phase.)

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kwa kiasi kikubwa ujenzi kuwa chini ya kiwango kisichoridhisha au kupelekea kutofikia malengo yaliokusudiwa.

Ukaguzi umebaini kukosekana kwa tathmini za athari za kimazingira na urithi zinazofanywa kabla ya kufanyika matengenezo, tathmini ambazo zitaweza kuishauri Serikali na kutoa taswira halisi ya umuhimu wa majengo hayo na madhara yake pindi ya kiachwa hadi kuanguka, pamoja na matumizi sahihi baada ya kuimarishwa kwake ili yawe endelevu. Pia hakuna kumbu kumbu za michoro na picha ambazo hutoa sura halisi ya jengo kabla ya kufanyiwa matengenezo na baada ya kumalizika hali inayopelekea kujua mabadiliko yaliyofanyika kwa nyakati tofauti.

Maeneo yaliyofanyiwa matengenezo pamoja na thamani iliyotumika kwa kipindi cha miaka miwili ni kama ifuatavyo:-

**Jadweli Nambari 33 : Kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020**

| Eneo | Pahala | Thamani fedha (Shs) |
|---|---|---|
| Mwinyi Mkuu | Dunga | 802,474,304 |
| Mvuleni | Fukuchani | 695,855,383 |
| Mkamandume | Pujini - Pemba | 878,309,587 |
| **Jumla** | | **2,376,639,274** |

**Jadweli Nambari 34 : Kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021**

| Eneo | Pahala | Thamani ya fedha (Shs) |
|---|---|---|
| Mvuleni | Fukuchani | 67,721,275.53 |
| Mwinyi mkuu | Dunga | 143,056,387.72 |
| Mkamandume | Pujini – Pemba | 66,398,542.77 |
| ZBC | Chake chake - Pemba | 118,927,310.10 |
| **Jumla** | | **396,103,516.12** |

Kutokufuatwa kwa taratibu za ujenzi kunapelekea kutokuwa na majengo yaliyoimara na kupelekea kufanyika kwa ujenzi huo mara kwa mara ambapo kunasababisha kutofanyika kwa malengo mengine yaliokusudiwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale usimamie kwa uangalifu juu ya ujenzi wa nyumba za Serikali kwani kutapelekea kwa rasilimali hizo kudumu na kufikia lengo lililokusuiwa na hatimae kuweza kurithiwa na vizazi vijavyo.

### 5.5.1.3 Kutokupatikana kwa maelezo yakutosha juu ya kugundulika kwa maeneo ya kihistoria na mambo ya kale

Baada ya ukaguzi kupitia ripoti za utekelezaji ukaguzi ulibaini kwamba kuna utekelezaji wa malengo ya Wizara umefanyika juu ya utafutaji wa maeneo mapya kwa ajili ya kukuza mapato ya Serikali, lakini ukaguzi umepata maelezo ya kutosha kwa baadhi ya maeneo na baadhi ya maeneo bado haijafanikiwa kupata maelezo husika.

Katika muendelezo wa hatua zake za kuyatafuta, kuyahifadhi na kuyalinda maeneo ya kihistoria Idara ya Makumbusho na mambo ya kale imefanikiwa kufunga Boya katika Mji wa Kale uliozama wa Mkumbuu uliopo Pemba. Kwa mujibu wa wanahistoria ni kwamba mji huu ulikuwa wakiishi watu kama kawaida mwanzoni mwa karne ya kwanza, kabla ya kuongezeka kina cha maji ya bahari na kusababisha mji huu kuzama. Kufungwa kwa boya hilo kutapelekea kulitangaza eneo hilo na kuongeza idadi ya wageni.

Ukaguzi unaomba kupatiwa ripoti ya ugunduzi wa mji na kupata gharama za ujenzi wa boya hilo.

Idara ya Makumbusho na mambo ya kale bado inaendelea kufanya utafiti mkubwa wa Akiolojia katika maeneo mapya ya kaskazini Unguja. Maeneo haya yanajumuisha Shehia ya Mangapwani, Mafufuni, Makoba, Kiongwe Kidogo, Kidanzini, Muanda na Misufini.

Katika utafiti huo mapango manne yaligunduliwa nayo ni:-

a) Pango la Nawawi

b) Pango la Umundi

c) Pango la Mwenge

d) Pango la Mapopo.

Aidha Idara pia ilifanya tafiti ndogo katika baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Kusini Unguja kama Muungoni, Unguja Ukuu, Fumba, Uzi na Pete.

Ukaguzi umetembelea maeneo yaliopo Kaskazini na kuyaona yapo na yanatumika kwa mambo ya kijamii kama vile Pungwa n.k lakini ikiwa Wizara ina mpango wa kuyaendeleza maeneo hayo itatakiwa kurekebisha baadhi ya mambo bila ya kuharibu utamaduni wa Wananchi wa maeneo husika, na pia njia za kufikia maeneo hayo bado haziko katika hali ya kuridhisha na kubwa zaidi la kuzingatia usalama wa wageni wataofika katika maeneo hayo. Kwa maeneo yaliopo Mkoa wa Kusini ukaguzi bado haukuwahi kufika kuyakagua maeneo hayo.

Baadhi ya mapango hayo ni kama yanavyoonekana katika picha zifuatazo:-




*Pango la Umundi*



*Pango la Mapopo*



*Pango la Nawawi*



*Pango la Mwenge*

Fedha zinapotumika kufanya tafiti mbali mbali na zisipofanyiwa malengo yaliyokusudiwa inapelekea kurejesha nyuma jitihada za maendeleo ya Serikali.

Ukaguzi unashauri Uongozi na watendaji wa Idara ya makumbusho na Mambo ya kale kuyatunza na kuyaimarisha maeneo yote yenye fursa za Utalii mambo ya kale yaliyopo nchini.

### 5.5.1.4 Kukosekana kwa ripoti ya nyumba za kulaza wageni ambazo sio rasmi

Idara ya Utalii imekutana na Kamati za Utalii za Wilaya zote za Unguja na kuzielekeza njia bora za utoaji wa huduma kwa wateja hasa katika kipindi hiki ambapo dunia imekabiliwa na janga la COVID 19.

Pia Idara imezitaka Kamati hizo kuzifuatilia nyumba zote za kulaza wageni ambazo sio rasmi kwa lengo la kuzirasimisha nyumba hizo ili ziweze kutambulika na kuchangia pato la nchi.

Ukaguzi umeomba kupatiwa ripoti hiyo ya kuzitambua hizo nyumba za kulaza wageni ambazo sio rasmi kama kamati zilivyoagizwa. Vile vile ukaguzi ukataka kujua ni hatua zipi zimechukuliwa na Wizara juu ya kuliondosha suala hilo lakini hadi ukaguzi unakamilika ripoti hiyo haikupatikana kutoka kwa wahusika.

Kutokufuatilia sehemu za wawekezaji kwa umakini kunapelekea kujitokeza kwa vitendo vya upotevu wa mapato ya Serikali na kufanya isifikie malengo yake iliyokusudia na pia kuweza kujificha kwa wageni wasio waaminifu.

Ukaguzi unashauri kwamba Wizara isimamie kwa ukamilifu sheria za wawekezaji ili ziende sambamba na malengo yaliokusudiwa.

### 5.5.1.5 Utelekezwaji wa mali za Mkandarasi na Serikali

Ukaguzi umebaini kwamba kuna malipo ya walinzi ambao wapo Kibele kwa ajili ya kulinda eneo la mambo ya kale ya Serikali lakini baada ya kufuatilia ukaguzi ukabaini kwamba walinzi waliokuwepo sio kwa ajili ya Wizara ni Walinzi wa Kampuni ya MECCO kwa ajili ya kazi zao. Ukaguzi ulibaini kwamba mara tu baada ya kuporomoka kwa jengo la Beit-el-Ajab tarehe 25/12/2020 taratibu ya kulishughulikia jengo hilo zikaanza kwa kutafuta Wakandarasi kwa ajili ya

kulijenga jengo hilo.

Aidha baada ya kufika eneo la Kibele na kujadiliana na Muhandisi wa Wizara alieleza kwamba Mkataba wa Mkandarasi ulikuwa na kipengele kinacholeleza kwamba ikiwa Mkandarasi atashindwa kuendelea na kazi,vifaa vyote vitakuwa ni mali ya Serikali.

Baada ya kuonekana Mkandarasi huyo ameshindwa kutokana na jengo hilo kuporomoka Serikali ilichukua vifaa hivyo na kuvipeleka Kibele kwa kuvihifadhi. Ukaguzi ulifika katika eneo vilipohifadhiwa na kubaini kwamba vifaa havikuwa katika mazingira salama ya uangalizi mzuri ambapo pi kulikuwa na hatari ya kuja kuchakaa kwa vifaa hivyo kwa baadae kutokana na mazingira mabaya yaliyowekwa vifaa hivyo.

Aidha, ukaguzi umepata taarifa ya kwamba Mkandarasi amefungua kesi Nchini kwao wakati mkataba unamtaka afungue kesi nchini Tanzania, ikiwa Mkandarasi atashinda kesi au Serikali na vifaa vile tayari vimetelekezwa na kupelekea kuchakaa (kuharibika) Serikali inaweza kupata hasara ya kulipa vifaa hivyo kutokana na kuchakaa kwa vifaa hivyo kunakosababishwa na sehemu mbaya iliyohifadhiwa vifaa.

Vile vile zipo haki za wafanyakazi ambao walifariki na wengine kujeruhiwa hadi ukaguzi unakamilika umeshindwa kupata taarifa ya hatima ya Wafanyakazi hao.

Baadhi ya vifaa vya Mkandarasi vilivyotelekezwa ni kama inavyoonekana katika picha zifuatazo: -











Ukaguzi unashauri kwamba Wizara ifungue kesi kwa ajili ya kusimamia mkataba wao waliofunga na pia kusimamia haki za waathirika wa janga hilo kwa lengo la kupata haki zao. Muendelezo wa ukaguzi wa matukio mbalimbali yanayohusiana na shughuli nzima za utalii utaendelea na kutolewa ripoti kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali pindipo hali ya fedha itakapo ruhusu.

Ni matumaini yangu kwamba ripoti hii italeta chachu ya mabadiliko katika sehemu mbalimbali zilizoibuliwa kuonekana kwa kasoro ambazo tunatarajia kwa namna moja au nyengine zitachukuliwa na kufanyiwa kazi ili tija iliyokusudiwa iweze kupatikana. Hata hivyo nitakuwa na furaha kubwa sana pindipo watumiaji wa taarifa hii watakuja na maboresho,mapendekezo pamoja na maelekezo ya namna ya kufanya ukaguzi wa muendekezo wa mambo yanayohusu uibuaji wa vyanzo vipya vya mapato vitokanavyo na utalii wa ndani.

# SURA YA SITA

## 6.0 MIRADI ILIYOTEKELEZWA KATIKA SEKTA ZA AFYA

## 6.1 MRADI WA KUDHIBITI VVU, KIFUA KIKUU NA UKOMA ZANZIBAR (ZIHTLP)

Wizara ya Afya Zanzibar inapokea ruzuku ya Mfuko wa Kimataifa tangu mwaka 2003. Ruzuku za GF zinatekelezwa kupitia Mpango Jumuishi wa VVU/TB na Ukoma (ZIHTLP). Uangalizi hutolewa na Katibu Mkuu, ambaye ni afisa mhasibu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, akisaidiwa na Naibu Katibu Mkuu, Mkurugenzi Mkuu na Mkurugenzi wa Huduma za Kinga na Elimu ya Afya.

Mipango hiyo inasaidiwa na idara nyingine za Wizara ya Afya kama vile Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi (PMU) chenye jukumu la kuratibu shughuli zote za manunuzi, Bohari Kuu ya Dawa (CMS) inayohusika na utabiri wa dawa na vitendanishi, uhifadhi na usambazaji na Mfumo wa Taarifa za Zanzibar imekuwa ikitekeleza shughuli za ushirikiano wa VVU na TB tangu mwaka 2006. Wagonjwa wote wanapimwa VVU, pamoja na kuchunguzwa TB, na walioambukizwa TB-VVU hupelekwa kwenye vituo vya matunzo na matibabu kwa ajili ya kuanza ART.

Idadi ya wagonjwa wa Kifua Kikuu walioambukizwa VVU kwa pamoja ilikuwa karibu 15% mnamo  mwaka 2016. Asilimia ya wagonjwa wa Kifua Kikuu/ VVU walioanza ART imeongezeka kutoka asilimia 52 kwa mwaka 2012 hadi asilimia  kwa 88 mwaka 2016. Kwa VVU, wao Key Population (KPs) Zanzibar wanafafanuliwa kama wanaume wanaofanya ngono na wanaume (MSM), watu wanaojidunga dawa (PWID), wanafunzi katika vituo vya kurekebisha tabia (magereza) na wafanyabiashara ya ngono (SW).

Kwa ugonjwa wa TB, KP wanatambuliwa kama wanafunzi katika Taasisi za Huduma za Urekebishaji (Magereza), , watoto, watu walioko kwenye mikusanyiko na wahudumu wa afya wanaofanya kazi katika vituo vya afya vinavyodhibiti Ugonjwa TB na VVU.

### 6.1.1 TAARIFA YA FEDHA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MRADI

**Taarifa ya Mapato na Matumzi**

Mradi wa kudhibiti VVU, Kifua Kikuu na Ukoma kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi 2020/2021 ulikadiriwa kutumia jumla ya dola za Kimarekani 5,095,999.98 zilizofadhiliwa na Mshirika wa Maendeleo (Global Fund). Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya dola za Kimarekani 3,602,890.02 zimetumika sawa na asilimia 70.7 ya makadirio. Mchanganuo wa upatikanaji na utumiaji wa fedha za mradi huo ni kama inavyonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 35 : Mapato na Matumizi**

| Maelezo | Kiasi cha fedha (USD) |
|---|---|
| Salio anzia 1 Julai,2020 | 184,935 |
| **Fedha zilizopokelewa** | |
| Mshirika wa Maendeleo (Global Fund) –paid direct by GF to Suppliers | 2,328,045.02 |
| Mshirika wa Maendeleo (Global Fund)- direct by GF to Wizara ya Afya | 2,582,999.98 |
| Jumla ya fedha iliyopokelewa | 4,911,045 |
| **Jumla ya fedha iliyopatikana** | **5,095,980** |
| Matumizi kwa 2020/2021 | 3,602,890.02 |
| Salio la mwisho 31 disemba,2020 | **1,493,090** |

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.1.1.1 Kukosekana kwa taarifa za matumizi ya fedha za mradi shilingi 48,020,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 48,020,000 zimelipwa kwa Msambazaji K. Brain Scientific kwa kutumia hati hambari 5774 ya tarehe 20 Novemba,2020 kwa ajili ya ununuzi wa dawa za Metadone lakini hadi ukaguzi unakamilika taarifa za matumizi ya fedha hizo hazikuweza kupatikana. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa upotevu wa fedha za Umma ambapo ni kwenda kinyume na Kifungu Nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kupitia wasimamizi wa mradi kuhakikisha kwamba katika kipindi chote cha utekelezaji wa mradi panakuwepo na matumizi sahihi ya fedha na rasilimali za Umma kwa kuzingatia Sheria, Kanuni pamoja na miongozo mbali mbali ya fedha inayotolewa Kitaifa na Kimataifa ikiwa ni pamoja na kuongeza umakini katika uaandaaji wa ripoti mbali mbali za mradi

#### 6.1.1.2 Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 196,902,972

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Afya kupitia mradi wa ZIHTLP imefanya manunuzi ya bidhaa kwa watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato, ambapo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba inafanya manunuzi ya bidhaa na huduma kwa watoa huduma waliosajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 36 : Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa**

| Nambari ya Hati | Tarehe ya malipo | Aliyelipwa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 5774 | 20-11-2020 | K Brain Scientific | 48,020,000 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa Methadone |
| 5842 | 28-12-2020 | K Brain Scientific | 47,411,175 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa dawa za kulevya (DOA) Unguja |
| 5815 | 10-12-2020 | Kaya Furniture | 28,422,940 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa Jokofu, UPS na Sanduku baridi |
| 5821 | 11-12-2020 | Akama Holding Company | 14,781,830 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya Maabara |
| 5840 | 21-12-2020 | Alkaga Enterprises | 46,907,357 | Malipo kwa ajili ya uchapishaji wa fomu mbali mbali |
| 5635 | 23-07- 2020 | Ramson Enterprises | 11,359,670 | Malipo kwa ajili uchapishaji wa zana za kufanyia kazi |
| **Jumla** | | | **196,902,972** | |

## 6.2 MRADI WA KUTOKOMEZA MALARIA ZANZIBAR (ZAMEP)

Mradi wa Kutokomeza Malaria Zanzibar (ZAMEP) upo chini ya Idara ya Huduma za Kinga na Uhamasishaji wa Afya katika Wizara ya Afya Zanzibar.

Mradi huo ulipokea fedha chini ya programu ya kuongeza kasi ya kutokomeza Malaria Zanzibar ikiwa ni Muendelezo wa Mpango ulioanza tarehe 1 januari, 2018 hadi tarehe 31 Disemba,2020.

Mpango wa Kutokomeza Malaria Zanzibar (ZAMEP) unafadhiliwa na Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Malaria kwa kushirikiana na Rais wa Marekani Malaria Initiatives (PMI).

### 6.2.1 MALENGO YA MRADI

Mradi wa ZAMEP umepangwa kutekelezwa katika kipindi cha miaka 5 ukiwa na lengo la kupunguza kiwango kikubwa cha maambukizo ya ugonjwa wa Malaria kwa asilimia 100 ifikapo mwaka 2023. Katika kulifikia lengo lililokusudiwa mradi huu umeelekeza kutekeleza mambo yafuatayo:-

- Kuanzisha uchunguzi wa" entomological " katika maeneo yenye malaria kutoka asilimia 0 ya mwaka 2017 hadi asilimia100 ifikapo mwaka 2023.
- Kuboresha tabia, mawasiliano ya kijamii na uhamasishaji kwa watu juu ya hatua ya kutokomeza malaria kwa asilimia 90 ifikapo 2023.

### 6.2.2 TAARIFA YA FEDHA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MRADI

#### Taarifa ya Mapato na Matumzi

Mradi wa Kutokomeza Malaria Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ulikadiriwa kutumia jumla ya dola za Kimarekani 1,196,161. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 jumla ya dola za Kimarekani 837,205 zimetumika sawa na asilimia 69.99 ya makadirio. Mchanganuo wa upatikanaji na utumiaji wa fedha za mradi huo ni kama inavyonekana hapo chini:-

**Jadweli Nambari 37 : Taarifa ya fedha za mradi**

| Maelezo | Kiasi cha fedha kilichotumika (USD) |
|---|---|
| Salio anzia 1 Julai,2019 | 359,464 |
| **Fedha zilizopokelewa** | |
| Global Fund (GF) | 836,697 |
| Mchango wa serikali | - |
| Jumla ya fedha iliyopokelewa | 836,697 |
| **Jumla ya fedha iliyopatikana** | **1,196,161** |
| Matumizi kwa 2019/2020 | 837,205 |
| Salio la mwisho 30Juni,2020 | **358,956** |

## MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI

### 6.2.2.1 Kutokuwepo kwa Mpango wa mwaka wa manunuzi

Katika ukaguzi wa Mradi wa ZAMEP imebainika kwamba uongozi wa Mradi haukuandaa mpango wa ununuzi wa mwaka ili kuweza kubainisha mahitaji yake ya manunuzi ya bidhaa au huduma katika kipindi cha mwaka husika kulingana na makadirio ya mapato na matumizi kuhusu utekelezaji wa mradi wa ZAMEP.

Kutokuwepo kwa mpango wa mwaka wa manunuzi kunaweza kusababisha uwepo wa kufanyika manunuzi ambayo hayakuidhinishwa pamoja na kupelekea matumizi mabaya ya fedha za Serikali ambapo ni kwenda kinyume na kifungu cha 42(1) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Nambari 11 ya mwaka 2016

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mradi kuhakikisha kwamba unaandaa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka kwa mujibu wa matakwa ya Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 ili kuepuka kufanya manunuzi ambayo hayakuainishwa na kuthibitishwa katika mpango wa manunuzi wa mradi

### 6.2.2.2 Vifaa ambavyo havikurikodiwa katika daftari la ghalani shilingi 16,549,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainka kwamba jumla ya shilingi 16,549,000 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbalimbali vinavyohusiana Covid-19 katika utekelezaji wa mradi huo Pemba lakini dosari iliyobainika ni kutokurikodiwa kwa vifaa hivyo katika daftari la ghalani hali ambayo inaweza kupelekea kutokujulikana kwa idadi ya vifaa vilivyonunuliwa pamoja na pahala vilipotumika ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mradi kuandaa daftari na kurikodi taarifa zote zinazohusiana na vifaa vinavyonunuliwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo mbali mbali iliyopo. Mchanganuo wa malipo ya ununuzi wa vifaa hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 38 : Vifaa ambavyo havikurikodiwa katika daftari la ghalani**

| Hati Namba | Hundi Namba | Aliyelipwa | Maelezo | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 2640 ya 23/10/2020 | TT | One 2 one Limited | Ununuzi wa vifaa mbali mbali vya Komputers kwa ajili kuimarisha maabara ya PHL kwa taratibu za PCR | 10,488,000 |
| 2641 ya 23/10/2020 | TT | One 2 one Limited | Ununuzi wa vichapishaji ili kuendesha mfumo wa usimamizi wa matukio na maendeleo ya RRT katika ngazi ya kitaifa | 1,425,000 |
| 2642 ya 23/10/2020 | TT | One 2 one Limited | ununuzi wa vichapishi ili kuendesha mfumo wa usimamizi wa matukio wa Wilaya na maendeleo ya RRT katika ngazi ya kitaifa. | 4,636,000 |
| **Jumla** | | | | **16,549,000** |

### 6.2.2.3 Matumizi yaliyofanyika nje ya bajeti dola za Kimarekani 359,928

Katika ukaguzi wa mradi imebainika kuwepo kwa matumizi mbali mbali yaliyofanyika kwa ajili ya shughuli za mradi wa ZAMEP lakini dosari iliyobainika ni kufanyika kwa matumizi hayo nje ya bajeti hivyo kupelekea jumla ya dola za Kimarekani 359,928 kufanyiwa matumizi bila ya kupata muongozo unaotokana na makadirio ya mapato na matumizi. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa matumizi ya fedha kinyume na mpango wa Mradi pamoja na matumizi ya fedha yasioidhinishwaji ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyonekana katika jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 39 : Matumizi yaliyofanyika nje ya bajeti**

| Namba | Maelezo | Kiasi kilichokadiriwa (USD) | Kiasi kilichotumika (USD) | Tofauti ya fedha (USD) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Gharama za usafiri | 304,497 | 393,982 | 89,485 |
| 2. | Bidhaa za Afya zisizona dawa (HPNP) | 16,065 | 154,254 | 138,189 |
| 3. | Bidhaa za Afya -Vifaa (HPE) | - | 1,304 | 1,304 |
| 4. | Ununuzi na usambazaji wa -Chain Mgt Cost (PSM) | 321 | 103,094 | 102,772 |
| 5. | Vifaa visivyo vya (NHP) | 49,019 | 70,329 | 21,310 |
| 6. | Nyenzo za Mawasiliano na Machapisho (CMP) | 1,950 | 4,418 | 2,467 |
| 7. | Programu za Utawala | 19,306 | 23,706 | 4,401 |
| **Jumla** | | | | **359,928** |

### 6.2.2..4 Kutokutekelezwa kwa baadhi ya shughuli za Mradi USD 38,222

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa jumla ya dola za Kimarekani 38,222 ambazo zilipangwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali za mradi katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Desemba, 2020 lakini dosari iliyobainika ni kutokutekelezwa kwa shughuli hizo kwa mujibu wa mpango wa utekelezaji wa mradi huo hali iliyopelekea kukosekana kwa huduma ziliziokusudiwa.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kutokufikiwa kwa malengo tarajiwa ya mradi ambapo ni kwenda kinyume na Muongozo wa Utekelezaji wa Mradi.

Ukaguzi unashauri uongozi mradi wa ZAMEP uhakikishe shughuli za mradi zilizopangwa zinafanyika kwa wakati kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa ili kuweza kufikia lengo la mradi.

**Jadweli Nambari 40 : Kutokutekelezwa kwa baadhi ya shughuli za Mradi**

| Namba | Shughuli ya mradi | Kiasi kilichotengwa (USD) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1. | Msaada wa maisha kwa wateja | 8,701 | Shughuli hii ilikusudiwa kutoa huduma za uendeshaji katika Vituo viwili vya Tiba ya Maradhi ya maambukizo ya Virusi vya Corona (HIDTU) (Vitongoji na Kidimni) na majumbani Zanzibar. |
| 2. | Msaada wa Kiufundi kwa Toleo la Zanzibar ELMIS Utoaji wa CMS | 29,521 | Shughuli hii ilipangwa kutekelezwa katika robo ya 11. |
| **Jumla** | | **38,222** | |

## 6.3 MRADI WA UJENZI WA JENGO LA MAMA NA MTOTO - HOSPITALI YA CHAKE CHAKE PEMBA

Mradi wa ujenzi wa jengo la Mama na Mtoto la Hospitali ya Chake Chake Pemba limeanzishwa ukiwa na lengo la kupunguza changamoto ya ufinyu wa nafasi kwa watu ambao wanapata huduma ya mama na mtoto.

Mradi huu umefadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asilimia 100 ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Afya umeingia makubaliano ya mkataba yenye kumbu kumbu namba SMZ/HO1/W/NCB/W/2018/2019/13 uliosainiwa tarehe 17/09/2019 baina ya Wizara ya Afya Zanzibar na kampuni ya ujenzi (RANS Company Limited) wenye thamani ya shilingi 1,449,968,660 pamoja na VAT ambapo kwa mujibu wa mkataba wa ujenzi muda halisi uliopangwa kukamilika ni miezi kumi na mbili (12) kuanzia tarehe 01/06/2020 hadi 01/06/2021.

Katika hatua ya utekelezaji wa mradi imebainika mshauri elekezi alifunga mkataba na Wizara ya Afya wenye thamani ya shilingi 36,721,000 tarehe 20/9/2021 ambapo katika mkataba huo malipo hayo yalitakiwa yalipwe kwa awamu na kwa kima tofauti ambapo asilimia 40 italipwa wakati wa kufungwa kwa mkataba na asilimia 30 italipwa wakati kazi inaendelea na asilimia iliyobakia 30 italipwa wakati kazi itakapo kamilika na kukabidhiwa ikiwemo kuridhika kwa kiwango cha kazi iliyofanyika.

### 6.3.1 TAARIFA YA FEDHA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MRADI

**Taarifa ya Matumizi**

Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto katika Hospitali ya Chake Chake Pemba ulikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,449,968,660 katika hatua za awali ambapo hadi ukaguzi unakamilika imebainika kuwepo kwa ongezeko la makadirio ya gharama za ujenzi la shilingi 2,288,972,200 na kupelekea kuongezeka kwa makisio halisi ya gharama za ujenzi na kufikia jumla ya shilingi 3,738,940,860 sawa na asilimia 157 ya makadirio ya awali.

**Utekelezaji wa mradi**

Katika utekelezaji wa mradi wa jengo la mama na mtoto imebainika uwepo wa dosari mbali mbali za kiutendaji ambapo kunapelekea kujitokeza kwa viashiria vya kutokutekelezeka kwa mradi kwa mujibu wa viwango vilivyokusudiwa jambo ambalo huenda likapelekea kujitokeza kwa gharama za ziada kinyume na matarajio na matakwa ya Serikali.

**MATOKEO YA UKAGUZI NA MAPENDEKEZO**

#### 6.3.1.1 Kutokutayarisha na kuwasilisha taarifa za hesabu za miradi

Kwa mujibu wa kifungu Nambari 119(1) cha sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa fedha za Umma ya mwaka 2016 inawataka wakuu wa taasisi kutayarisha taarifa za mapato na matumizi na kuziwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kukamilika kwa matumizi.

Ukaguzi umebaini Wizara ya Afya imetekeleza Miradi wa ujenzi wa ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto Hospitali ya Chake Chake ambapo kwa mujibu wa taratibu za kisheria Wizara ilitakiwa kutayarisha na Kuwasilisha Taarifa za matumizi zinazohusiana na utekelezaji wa mradi huo kwa lengo la kukaguliwa na kutolewa ushauri wa kitaalamu.

Hadi ukaguzi unakamilika taarifa hizo hazikuwasilishwa jambo ambalo limenyima fursa ya kuweza kufahamu fedha halisi iliyopatikana na kutumika katika shughuli za uendeshaji na utekelezaji wa mradi huo.

#### 6.3.1.2 Kuwepo kwa ucheleweshwaji wa malipo

Katika dosari hiyo imebainika kujitokeza kwa kasoro ya ucheleshwaji wa upatikanaji wa malipo kwa muibu wa barua yenye R/MOH/CMCH/18 ya tarehe 28/5/2021 iliyotolewa na Mkandarasi kwenda kwa Wizara ilionesha madai kuomba kulipwa fedha hizo. kwa mujibu wa ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya shilingi 632,752,504.06 zimelipwa kwa certificate tatu za awali.

#### 6.3.1.3 Kuongezeka kwa gharama za ujenzi

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa ongezeko la gharama za ujenzi zilizowasilishwa kwa mkandarasi kwa mujibu wa barua yenye kumbu kumbu namba R/MOH/NCHP/04 ya tarehe 21/11/2019 yenye thamani ya shilingi 982,397,200 na kupelekea jumla ya gharama ya ujenzi kufikia shilingi 2,432,365,860 ambapo sawa na aslimia 67.75

Aidha ukaguzi umebaini kuwepo ongezeko jengine la gharama kwa kazi za ziada zilizowasilishwa kwa mujibu wa barua yenye kumbu kumbu namba R/MOH/CMCH/16 ya tarehe 29/7/2021 kutoka kwa mkandarasi kwenda kwa mshauri elekezi ambapo barua hiyo ilikuwa na ongezeko la shilingi 1,306,575,000 na kupelekea gharama kamili kufikia shilingi 3,738,940,860 sawa na ongezeko la asilimia 53.72 na kupelekea kuwepo kwa ongezeko la jumla ya shilingi 2,288,972,200 sawa na ongezeko la asilimia 157.86 kutokana na gharama za awali za mkataba.

Kutokana na kuongezeka kwa gharama za ujenzi mambo yafuatayo yamebainika:-

- Kutokana na kuwepo kwa ongezeko hilo kumejitokeza ukiukwaji wa sheria ya Ununuzi ambapo kifungu nambari 49(4-5) cha kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2021 kinaeleza kwamba " iwapo malipo yatazidi bei ya mkataba zaidi ya 15% yawasilishwe kwa mlipaji Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata uthibitisho au Baraza la Wawakilishi (Approval)." Jambo ambalo ukaguzi haukupatiwa uthibitisho huo.
- kwa mujibu wa kifungu cha 6(1)(c) cha Sheria ya manunuzi namba ya 2016, pindipo inapotokezea nyongeza ya mkataba wa awali kupewa mzabuni wa mwanzo kuendela na kazi hio haitatakiwa uongezeka kwa asilimia 25 ya thamani ya zabuni ya awali jambo ambalo halikuzingatiwa katika utowaji wa zabuni hio.

Ukaguzi umebaini gharama za ujenzi huengezeka kutokana na kuwepo kwa mabadiliko ya ramani ya awali na kupelekea kuengezeka kwa baadhi ya vitu ambavyo havikuwemo kwenye mchoro wa awali na kupelekea ongezeko la shilingi 2,288,972,200 sawa na ongezeko la asilimia 157.86 jambo ambalo linapelekea kuchelewa kukamilika kwa mradi kulingana na wakati uliopangwa ambapo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Afya kusimamia kwa karibu ujenzi huo ikiwemo kuzifanyia kazi kasoro zilizobainishwa ili kuhakikisha kwamba ujenzi huo unamaliza kwa wakati na kwa kiwango kinachotarajiwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Mchanganuo wa ongezeko hilo ni kama inavyoonekana katika barua hapo chini:-

RANS Building & Civil Contractor

**RANS COMPANY LIMITED**
P.O.BOX - 3267 Zanzibar, Tanzania.
Head Office - Dimani.
Mobile : +255 777 469691 / +255 777 426670
Email : info@rans.co.tz | Website : www.rans.co.tz
BANKER - THE PEOPLE'S BANK OF ZANZIBAR LIMITED

Ref: R/MOH/CMCH/16 Thu. 29th July 2021.

COORDINATOR,
ZANZIBAR BUILDING AGENCY,
CHAKE CHAKE – PEMBA.

**REF: PROPOSED CONSTRUCTION OF MOTHER AND CHILD BUILDING AT CHAKE CHAKE – PEMBA. (SMZ/H01/W/NCB/2018/2019/13).**

**SUB: ADDITIONAL WORKS.**

Your letter dated 16th July 2021 regarding the above subject refers.

Along with this letter, please receive the following quotations for works requested and agreed in the last site meeting of Saturday 24th July 2021 for your approval:

1. Gas Installation; TZS 416,000,000/- excluding VAT.
2. ICT Installation; TZS 183,300,000/- excluding VAT.
3. Plumbing works; TZS 51,240,000/- excluding VAT.
4. Electrical works; TZS 51,407,000/- excluding VAT.
5. Plaster works; TZS 52,750,000/- excluding VAT.
6. Floor finish; TZS 54,550,000/- excluding VAT.
7. Firefighting Installation; TZS 8,400,000/- excluding VAT.
8. Stairs; TZS 42,762,000 excluding VAT.
9. Ramp and Bridge; 51,040,000/- excluding VAT.
10. Handrails to Balconies; TZS 22,050,000/- excluding VAT.
11. Aprons; TZS 3,135,000/- excluding VAT.
12. Doors, Windows and Grills; TZS 182,560,000/- excluding VAT.
13. Courtyard Toilets; TZS 162,145,000/- excluding VAT.
14. Rear toilets; to be used for ICT and GAS works; TZS 25,236,000/- excluding VAT.

Thanking you again,

Sincerely yours,

29.07.2021

Ali Nassor Al-Miskiry,
Managing Director,
RANS CO LTD.

Your Contractor

#### 6.3.1.4 Kutokuainishwa kwa baadhi ya kazi katika BOQ

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba baadhi ya kazi ambazo zimeainishwa katika ramani ya ujenzi kwa mujibu wa mkataba wa awali hazikuoneshwa uhalisia wake katika BOQ. Kutokuonekana kwa ongezeko la baadhi ya kazi katika BOQ iliyowasilishwa kumepelekea kujitokeza kwa ongezeko la gharama kwa kazi za ziada ambazo zilihitajika kutekelezwa kwa mujibu wa matakwa ya mradi huo. Kwa mujibu wa barua yenye kumbu kumbu namba R/MOH/CMCH/16 ya tarehe 26/7/2021 iliyonakili makubaliano ya ongezeko ya kazi za ziada kwa mujibu wa kikao kilichofanyika tarehe 24/7/2021 kilibainisha jumla ya kazi kumi na nne zilizoongezeka zenye thamani ya shilingi 1,306,575,000.

Dosari ya ukaguzi iliobainika ni kushindwa kufunga mkataba mpya kutokana na mkataba wa awali umekiuka taratibu za kisheria.

#### 6.3.1.5 Kutokukamilika Mradi kwa wakati

kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba wa ujenzi wa awali baina ya Wizara ya Afya na Mkandarasi RANS CO.LTD kwa mujibu wa mkataba wenye kumbu kumbu namba SMZ/HO1/W/NCB/W/2018/2019/13 mkandarasi alitakiwa kukamilisha mradi huo ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili kuanzia tarehe 01/06/2020 hadi 01/06/2021. Hadi ukaguzi unakamilika mradi huo bado haujakamilika, kutokukamilika kwa mradi huo kwa wakati kunaweza kukapelekea kushindwa kutekelezeka kutokana na kuongezeka kwa thamani ya vifaa vya ujenzi siku hadi siku jambo ambalo litapeleka kukosekana kwa tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya ni vyema kubuni miradi michache ambayo watakuwa na uwezo wa kuitekeleza kwa wakati ili kunusuru upotevu wa fedha za umma unaotokana na ongezeko la thamani ya dola kwa shilingi.

#### 6.3.1.6 Kutokulipwa kwa Fedha za Mshauri Elekezi shilingi 25,705,120

Kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba baina ya Wizara ya Afya na Mshauri elekezi ambaye ni msimamizi wa jengo la mama na mtoto la hospitali ya Chake Chake Pemba imebainika makubaliano ya gharama ya usimamizi wa ujenzi huo ni shilingi 36,721,000 ambazo zilitakiwa kulipwa kwa awamu mbali mbali kama mkataba unavyoonesha.

Ukaguzi umebaini kutokulipwa kwa fedha za mshauri elekezi kwa malipo ya awamu mbili (2) tofauti zenye thamani ya shilingi 25,705,120 na kunapelekea kujitokeza kwa usimamizi usioridhisha wa kazi ya ujenzi, jambo ambalo huenda likapelekea utekelezaji wa mradi huo kutotekelezwa kwa wakati au kutekelezwa chini ya kiwango cha makubaliano.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha hatua za haraka zinachukuliwa za kumlipa mshauri elekezi kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba wao kwa lengo la kunusuru kujitokeza kutokufahamiana na kuzorotesha maendeleo ya mradi.

SURA YA SABA

# 7.0 MIRADI ILIYOTEKELEZWA KATIKA SEKTA ZA MIUNDOMBINU NA NISHATI

## 7.1 MRADI WA UIMARISHAJI WA SEKTA YA UMEME ZANZIBAR

Idara ya Nishati na Madini (DoEM) ndani ya Wizara ya Ardhi, Maji, Mazingira na Nishati (MLWEE) ina jukumu la kusimamia masuala ya nishati Zanzibar.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika barua ya Oktoba 2013 kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati imewasilisha ombi kwa Ubalozi wa Sweden kuhusu ufadhili wa mapendekezo ya awamu ya pili ya Mpango wa Sekta ya Nishati Zanzibar hali iliyotokana na Sweden ilipendekezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuchangia katika kuimarisha utawala, uratibu, utendaji wa fedha, ufanisi wa nishati na uwezo wa usimamizi katika sekta ya nishati Zanzibar kupitia ufadhili wa Awamu ya Uimarishaji wa Sekta ya Nishati Zanzibar, mradi namba 51170007 kuanzia Agosti 2014 hadi Juni 2019.

Mnamo tarehe 6 Agosti, 2014 Sweden kupitia Shirika la maendeleo ya kimataifa la Sweden na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliingia makubaliano ya kutekeleza Mradi unaojulikana kwa jina la "The Zanzibar Energy Sector Consolidation Phase".

Katika makubaliano hayo Sweden imetoa jumla ya SEK 47 milioni zitakazotumika mahususi kufadhili mradi huo katika kipindi kilichopangwa na kukubaliwa kuanzia mwaka wa fedha 2014 hadi mwaka 2019.

### 7.1.1 MALENGO YA MRADI

Lengo kuu la mradi ni kuimarisha sekta ya nishati Zanzibar ili kuondokana na mgao wa umeme Zanzibar na kuchangia ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kijamii kama:-

i) Kuongeza uwezo na utendaji wa Idara ya Nishati na Madini katika jukumu lake la kuratibu sekta ya nishati.

ii) Kuboresha mapato ya Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO)

iii) Kutumia nishati kwa njia endelevu zaidi Zanzibar.

### 7.1.2 VYANZO VYA FEDHA ZA MRADI

Wizara ya Ardhi, Maji, Mazingira na Nishati kupitia mradi wa uimarishaji wa sekta ya umeme Zanzibar ilikadiriwa kupata msaada wa jumla ya SEK 47,000,000 kutoka katika Shirika la maendeleo la kimataifa la Sweden fedha ambazo zitatumika katika kipindi cha miaka mitano ya mradi kuanzia mwaka 2014 hadi 2019 kwa ajili ya kutekeleza mradi huo lakini katika utekalezaji wa mradi huu muda wa utekelezaji uliengezwa tena kutoka mwaka 2019 hadi mwaka 2021.

Shirika la maendeleo ya kimataifa la Sweden hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 lilifanikiwa kutoa jumla ya SEK 5,000,000 kwa ajili ya kuendeleza mradi huu.

### MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI

#### 7.1.2.1 Malipo yaliyofanyika kinyume na taratibu shilingi 127,721,007

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 127,721,006.80 zimetumika kwa ajili wa ununuzi wa Sergeflex 32 cable fault distance location kwa kutumia hati namba Sera 01/09/2019 ya tarehe 04/09/2019, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutofuatwa kwa utaratibu wa kushindanisha zabuni ili kuweza kumpata mzabuni aliyekizi vigezo kwa mujibu wa Sheria.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kupatikana kwa mzabuni aliyekosa sifa kuweza kufanya kazi na Serikali pamoja na upatikanaji wa bidhaa kwa thamani kubwa na zilizo chini ya kiwango ambapo ni kwenda kinyume na Kifungu cha 72(2) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa unasimamia ipaswavyo utaratibu mzima wa manunuzi katika kushindanisha zabuni zinazofanywa chini ya utekelezaji wa miradi kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo ili kuepusha upatikanaji wa wazabuni ambao hawafai katika usambazaji wa bidhaa na utoaji wa huduma zinazotakikana katika miradi ya Serikali.

#### 7.1.2.1 MRADI WA KUSAIDIA SEKTA YA UCHUKUZI (TSSP)

Mradi wa kusaidia Sekta ya Uchukuzi (Transport Sector Support Project -TSSP) ni mradi unaotekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar ambao unahusika na Sekta

ndogo za barabara na reli na anga Nchini ambapo utekelezaji wa mradi huu ulianza rasmi tarehe 27 Mei 2016. Mradi huu kupitia Katika sekta ndogo ya barabara umehusika kufanya kazi zifuatazo:-

(a) Kazi za kiraia za ukarabati/uboreshaji wa baadhi ya kilomita 462 za barabara kwa kiwango cha lami Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar.

(b) Huduma za ushauri kuhusiana na kazi za barabara na masomo ya barabara;

(c) Kujenga uwezo.

(d) Ulipaji wa Fidia na utoaji wa makazi mapya.

(e) Kufanya utekelezaji wa miundombinu ya kijamii.

Miongoni mwa watekelezaji wa mradi huu ni Wakala wa barabara Tanzania (TANROADS) na Wizara ya Miundombinu, Mawasiliano na Uchukuzi (MOICT) zinazotekeleza majukumu yake Tanzania Bara na Zanzibar kwa pamoja.

## 7.2 MALENGO YA MRADI

Lengo kuu la mradi ni kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kupunguza umaskini na ushirikiano wa kikanda kupitia mfumo bora wa usafiri unaounganisha shughuli za kiuchumi za Nchi. Madhumuni mahususi ya mradi ni kuboresha miundombinu ya usafiri Zanzibar ili kupunguza gharama za uendeshaji wa magari na muda wa usafiri katika viunganishi vya barabara zilizolengwa na kukuza ushirikiano wa kikanda kwa kuboresha huduma za usafiri.

### 7.2.1 TAARIFA YA FEDHA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MRADI

#### Taarifa ya Mapato na Matumzi

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 programu ilifungua bakaa ya fedha shilingi 299,213.75, ambapo mradi wa TSSP ulipokea fedha kutoka ADB jumla ya shilingi 12,996,637,761.25 na kufanya jumla ya fedha zilizopatikana kwa ajili ya utekelezaji mradi ni shilingi 12,996,936,975 na fedha halisi ambazo ziltumika ni shilingi 12,119,848,999.84 na kupelekea uwepo wa bakaa la mwisho la shilingi 384,336,090.60. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyonekana katika jadweli hapo hapo chini:-

**Jadweli Nambari 41 : Uingiaji wa fedha za mradi**

| Maelezo | Kiasi cha fedha za mradi (Tshs) |
|---|---|
| Salio anzia 1 Julai,2020 | 299,213.75 |
| **Fedha zilizopokelewa:** | |
| Benki ya maendeleo ya Afrika (ADB) | 12,996,637,761.25 |
| Mchango wa Serikali | |
| Jumla ya fedha iliyopokelewa | 12,996,637,761.25 |
| **Jumla ya fedha iliyopatikana** | 12,996,936,975 |
| Matumizi kwa 2020/2021 | 12,119,848,999.84 |
| Salio la mwisho 30Juni,2021 | 384,336,090.60 |

### 7.2.3 VIPENGELE VYA MRADI

Mradi huu unahusika katika sekta ndogo za barabara na usafiri wa anga Zanzibar, katika sekta ndogo ya barabara imekusudiwa kukarabati kilomita 31 za barabara za lami (Bububu-Mahonda-Mkokotoni) na kuboresha kilomita 21 za barabara za changarawe (barabara tatu za miji ya Pale-Kiongele, Matemwe-Muyuni na Fuoni-Kombeni) kwa kiwango cha lami. Katika sekta ndogo za usafiri wa anga, mradi una vipengele vya utafiti ili kuendeleza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kiwanja cha Ndege cha Pemba na kutayarisha mpango mkuu wa kiwanja cha Ndege cha Zanzibar.

### MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI

#### 7.2.3.1 Kutotumika kwa fedha za mradi Dola za Kimarekani USD 166,469.25

Katika ukaguzi uliyofanyika imebainika kuwa Wizara ya Miundombinu, Mawasiliano na Uchukuzi imepokea jumla ya dola za kimarekani 166,469.25 kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumishi mbali mbali wa Wizara lakini fedha hizo hazikutumika kama ilivyokusudiwa hali iliyopelekea kutokukamilika kwa vipengele vya utekelezaji wa mradi huo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Miundombinu, Mawasiliano na Uchukuzi kuhakikisha kwamba fedha zote zilizopangwa kwa ajili ya utekelezaji mradi zinatumika kulingana na bajeti iliyoidhinishwa ili kuepusha uwezekano wa kufanyika kwa matumizi kinyume na utaratibu.

### 7.2.3.2 Kutokulipwa kwa fidia kwa wananchi walioathirika na utekelezaji wa mradi (PAP) shilingi 188,486,250

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 188,486,250 ni fedha mbazo zingepaswa kulipwa kwa ajili ya fidia kwa watu walioathirika na mradi (PAP) ambapo dosari iliobainika na ukaguzi ni kutokulipwa kwa fedha hizo kwa watu hao hali mabyo inaweza kupelekea kuwepo kwa migogoro miongoni mwa wananchi na Serikaliambapo kunaweza kukapelekea viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma

Ukaguzi unashauri Wizara ya Miundombinu, Mawasiliano na Uchukuzi (MOICT) kuhakikisha kwamba inafanya malipo ya fidia kwa mujibu wa ripoti ya Mtathmini Mkuu kwa wananchi walioathirika na mradi (PAPs) ili kuepusha atahari zinazoweza kujitokeza.

Mchanganuo wa wananchi waliyoathirika kupitia mradi huo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 42 : Orodha ya fidia za waliothirika na mradi (PAA)**

| PALE - KIONGELE (4.6 KM) ROAD | | | |
|---|---|---|---|
| Tathmini ya Mazao | | | |
| **Namba** | **Jina** | **Shehia** | **Kiasi cha fedha kilichostahiki Kulipwa (Tshs)** |
| 1. | Kombo Ubwa Juma | Pale | 1,125,000 |
| 2. | Hadia Foum Khamis | Pale | 2,130,000 |
| 3. | Salum Foum Khamis | Pale | 735,000 |
| 4. | Riziki Ali Amour | Pale | 625,500 |
| 5. | Amour Ali Amour | Pale | 3,475,000 |
| 6. | Ngwali Kona Kheir | Pale | 389,500 |
| 7. | Tatu Moh'd Makame | Pale | 2,165,000 |
| 8. | Patima Jamal Foum | Pale | 142,500 |
| 9. | Kombo Hakim Makame | Pale | 933,000 |
| 10. | Moh'd Juma Ussi | Pale | 2,265,000 |
| 11. | Said Mossi Makame | Pale | 2,425,000 |
| 12. | Kassim Machano Jaml | Pale | 706,500 |
| 13. | Abudu Makame Abudu | Pale | 13,185,000 |
| 14. | Khamis Khamis Makame | Pale | 1,630,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 15. | Khamis Ali Khamis | Pale | 978,000 |
| 16. | Ali Hamdu Makame | Pale | 616,500 |
| 17. | Mwajuma Juma Ussi | Pale | 447,000 |
| 18. | Khamis Juma Ussi | Pale | 1,253,500 |
| 19. | Ali Ussi Nyange | Pale | 834,500 |
| 20. | Shaib Makame Mashaka | Pale | 427,500 |
| 21. | Machano Mkinai Khamis | Pale | 399,000 |
| 22. | Muhamadi Ali Hamdu | Pale | 565,500 |
| 23. | Mboja Ali Hamdu | Pale | 3,085,000 |
| 24. | Mboja Muhammed Makame | Pale | 624,000 |
| 25. | Patima Makame Mossi | Pale | 2,860,500 |
| 26. | Haji Saburi Mtwana | Pale | 900,000 |
| 27. | Haji Haji Chetu | Pale | 631,500 |
| 28. | Nyange Hassan Kombo | Pale | 978,000 |
| 29. | Mda Saleh Haji | Pale | 465,500 |
| 30. | Mgeni Vuai Kheir | Pale | 760,000 |
| 31. | Ussi Jamal Foum | Pale | 315,000 |
| 32. | Mashavu Mrisho Omar | Pale | 1,017,000 |
| 33. | Zubeir Juma Abushiri | Mkwajuni | 750,000 |
| 34. | Kombo Simai Juma | Mkwajuni | 322,500 |
| 35. | Suleiman Mtwana Khamis | Mkwajuni | 100,000 |
| 36. | Khamis Nuhu Muhamadi | Mkwajuni | 496,000 |
| 37. | Ali Vuai Kona | Mkwajuni | 589,000 |
| 38. | Silima Hassan Silima | Mkwajuni | 1,212,500 |
| 39. | Bakari Khamis Ali | Kivunge | 250,000 |
| 40. | Bakari Zamir Bakari | Mkokotoni | 113,000 |
| 41. | Zakia Ali Makame | Mkokotoni | 75,000 |
| 42. | Jabir Bakari Jabir | Mkokotoni | 75,000 |
| 43. | Kombo Hakim Makame | Mkokotoni | 266,500 |
| 44. | Khamis Bakari Ali | Mkokotoni | 225,000 |
| 45. | Bakari Ali Makame | Mkokotoni | 225,000 |
| 46. | Mariam Shaabani Mohd | Mbaleni | 1,046,000 |
| 47. | Mchuzeni Khamis Juma | Kwagube | 450,000 |
| 48. | Masoud Kombo | Kikombweni | 325,000 |
| 49. | Khamis Haji Khamis | Kikombweni | 2,875,000 |
| 50. | Kassim Ali | Kikombweni | 652,000 |
| 51. | Nasoro Khamis Said | Kikombweni | 1,375,000 |
| 52. | Ega Shaame Khamis | Pale | 114,000 |
| 53. | Juma Ayubu Juma | Pale | 95,000 |
| 54. | Mgeni Vuai Kheir | Pale | 142,500 |
| 55. | Bimkubwa Said Khamis | Pale | 326,500 |
| 56. | Mashaka Makame Mashaka | Pale | 125,000 |
| 57. | Moh'd Juma Ussi | Pale | 592,000 |
| | **Jumla** | | **61,907,500** |

| PALE - KIONGELE (4.6 KM) ROAD | | | |
|---|---|---|---|
| **Tathmini ya Nyumba** | | | |
| **Namba** | **Jina** | **Shehia** | **Kiasi alichostahiki kulipwa (Tshs)** |
| 1 | Salum Fumu Khamis | Pale | 9,200,000 |
| 2 | Khamis Fumu Khamis | Pale | 9,200,000 |
| 3 | Hadiya Fumu Khamis | Pale | 9,600,000 |
| 4 | Bakari Kheri Haji | Pale | 7,300,000 |
| 5 | Ali Mgwali Kona | Pale | 3,000,000 |
| 6 | Machano Mkinai Khamis | Pale | 3,000,000 |
| 7 | Ngwali Kheri Haji | Pale | 300,000 |
| 8 | Amina Miraji Haji | Mfenesini | 11,000,000 |
| 9 | Balozi Maskani | Mfenesini | 8,000,000 |
| 10 | Makame Mosi Makame | Pale | 400,000 |
| 11 | Juma Haji Khamis | Pale | 70,000 |
| **Jumla** | | | **61,070,000** |
| **FUONI - KOMBENI (8.56 KM) ROAD** | | | |
| **TATHMINI YA NYUMBA NA VIPANDO** | | | |
| **Namba** | **Jina** | **Shehia** | **Kiasi cha Fedha (Tshs)** |
| 1. | Ahmed Mbarak Matar | Fuoni | 7,567,000 |
| 2. | Kassim Khamis Ali | Kombeni | 5,341,750 |
| 3. | Khamis Suleiman Mwalim | Kombeni | 52,600,000 |
| **Jumla** | | | **65,508,750** |

### 7.2.3.3 Dosari zilizobainika katika utekelezaji wa miradi ya Barabara

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa shughuli za ujenzi wa barabara kupitia mradi wa kusaidia Sekta ya Uchukuzi (TSSP) zimetekelezwa lakini dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuchakaa kwa alama za barabarani (Bububu-Mahonda –Mkokotoni na Bububu Police – Kwanyanya Junction) hali inayopelekea uwezekano wa kukosekana kwa ufanisi wa madereva wanaotumia barabara hiyo. Hali halisi ya utekelezaji wa mradi huo ni kama inavyoonekana katika picha za hapo chini.

**Ukarabati wa barabara ya Bububu-Mahonda – Mkokotoni, 31.0 km**





**Ukarabati wa bara bara ya Fuoni – Kombeni, 8.59 Km**





**Ukarabati wa bara bara ya Bububu Police – Kwanyanya Junction, 2.80 Km**



